**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**2020 - 2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | **Mhe. Zubeir Ali Maulid** | - | **SPIKA** |
| 2. | **Mhe. Mgeni Hassan Juma** | - | **Naibu Spika/Nafasi za Wanawake** |
| 3. | **Mhe. Mwanaasha Khamis Juma** | - | **Jimbo la Dimani** |
| 4. | **Mhe. Shaaban Ali Othman** | - | **Jimbo la Mpendae** |
| 5. | **Mhe. Hemed Suleiman Abdulla** | - | **MBM/Makamu wa Pili wa Rais/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais** |
| 6. | **Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman** | - | **MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji/ Jimbo la Bububu.** |
| 7. | **Mhe. Masoud Ali Mohammed** | - | **MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Ole.** |
| 8. | **Mhe. Haroun Ali Suleiman** | - | **MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora/Jimbo la Makunduchi.** |
| 9. | **Mhe. Jamal Kassim Ali** | - | **MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Fedha na Mipango/Jimbo la Magomeni.** |
| 10. | **Mhe. Dkt Khalid Salum Mohamed** | - | **MBM/Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi/Jimbo la Donge.** |
| 11. | **Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan** | - | **MBM/Waziri wa Kilimo,** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo/Jimbo la Paje |
| 12. Mhe. | Simai Mohammed Said | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Tunguu |
| 13. Mhe. | Tabia Maulid Mwita | - | MBM/Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. | Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi/ Nafasi za Wanawake |
| 15. Mhe. | Rahma Kassim Ali | - | MBM/Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi/Nafasi za Wanawake |
| 16. Mhe. | Suleiman Masoud Makame | - | MBM/Waziri wa Maji, Nishati na Madini/Jimbo la Chonga |
| 17. Mhe. | Abdulla Hussein Kombo | - | MBM/Waziri wa Uchumi wa Bluuu na Uvuvi /Jimbo la Mkoani |
| 18. Mhe. | Lela Muhamed Mussa | - | MBM/Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale/Nafasi za Wanawake |
| 19. Mhe. | Abdalla Abasi Wadi | - | Jimbo la Nungwi |
| 20. Mhe. | Ali Abdulgulam Hussein | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 21. Mhe. | Ali Suleiman Ameir | - | Jimbo la Pangawe |
| 22. Mhe. | Ameir Abdalla Ameir | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 23. Mhe. | Anna Athanas Paul | - | Uteuzi wa Rais |
| 24. Mhe. | Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Mahonda |
| 25. Mhe. | Azza Januar Joseph | - | Nafasi za Wanawake |
| 26. Mhe. | Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 27. Mhe. | Bakar Hamad Bakar | - | Jimbo la Wawi |
| 28. Mhe. | Bihindi Hamad Khamis | - | Nafas iza Wanawake |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 29. | Mhe. | Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) | | Nafasi za Wanawake |
| 30. | Mhe. | Habibu Ali Muhamed | - | Jimbo la Mtambwe |
| 31. | Mhe. | Haji Omar Kheri | - | Jimbo la Tumbatu |
| 32. | Mhe. | Haji Shaaban Waziri | - | Jimbo la Uzini |
| 33. | Mhe. | Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Kwamtipura |
| 34. | Mhe. | Harusi Said Suleiman | - | Jimbo la Wete |
| 35. | Mhe. | Hassan Hamad Omar | - | Jimbo la Kojani |
| 36. | Mhe. | Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 37. | Mhe. | Hudhaima Mbarak Tahir | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. | Mhe. | Hussein Ibrahim Makungu | - | Jimbo la Mtoni |
| 39. | Mhe. | Juma Makungu Juma | - | Jimbo la Kijini |
| 40. | Mhe. | Juma Ali Khatib | - | Uteuzi wa Rais |
| 41. | Mhe. | Issa Haji Ussi Gavu | - | Jimbo la Chwaka |
| 42. | Mhe. | Kombo Mwinyi Shehe | - | Jimbo la Wingwi |
| 43. | Mhe. | Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 44. | Mhe. | Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 45. | Mhe. | Mihayo Juma Suleiman | - | Jimbo la Mwera |
| 46. | Mhe. | Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 47. | Mhe. | Mohamed Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 48. | Mhe. | Mohamed Ahmada Salum | - | Jimbo la Malindi |
| 49. | Mhe. | Mtumwa Peya Yussuf | - | Jimbo la Bumbwini |
| 50. | Mhe. | Mussa Foum Mussa | - | Jimbo la Kiwani |
| 51. | Mhe. | Mwanaidi Kassim Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 52. | Mhe. | Mwantatu Mbarak Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 53. | Mhe. | Mwanajuma Kassim Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 54. | Mhe. | Dkt. Mwinyi Talib Haji | - | Mwanasheria Mkuu |
| 55. | Mhe. | Nadir Abdullatif Yussuf | - | Jimbo la Chaani |
| 56. | Mhe. | Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 57. | Mhe. | Nassor Ahmed Mazrui | - | Uteuzi wa Rais |
| 58. | Mhe. | Omar Said Shaaban | - | Uteuzi wa Rais |
| 59. | Mhe. | Panya Ali Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 60. | Mhe. | Rukia Omar Ramadhan | - | Jimbo la Amani |
| 61. | Mhe. | Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafasi za Wanawake |
| 62. | Mhe. | Dkt. Saada Mkuya Salum | - | Uteuzi wa Rais |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 63. Mhe. | Saidi Saleh Salim | - | Jimbo la Tumbe |
| 64. 5Mhe. | Sabiha Filfil Thani | - | Nafasi za Wanawake |
| 65. Mhe. | Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |
| 66. Mhe. | Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |
| 67. Mhe. | Suleiman Makame Ali | - | Jimbo la Ziwani |
| 68. Mhe. | Suleiman Haroub Suleiman | - | Jimbo la Kiembe Samaki |
| 69. Mhe. | Sulubu Kidongo Amour | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 70. Mhe. | Shadya Mohamed Suleiman | - | Nafasi za Wanawake |
| 71. Mhe. | Shamata Shaame Khamis | - | Jimbo la Micheweni |
| 72. Mhe. | Shaib Hassan Kaduara | - | Jimbo la Chake Chake |
| 73. Mhe. | Yahya Rashid Abdulla | - | Jimbo la Kwahani |
| 74. Mhe. | Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 75. Mhe. | Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 76. Mhe. | Zawadi Amour Nassor | - | Jimbo la Konde |

| | | |
|---|---|---|
| Ndg. Raya Issa Msellem | - | Katibu |

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**BARAZA LA KUMI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 10 Februari, 2021**

*(Kikao kilianza Saa 3.00 asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

**DUA**

**TAARIFA YA SPIKA**

**KIAPO CHA UAMINIFU CHA WAHESHIMIWA WAJUMBE WA BARAZA**

Mhe. Habib Ali Mohamed

Mhe. Hassan Hamad Omar

Mhe. Kombo Mwinyi Shehe

Mhe. Nassor Ahmed Mazurui

Mhe. Omar Said Shaaban

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 13 Novemba , 2020.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Ripoti ya Utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2019 – 2020.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2018 – 2019.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka 2018 – 2019.

Mhe. naomba kuwasilisha hati mezani, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2018 – 2019.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Marekebisho ya Jadweli ya Pili ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar Nam. 4 ya 2015.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa:** Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa kazi za Tume za Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2019 – 2020. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mwenyekiti wa Kamati ta Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Mashirika na Serikali za Mitaa:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Mashirika na Serikali za Mitaa kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2018 – 2019 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka 2018 – 2019. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Asha Abdalla Mussa (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali):**Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhubiti Hesabu za Serikali naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kwa Mawizara kuhusu Uwasilishwaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:** Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuwaweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Marekebisho ya Jadweli ya Pili ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar Nam. 4 ya 2015. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea nalazimika kusimama nitoe tangazo la kifo. Mhe. Salma Mussa Bilal Mwakilishi wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kusini Unguja anasikitika kutangaza kifo cha mama yake mzazi Bi. Mwanajuma Ramadhan Mussa kilichotokea leo alfajiri katika hospitali ya MnaziMMoja na mazishi yatakuwa leo saa nane mchana Uzini. Mungu ailaze roho ya marehemu pahala pema na wafiwa awape subra. Baada ya tangazo hilo sasa naomba nimuite Katibu kwa shughuli inayofuata.

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 2

### Ahadi ya Kutiwa Kifusi Barabara ya Kijiji cha Andikoni Shehia ya Shumbageni

**Mhe. Bahati Khamis Kombo - ** Aliuliza:-

Kumekuwa na ahadi ya Mhe. Makamuwa Pili wa Rais katika Kijiji cha Andikoni Shehia ya Shumbageni kuwasaidia fedha taslim millioni mbili (2,000,000/-) kwa ajili ya kutiliwa kifusi barabara yao lakini hadi sasa bado ahadi hii haijatekelezwa.

(a) Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa.

(b) Na kama fedha hizo zimeshatolewa, basi bado wananchi hawa hazijawafika, nihatua gani zitachukuliwa juu ya mtu ambae amekabidhiwa fedha hizo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi –** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na kabla ya kumjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo, mwakilishi wa Jimbo la Chambani swali lake namba 2 lenye vifungu (a) na (b). Naomba kutanguliza maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, nakiri kwamba aliyekuwa Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi aliahidi kutoa shilingi milioni mbili (2,000,000) ili zitumike katika uwekaji wa kifusi katika barabara ya kijiji cha Sisimizini hadi kijiji cha Andikoni. Vyote hivyo viko katika Shehia ya Chumbageni Wilaya ya Mkoani Pemba. Mhe. Spika, ahadi hiyo aliitoa wakati wa ziara yake ya kutembelea mashamba ya mikarafuu yaliopo katika wilaya hiyo tarehe 8 Juni 2014. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo swali lake lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ahadi hii itatekelezwa katika mwaka wa fedha 2021 – 2022 kwa serikali kujenga barabara hiyo ya Sisimizini hadi Andikoni kwa kiwango cha kifusi, hii kwa sababu thamani ya shilingi milioni mbili kwa sasa haitoweza kukidhi madhumuni yaliokusudiwa ya wakati huo ya kuweka kifusi katika barabara hiyo. Mhe. Spika, tunaamini kupitia barabara hiyo wananchi watafaidika zaidi kwa kuitumia kufikia katika mashamba yao lakini pia kusafirishia mazao yao pamoja na kuitumia kwa harakati zao za kiuchumi na kijamii.

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana aliowapa matumaini mazuri wananchi wa Andikoni. Naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri umekiri kuwepo kwa ahadi hii na muda sasa umekuwa mkubwa tokea 2014 mpaka 2021, je upo tayari kwenda kwa pamoja tukaona ile kadhia ambayo inawapata wananchi wa Andikoni.

**Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba ni muda ni mrefu 2014 hadi leo lakini hiyo imetokana na kwamba shughuli zinazohitajika za ujenzi wa barabara ni nyingi katika visiwa vya Unguja na Pemba na zote ni muhimu lakini huwa zinapangiliwa kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha kuna ahadi zilizotolewa na viongozi, lakini kuna barabara zilizopangwa kujengwa kwa mujibu wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini vile vile kwa mujibu wa mipango ya Serikali na hii inatokana na *Transport Master Plan* iliyopo katika nchi hii. Sasa kuchelewa huko sio kwa makusudi lakini kulitokana na kwamba shughuli ni nyingi na zinawekewa kipaumbele kadri ya hali ya upatikanaji wa fedha inavyoruhusu. Sasa mimi niko tayari kufuatana na wewe lakini pia

na waziri anayehusika kutembelea katika eneo hilo na kwa hapa Waziri anayehusika ni wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mhe. Spika:** Ahsante nimekuona Mhe. Suleiman Makame Ali kwa swali la nyongeza.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri, Mhe. Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Makamu wa Kwanza wanapokwenda katika maeneo yetu Kiwilaya, Kimkoa hasa majimbo wanafuatana na magari mengi nyuma zaidi ya mia moja, kila gari ina watu wanaofika pengine watano mpaka sita. Lakini ahadi hizo zinazowekwa Mhe. Waziri huwa ni usufi unapeperuka, mfano jimboni kwangu kuna ahadi za tokea mwaka 2007.

Je, Mhe. Waziri nataka kujua kwamba wote wale wanaofuatana na Mhe. Rais au Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tuseme kasahau, je wale na wao wanasahau na nani hasa anaratibu ahadi zile kuhakikisha kwamba zinatekelezwa kwa wakati.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza hakuna ahadi inayotolewa na kiongozi ambayo inasahauliwa ahadi zote zimeorodheshwa na zipo na zinaratibiwa vizuri, lakini kama nilivyosema wakati najibu suala mama ni kwamba ahadi zinakuwa wakati nyengine ni nyingi na viongizi wetu wanapotembelea kwa wananchi wanatoa matatizo yao na viongozi wanayachukua, lakini hapo hapo tujue kwamba kuna vipaumbele ambavyo vimepangwa na Serikali katika kutekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, sasa zote kwa pamoja hizo zimewekewa mpango wa utekelezaji na sio jimboni kwake tu majimbo yote yapo katika hali hiyo hiyo.

Lakini niseme tu kwamba ahadi zote zipo na zitatekelezwa kadri hali itakavyoruhusu kifedha.

**Nam. 24**

**Juhudi za Ukuzaji na Uendeshaji wa Miskiti na Madrasa**

**Mhe. Saada Mkuya Salum (Kny. Salma Mussa Bilal)** – Aliuliza:

Naipongeza Serikali kupitia Ofisi ya Mufti kwa kufanya usajili wa madrasa na misikiti hapa Zanzibar.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha misikiti na madrasa zoteza Zanzibar zinasajiliwa.

(b) Je, Wizara ina ratiba maalum ya kuhakikisha inatembelea na kuangalia changamoto zinazowakabili na kuzisaidia madrasa na misikiti hiyo.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuziwekea mtaala madrasa hizo ili ziweze kusomesha katika mtaala mmoja kwa manufaa ya watoto wetu.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi naUtawala Bora** - Alijibu:

Mhe. Spika, awali ya yote kabla ya kujibu swali namba 24 la Mhe. Mwakilishi, naomba kuchukua nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kazi nzuri aliyofanya kwa kuleta maridhiano katika nchi yetu, aidha niwashukuru Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili lakini pia niwashukuru wajumbe wenzetu watano walioapishwa leo asubuhi na kuwatakia kila la kheri, karibuni na tuko tayari kushirikiana nao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kumjibu Mhe. Salma Mussa Bilali swali lake Nam. 24 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Ofsisi ya Mufti wa Zanzibar imepanga kufanya uhakiki wa Misikiti na Madrasa zote za Zanzibar ili kuhakikisha kuwa Misikiti na Madrasa zote zinasajiliwa kwa mujibu wa Sheria na taratibu. Kwa sasa Ofisi ya Mufti tayari imeshafanikiwa kufanya uhakiki wa Madrasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kaskazini Unguja na zoezi la uhakiki huo linaendelea kwa Mkoa wa Kusini Unguja na Mikoa ya Pemba. Jumla ya misikiti 817 na Madrasa 1011 imekaguliwa katika Mkoa wa Mjini Maghribi na Misikiti 466 na madrasa 477 kwa uapande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Uhakiki huo umebaini kuwa Madrasa nyingi za Mkoa wa Mjini Magharibi zimesajiliwa na baadhi hazijasajiliwa na hivyo kupelekea Ofisi ya Mufti kushajihisha Uongozi wa Madrasa hizo kuharakisha kufanya usajili kwa mujibu wa Sheria.

(b) Ofisi ya Mufti wa Zanzibar imepanga utaratibu wa kufanya ukaguzi wa Misikiti na Madrasa mara mbili kwa wiki ili kubaini matatizo yanayozikabili Madrasa hizo na kuyapatia ufumbuzi matatizo hayo kwa kushirikiana na wananchi wenyewe.

(c) Mhe Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Mufti wa Zanzibar imezingatia maoni na ushauri kwa wahusika mbali wakati wa matayarisho wa mitaala ya madrasa na tayari imeshaanda mtaala huo ili kuziwezesha madrasa hizo kusomesha kwa kutumia mtaala mmoja kwa manufaa ya watoto wetu, aidha Ofiti ya Mufti Zanzibar bado inaendelea na taratibu za uidhinishwaji wa Mtaala huo kwa kukaa pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwaajili ya kupata Baraka zake na hatimae kuuzindua rasmi Mtaala huo na kuanza kutumika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Saada Mkuya Salum kwa swali la nyongeza.

**Mhe. Saada Mkuya Salum:** Ahsante sana Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake ya kina, lakini pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza:

Mhe. Spika, usajili unaofanyika uwe kwa mujibu wa utaratibu na sheria, lakini kama Mhe. Waziri alivyokuwa amezungumza ni kwamba amebainisha changamoto mbali mbali ambazo

zinatokana na mambo yaliyopo kwenye misikiti hiyo pamoja na madrasa, Serikali inajipanga vipi kuhakikisha kwamba Madrasa zetu hususan pamoja na misikiti inapata *incentive* kwa ajili ya hususan kutoa huduma za jamii.

Kwa mfano watoto wanalelewa katika madrasa zetu lakini utakuta madrasa nyengine hazina maji, hazina vyoo wala hazina umeme, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba madrasa hizo zinasaidiwa.

Lakini swali la pili kuhusiana na mitaala ni kwa kiasi gani mtaala huo unatoa fursa kwa madrasa zetu pamoja na misikiti kuongeza masomo ya ziada, tunajua kutakuwa kuna mtaala mmoja lakini vile vile kuna fursa ambazo zinapatikana katika kuongeza masomo ya ziada ambayo yatanufaisha jamii, kwa kiasi gani mtaala huo unatoa fursa hizo.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Saada Mkuya Salum swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Suala la kuhudumia Misikiti na Madrasa ni zito kidogo kwa sababu Serikali hivi sasa ina majukumu mengi zaidi ya kuyachukulia ambayo yamo katika utaratibu wa kawaida, lakini jamii yetu tunaishauri na tunashawishi wananchi wote tukiwemo sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tushiriki kikamilifu katika kuwasaidia viongozi wanaohusika na madrasa pamoja na usimamizi wa misikiti, lakini vile vile Serikali haitaki kujiingiza moja kwa moja katika kusaidia mambo ya dini kwa sababu tuna dini nyingi hapa kwetu na Serikali haina dini.

Kwa hivyo ni wajibu wetu sisi sote tuliokuwemo humu ndani kila mmoja kwa upande wake na kwa imani yake kusaidia na kushiriki katika misaada mbali mbali. Hata hivyo serikali sasa hivi inafanya utaratibu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mufti kutafuta mbinu wale wahisani wote ambao wanaweza kusaidia madrasa ili walimu angalau wapate sabuni yao na wao kwa sababu wanafanya kazi nzuri, lakini wakati huo huo tunafanya utaratibu wa kuwachunguza hao walimu wanaosomesha madrasa tumebaini kuna matokeo mbali mbali mabaya yanayofanyika katika madrasa zetu.

Kwa hivyo kabla hujasomesha na umri utawekwa maalum kwa walimu wa madrasa ili kuwafanyia *vetting* wale walimu kwa sababu tumegundua matatizo mengi sana yanatokezea katika madrasa zetu kutokana na *ethics* au maadili ya walimu wetu yanakuwa hayaridhishi, kwa hivyo hayo tutayashughulikia.

Kuhusu suala la mitaala tutaiangalia vizuri lakini pia hakuna tatizo kuja kuongeza alimradi tu utapaongeza somo lolote itabidi basi ipate ridhaa kwa Afisi ya Mufti na Wizara ya Elimu. Ahsante sana.

**Mhe Spika:** Ahsante, Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf Jussab:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) kwa kuwa Ofisi ya Mufti ipo chini ya Wizara yako na Mufti ndio anayehusika na Waislam wote nchini Zanzibar, Je, Ofisi ya Mufti mpaka sasa hivi imejipanga vipi kuwasaidia walimu wa maeneo ya shamba ambao wana hali ya chini na wanafunzi hawawezi kulipa ada ukilinganisha na vyuo vya mjini wanafunzi wanalipa ada nzuri.

b) Kwa kuwa Zanzibar ina misikiti zaidi ya 2000 na misikiti mingi ipo katika hali mbaya imechoka husasan ya barabarani na ya ndani na kwa kuwa kuna watu wengi wameanza kujitokeza kutaka kujenga misikiti mipya.

Je, Wizara yako kupitia Ofisi ya Mufti imejipanga vipi kuwashauri wanaotaka kujenga misikiti mpya kuweza kuijenga ile ambayo iko katika hali mbaya halafu baadae ikaangaliwa sehemu nyengine ya kujenga misikiti mipya.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Suala la kusaidia kulipa ada Ofisi ya Mufti kwa sasa hivi halitowezekana, suala la madrasa ni suala la hiyari lakini ni muhimu kwa Zanzibar kwa sababu tupo asilimia kubwa ya waislam hapa zaidi ya asilimia 90%, lakini vile vile hatuwezi kusema kwamba tuwalipie ada elimu Zanzibar inatolewa bila ya malipo. Sskuli zote zinatolewa elimu bila ya malipo, kwa madrasa vile vile ni jambo ambalo ni vizuri na sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi linapotokea tatizo kusaidia si vibaya wabunge na viongozi wengine katika maeneo yetu.

Sasa unapoibebesha mzigo ofisi ya Mufti itakuwa hatuifanyii haki kusema kwali kwa kuwa ina majukumu mengine wao kusimamia maadili na taratibu za madrasa na misikiti zinatekelezwa vizuri ili kuhakikisha kwamba nidhamu inapatikana.

Kuhusu suala la misikiti inayojengwa ni kweli kumejitokeza wahisani mbali mbali kujenga misikiti katika maeneo mbali mbali na pengine ile ya zamani haifanyiwi ukarabati, sasa hayo ni maelewano kati ya jamii na wale wanaokuja. Kwa sababu wanapokuja wanakuja kukutana na jamii katika maeneo ya Wilaya na Mikoa, sasa ni vizuri wanapokuja basi wale viongozi wa eneo lile shehia, Masheha, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa basi angalau wawape maelekezo kuna misikiti ambayo inahitaji kufanyiwa ukarabati basi hilo linawezekana.

Lakini kukataza kwamba wasijenge misikiti mipya hilo haliwezekani tujenge misikiti kadri itakavyowezekana kwa sababu ibada ni muhimu na kama nilivyosema tuko wengi waislam hapa na ni wajibu wao kujenga msikiti kwa ajili ya kufanyia ibada, hatutaki kujenga misikiti kwa ajili ya vikundi fulani au kutokana na malengo fulani tunajenga misikiti kwa ajili ya ibada si kwa lengo lolote lile ahsante.

**Mhe. Spika:** Ahsante kwa suala la mwisho la nyongeza Mhe. Panya Ali Abdalla:

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona na kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika kusomesha kuna utaratibu maalum ambao wa kitaaluma wa kuwapatia walimu taaluma ili waweze kufanya kazi yao hiyo vizuri na kwa sasa tuna changamoto kubwa ya kuwa tuna walimu wengi katika madrasa lakini wenye kusomesha, sio wenye taaluma ya kusomesha na walimu wale wanatakiwa kusomesha vijana katika dini yao lakini pia kuwafunza maadili mazuri.

Je, Wizara yako imejipanga lini kuweza kuwapa walimu wetu hii taaluma na waweze kukabidhiwa vyeti kabisa ili kila atakapokwenda malimu huyu awe anazo sifa za kuweza kusomesha.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe: Panya Ali Abdalla swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kweli kama nilivyosema kwenye jibu langu mama lile nimesema kwamba tumeandaa mafunzo kwa ajili ya walimu wa madrasa na misikiti na tumebaini kwamba makosa yanayofanyika katika meneo ya misikitini au pengine katika madrasa kwa sababu ya watu wamekosa taaluma ya uongozi wa maiikiti na madrasa zetu, kwa hivyo utaratibu huo wa kuandaa mafunzo tayari Ofisi ya Mufti imeandaa program na mafunzo yataendelea ili kuhakikisha tunapata walimu wenye maadili mazuri wanaokidhi mahitaji ya jamii ya Zanzibar ahsante sana.

**Nam. 15**

**Changamoto ya Ukusanyaji wa Kodi kwa Wafanyabiashara**

**Mhe: Yussuf Hassan Iddi (Kny: Machano Othman Said)** – Aliuliza:

Kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikiibiwa mapato yake na wanyabiashara kwa kukwepa kulipa kodi ikiwemo kutokutoa risiti au kutolewa risiti zisizohalali.

(a) Ni kwa nini Serikali inasita kutumia mfumo wa risiti za *EFD*.

(b) Kwa nini vituo vingi vya uuzaji mafuta havitoi risiti

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango** – Alijibu:
Mhe. Spika, kwanza nimuombee Mhe. Machano Othman Said apate nafuu ili aweze kujumuika na sisi katika ujenzi wa taifa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake Nam. 15 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali lake naomba nitoe maelekezo yafuatayo:-

Kwa mujibu wa Sheria Usimamizi wa Kodi ya Zanzibar *(The Tax Administration and Procedure Act No: 7 ya 2009)* kila mtu anaefanya biashara anatakiwa kutoa ankara au risiti kwa huduma au bidhaa anayouza. Risiti au ankara hiyo inaweza kuwa ya kieletroniki au ya kawaida yaani ya

karatasi iliyoandikwa kwa mkono na kisha mfanyabiashara kutunza nakala zake katika eneo la biashara.

Serikali baada ya kuona umuhimu na urahisi wa kutumia mfumo wa kieletroniki katika kutolea risiti, mwaka 2019 ilianza utengenezaji wa mfumo wa kutolea risiti na mfumo huo ulikuwa tayari kwa majaribio ilipofika mwezi Septemba, 2020.

Kuanzia tarehe 16/10/2020 mfumo huu ulianza rasmi kutumika kwa majaribio na hadi kufikia tarehe 15/1/2021 jumla ya wafanyabiashara 150 wa Unguja na Pemba walisajiliwa kupitia mfumo huo. Hata hivyo, katika kipindi hiki cha majaribio imebainika kuwepo kwa dosari za kimfumo ambapo hivi sasa tunaendelea kuzifanyia kazi na lengo letu ifikapo mwezi Aprili 2021 mfumo huu uweze kutumika kwa watu wote waliosajiliwa kulipa kodi.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haijasita kutumia mfumo wa utoaji risiti kwa njia ya Eletroniki bali inazifanyia maboresho kasoro ambazo zimejitokeza katika kipindi cha majaribio na ifikapo mwezi Aprili mfumo huu utaanza kutumika kama nilivyoeleza awali.

(b) Vituo vya kuuzia mafuta vinapaswa kutoa risiti kama ni ya eletroniki au ya kawaida, tunawahimiza wananchi kudai risiti kila wanapolipa fedha kwa ununuzi wa mafuta. Kutokutoa risiti ni kosa na kwa mujibu wa sheria na mfanyabiashara akipatikana na kosa la kutokutoa risiti basi anapaswa kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria yaUsimamizi wa Kodi yaNam. 7 ya 2019.

**Mhe. Spika:** Mhe. Yussuf Hassan Iddi kwa suala la nyongeza.

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi:** Ahante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

a) Kwa kuwa amekiri katika kipindi kile cha majaribio kuna dosari ambazo zimejitokeza katika mfumo huu je, Serikali imejipanga vipi watakapoanza mwezi wa Aprili, hii dosari iliyotokezea nyuma haitokezei tena.

b) Serikali ni lini itahimiza wauzaji wa mafuta waatatumia mashine zinazotoa risiti kama wanavyofanya wenzetu wa Tanzania Bara.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, kwanza na nimshukuru Mhe. Yussuf Hassan Iddi kwa maswali yake ya nyongeza.

a) Kama nilivyoeleza awali kwamba mfumo huu tayari ulishakamilika lakini katika kipindi hichi cha majaribio kulionekana kuna dosari ambazo tunahitajika kuzifanyia kazi kabla ya ku-*roll out* kwa wafanyabiashara wote. Kwa hivyo hizi dosari ni kawaida, mifumo kama hii ukishamaliza kukamilisha unaifanyia *testing*, kwa hivyo unaangalia aidha kama kuna dosari yoyote ya kimfumo unazifanyia kazi lakini naamini kabisa dosari hizi tutazifanyia kazi na huko mbele ya safari *inshaallah* hizi dosari hazitojitokeza pale ambapo tutapo-*roll out* mfumo.

b) Suala la utumiaji wa mashine hizi za ki-*electronic* na kweli katika mmoja wa mkakati wetu *once* maboresho haya yatakapofanyika basi vituo vyetu vyote vya mafuta kwa Zanzibar vitakuwa na mfumo wa kutoa risiti kwa electronic lakini katika kipindi hichi cha mpito niwatake watoa huduma hizi watoe risiti hizo hizoi za mkono na wale wanaopatiwa huduma basi waendelee kudai risiti za mkono. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria yetu kila mtu anayetoa huduma au anayefanya biashara yoyote anapaswa kutoa risiti.

**Mhe. Spika:** Mhe. Shadya Mohammed Suleiman nilikuona kwa swali la nyongeza.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi na mimi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Kabla ya kumuuliza Mhe. Waziri, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kunipa pumzi zake na nikaweza kusimama hapa nikiwa mzima na mwenye afya, lakini pia niendelee kumshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ya ufasaha. Lakini naomba nimuulize Mhe. Waziri swali kama ifuatavyo.

Katika majibu yake amesema wafanyabiashara 150 Unguja na Pemba tayari wameanza kutumia mtandao huu katika njia ya majaribio, suala langu liko hapa. Ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kuingia Serikalini katika muda huo wa majaribio ambao wafanyabiashara hao wameanza kutumia huu mtandao.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi nimpongeze Mhe. Shadya Mohammed Suleiman kwa swali lake dogo na zuri la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa sasa sitokuwa na taakwimu halisi kwa hawa wafanya biashara 150 na naomba hili suala niweze kumletea takwimu hizi rasmi kwa sababu ni suala la kitakwimu kwa hiyo nitamletea kwa maandishi. *(Makofi)*

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza suala dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a). Mhe. Waziri, kodi ndio inayoendesha serikali bila ya kodi hatuwezi kufika popote lakini Mhe.Waziri katika majibu yako umesema kwamba umetoa mashine mia moja na hamisini (150) kwa wafanyabiashara.

Zanzibar tuna wafanya biashara zaidi ya elfu kumi (10,000) wakubwa, wadogo na wa kati je, mashine hizi mlizozitoa mmewapa wafanyabiashara wa aina gani? Lakini Mheshimiwa Waziri, mashine hizi zina ubora gani maana Mheshimiwa Waziri unapokwenda halmashauri unaambiwa mashine watoa risiti zile za kawaida ukiuliza unaambiwa mashine zina baridi.

Sasa nilitaka kujua hizi mashine munazotoa zinafanya kazi mmezihakiki na kuhakikisha zinafanya kazi kama ilivyo ili kupata hiyo kodi na kundoka na hiyo baridi kama iliyoko halmashauri. Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mhe. Suleiman Makame Ali kama ifuatavyo:

Kwanza swali la wafanyabiashara ambao katika kipindi hichi cha majaribio tumewachukua wafanyabiashara katika makundi yote kwa sababu ni kipindi cha majaribio kwa hiyo tume-*sample specimen* ambayo inaweza ikawakilisha makundi yote ya wafanyabiashara.

Lakini swali la pili kuhusu ubora wa mfumo wa mashine kusema la ukweli mfumo huo ni bora kabisa, labda kwa kitaalamu kinaitwa *virtual physical device* ambayo risiti yake inatoka moja kwa moja kwenye mfumo wa *server* zetu ambazo ziko chini ya mamlaka yetu ya kodi hizi yaani Mamlaka ya Bodi ya Mapato ya *ZRB.*

Kwa hiyo kila utakapotoa risiti ile risiti moja kwa moja itaonekana na maafisa wetu wa kodi kwa hiyo ni mfumo ambao bora utasaidia sana na kwa kiasi kikubwa kutusaidia kupata mapato kupunguza pia ukwepaji kodi ambao kwa kipindi chote hichi toka serikali ya awamu ya nane ianze kazi imekuwa jambo moja kubwa ambao linasisitiza kwamba kila mtu kila mfanya biashara lazima alipe kodi kama ulivyoeleza kwamba serikali inaendeshwa kwa kodi na mimi nitumie nafasi hii kwanza kukutaka wewe binafsi uwe *champion* mzuri kuhimiza wafanyabiashara na wananchi wote kulipa kodi, kwa sababu ndio maendeleo yetu. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 21**

**Kukosekana Huduma Katika Wilaya Ndogo Ya Kojani**

**Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:**

Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii lakini swali langu limejibiwa kwa mujibu wa barua, lakini pamoja na barua nina swali la nyongeza.

**Mhe. Spika:** Samahani sijakuelewa mheshimiwa uliza swali tu toa ruhusa ya swali lako kuulizwa.

Mnamo mwaka 1990, Mhe. Rais mstaafu Dkt. Salmin Amour Juma alitangaza Kojani kuwa Wilaya ndogo kwa ajili ya kuwasogezea wananchi huduma za kiserikali. Tokea wakati huo mpaka sasa, hakuna huduma yoyote inayotolewa katika ofisi hiyo ambayo ina watumishi watano (5).

a) Ni kwanini Serikali tokea wakati huo haijasogeza huduma hizo kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

b) Je, Wizara ina mpango gani katika kuiboresha Wilaya ndogo ya Kojani ili wananchi wapunguziwe usumbufu wa kufuata huduma Wilaya ya Wete, kama ilivyo Wilaya ndogo ya Tumbatu.

c) Je, Serikali haioni kuiweka ofisi bila ya huduma zilizo kusudiwa n ikupoteza mali ya umma bila faida kwa wananchi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar suala lake Nam. 21 lenye vifungu (a), (b) na (c). Mhe. Spika, kabla kumjibu swali lake naomba nitowe maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Spika, nakubaliana kwamba mnamo mwaka 1990, Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar Dkt. Salmin Amour Juma aliitangaza Kojani kuwa Wilaya ndogo kwa ajili ya kuwasogezea wananchi huduma za kiserikali. Lakini sikubaliani na maelezo ya kwamba tokea wakati huo mpaka sasa, hakuna huduma yoyote inayotolewa katika afisi hiyo ambayo ina watumishi watano (5). Jukumu kubwa la Afisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya ni kuratibu na kusimamia shughuli zote za Serikali katika maeneo yao.

Shughuli hizo zimegawika katika maeneo makuu mawili ambayo ni utekelezaji wa shughuli za kawaida na shughuli za miradi ya maendeleo zinazotekelezwa katika sekta mbali mbali na Wizara husika.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba kujibu kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Serikali kupitia sekta mbali mbali imehakikisha huduma muhimu hasa za kijamii zikipatikana katika Wilaya ndogo ya Kojani kiwemo afya, elimu, maji na umeme. Maendeleo yaliyopo Kojani ya leo si yale ya Kojani ya mwaka 1990 ambapo mfano mzuri ni Ujenzi wa Skuli Mpya ya Sekondari Kojani ambayo imefunguliwa tarehe 09/01/2021 na Rais Mstaafu Dkt. Ali Mohamed Shein katika kuadhimisha sherehe za miaka 57 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Aidha, Serikali imekuwa ikisogeza rasilimali katika Afisi zake zote za Wilaya kulingana na uwezo uliopo ikiwa ni pamoja na miundombinu, rasilimali watu na rasilimali vifaa na baadae jitihada zinaendelea za kupeleka huduma zote muhimu katika Wilaya ndogo ya Kojani na maeneo mengine kama hayo ya visiwani.

b) Mhe. Spika, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina mpango wa kuiboresha Wilaya ndogo ya Kojani ili wananchi wapunguziwe usumbufu wa kufuata huduma mbali mbali katika Wilaya ya Wete, mpango huo unajumuisha kujenga majengo mapya ya Afisi za Wakuu wa Wilaya ikiwemo Afisi ya Wilaya ndogo ya Tumbatu; kupeleka Maofisa wa Sekta katika Wilaya ndogo ya Kojani mfano Afisa wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (vizazi, vifo, ndoa, talaka na vitambulisho vya Mzanzibar); pamoja na ununuzi wa vifaa muhimu vya Afisi na mawasiliano.

c) Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema hapo awali kwamba Afisi ya Wilaya ndogo Kojani kazi yake kubwa ni kuratibu na kusimamia Shughuli zote za Serikali zilizopo kwenye Wilaya hiyo.

Kuwepo kwa Afisi ya Wilaya ndogo ya Kojani kunasaidia kuratibu usuluhishi wa migogoro ya ardhi, upatikanaji wa elimu na pembejeo za kilimo, upatikanaji wa huduma za afya, elimu, maji na umeme na shughuli nyengine za kimaendeleo. Kwa mnasaba huo, hakuna upotevu wa mali ya umma unao nasibishwa na uwepo wa Afisi hii na kazi zilizokusudiwa zinafanyika na kwamba tutaendelea kuboresha zaidi huduma za Serikali katika Wilaya ndogo ya Kojani na Wilaya ndogo ya Tumbaku.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, nashukuru sana kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwanza Mhe. Waziri nikupongeze sana kwa kuanza vizuri kwa kweli kulikuwa na kadhia kubwa sana upatikanaji wa shughuli za kijamii. Lakini mwanzo wako unaonesha mzuri na nakuombea kwa Mwenyezi Mungu uendelee. *(Makofi)*

Lakini pamoja na shukurani hizo bado kuna kadhia ya wananchi katika Kisiwa cha Kojani kwa usumbufu wa kupatikana huduma nyengine muhimu zikiwamo vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi pamoja na vyeti vya kuzaliwa. Ni jambo linalowasumbua wananchi kuvuka bahari wakafuatilia kwenda Wilaya ya Wete, wakati Wilaya ndogo ya Kojani ipo ni maafisa wako tu kujipanga vizuri alau kwa wiki kwenda mara mbili kwenda kusaidia. Je, Mhe. Waziri ni lini utatusaidia ili wananchi wapate huduma muhimu pale pale Kisiwani Kojani na vitongoji vyake.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Hassan Hamad Omar swali lake la nyongeza lenye mnasaba wa shughuli za vitambulisho vya Mzanzibari na vyeti vya kuzaliwa.

Mhe. Mwakilishi labda nimjulishe kama nilitanauglia kwenye jibu langu la awali kwamba serikali inayo mpango sasa wa kufungua Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii katika Wilaya ndogo ya Kojani, imani ya serikali na ni imani yetu kwamba tutakapofungua ofisi hii hizi changamoto zitaondoka ama kupungua kabisa.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Kwanza Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini la pili kumhsukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, nilikuwa na swali moja tu dogo la nyongeza jee, ni vigezo gani vinavyotumika kutokana na eneo ama kisiwa husika ili kiweze kutangazwa kuwa Wilaya ndogo Mhe. Spika nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika ningeomba Mhe. Mjumbe arudie swali lake.

**Mhe. Spika:** Mhe. Issa Haji Ussi muwekee vizuri Mhe. Waziri.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe. Spika, ahsante swali langu lipo juu ya uanzwishaji wa Wilaya ndogo nauliza ni vigezo gani vinavyotumika na serikali mpaka pale serikali inaporuhusu kuanzishwa kwa Wilaya ya ndogo ili kama kuna maeneo mengine nayo pia tuweze kujua kama yatakuwa yamekidhi vigezo vya kutangazwa wilaya ndogo.

**Mhe. Spika:** Ahsante ni vigozo vya uanziswaji wa Wilaya.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chwaka kama ifuatavyo:

Ni vigezo gani vinavyotumika kuanzisha Wilaya ndogo moja ni kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa au Sheria za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambayo ni sheria namba 7 na sheria namba 8 ambayo inatoa mwongozo wa uanzishwaji wa Wilaya ndogo. Kwa hiyo kama ilivyokuwa katika Wilaya nyengine iwe ni Mikoa ama Wilaya zinaanzishwa hizi kwa mujibu wa sheria ambao zimeanishwa katika sheria hizo mbili nilizozitaja, hivyo ni vigezo vikubwa zaidi vinavyotumika.

**Nam. 6**

**Ununuzi Wa Vifaa Vya Kujifundishia Kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum**

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis – Aliuliza:**

Naipongeza Serikali kwa kuendelea na juhudi za kuimarisha Sekta ya Elimu kwa kununua vitendea kazi ikiwemo vitabu vya kujifunzia pamoja na kuimarisha huduma bora kwa walimu.

a) Kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, ni vifaa gani ambavyo vimeweza kununuliwa kwa lengo la kusaidia wanafunzi hao kujifunza.

b) Je, ni skuli zipi ambazo zimenufaika.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) - Alijibu:**

*Bismillah Rahmani Rahim*, Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba nimjibu Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis Mwakilishi wa Viti Maalum swali lake Nam. 6 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wazee na Watoto imewapima wanafunzi wenye mahitaji maalum katika skuli mbalimbali ili kuweza kununua vifaa vitakavyoendana na ukubwa wa matatizo yao.

Wizara yangu imeweza kununua Kompyuta 9, *Laptop* 4 zenye "*software*" kwa watoto wenye mahitaji maalum, *TV 7, DVD 7, Note taker 6, Wheelchair 1,* Shimesikio 20, Fimbo nyeupe 6, Mashine za kupimia usikivu 2, Mabusati, *"speech trainer" 2, "ear mode kits"*, saa zenye sauti *(talking watch)* kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Aidha, Wizara inaendelea na mchakato wa manunuzi ya vifaa zaidi vya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa mwaka huu.

Orodha ya vifaa ambavyo vitanunuliwa ndani ya mwaka huu wa fedha ni pamoja na Miwani 2,323, *Braille Machine* 40, *Laptop* 10, *Voice recorder* 40, Shimesikio 102, *Wheel Chairs* 33, *Kid Walkers* 4 na Fimbo nyeupe 65.

b) Mhe. Spika, skuli zilizonufaika kwa vifaa vilivyonunuliwa ni Jangombe msingi (A), Kisiwandui, Mwembemakumbi, Mwanakwerekwe (E), Mwanakwereke (F), Mwanakwerekwe (H), Mwanakwereke (A), Haile Selassie, Hamamni, Fuoni Msingi (A), Jambiani, Umoja Uzini, Mgeni Haji na Gamba kwa Unguja na Skuli za Michakaini, Pandani, Chokocho, Mtambile na Shumbaviamboni kwa Pemba. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza lenye kipengele (a) na (b).

Mhe. Spika, miongoni mwa vifaa vya kujifundishia naamini itakuwa ni vitabu ambavyo vitawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum hasa wenye ulemavu waweze kujivunza, ili waweze kupata ufaulu sawa na wale wanafunzi ambao hawana ulemavu na kutokana na Mhe. Waziri maelezo yake hayaoneshi kwamba kuna vitabu vyovyote vilivyochapishwa kwa ajili ya kujifunza wanafunzi hao.

a) Je, Mhe. Waziri serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanafunzi hao wanafaidika na kujifunza kama wanavyofaidika wenzao.

b) Mhe. Spika, idadi kubwa ya ulemavu hapa Zanzibar kutokana na tafiti zilizofanywa na Umoja wa Watu Wenye Ulemavu ni ulemavu wa viungo na kutokana na maelezo ya Mhe. Waziri ni kwamba vifaa walivyonunua wameweza kunaunua *wheel chair* moja naamini hii ni kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa viungo. Jee, kununua wizara *wheel chair* moja haioni kwamba kunawakosesha fursa wanafunzi wengine wenye mahitaji maalum wakiwemo walemavu wa viungo kukosa huduma hizo za kuweza kufaidika na visaidizi. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru na naomba nimjibu Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, suala la vitabu ni suala ambalo lina utaratibu wa kawaida kwamba serikali kawaida inatoa vitabu kwa wanafunzi wake wote na kwa upande wa wanafunzi wenye mahitaji maalum ni kwamba vitabu ambavyo tunatumia, vile vile vitabu ambavyo vipo katika mitaala yetu vinaandikwa kwa hati ambazo zinawafanya wanafunzi hawa nao waweze kusoma kama wengine.

Kwa mfano kwa wale wanafunzi ambao wenye uoni hafifu kwa maana kutumia *Braille* kwamba vile vitabu *content* ile ile lakini inaandikwa kwa mujibu mwanafunzi yule naye aweze kuona kwamba na yeye anaweza kusoma. Lakini kwa wanafunzi ambao wana mahitaji mengine kwa mfano kama tulivyoelezea vifaa kwa sababu kwa mwengine ambaye anakuwa yeye tatizo lake

sio la macho ni kwamba anaona vitabu tayari ni kwamba vipo na vinatumika katika utaratibu kama niliosema.

Mhe. Spika, suala la pili ni suala la *wheel chair* moja na ndio maana katika jawabu letu tumesema kwamba vifaa ambavyo vitaendelea kununuliwa katika bajeti yetu hii *wheel chair* thelathini na tatu (33), tunajua kwamba haziwezi kutosheleza kwa wanafunzi wote lakini mahitaji sio *wheel chair* peke yake na ndio maana tumeweka na vifaa vyengine.

Mhe. Spika, lakini kwa bahati nzuri kwamba serikali yetu inakuwa na wahisani mbali mbali ambao huwa wanatusaidia katika vifaa mbali mbali, miongoni mwa vifaa ambavyo tunakuwa tunapata vikiwemo *wheel chair*, kwa hivyo vile hatujaviingiza katika vile ambavyo sisi tunanunua lakini kwamba vinapokuwa vinakuja tunaendelea kuvisambaza kwa skuli zetu zote za Unguja na Pemba. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Anna Athanas Paul:** Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona na mimi napenda nimshukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa majibu yake mazuri lakini nilikuwa na swali langu la nyongeza kuhusu miundombinu ya kuweza kufikika baada ya kupatiwa hivyo vifaa hao watu wenye mahitaji maalum. Je, miundombinu ya kufika kwenye madarasa lakini pia miundombinu ya kuweza kufikia kwenye vyoo ikoje unahakikisha imekaa vizuri kwa ajili yao. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante Mheshimiwa swali linahusu miundo mbinu nahisi unaweza kulijibu kwa sababu halikuwa swali la msingi.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusu yako naomba nimjibu Mhe. Anna Athanas Paul swali lake na nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kuhusiana na miundo mbinu ya kufikika kwa yale majengo ambayo tumeyajenga mapya tunahakikisha kwamba tumejenga *ramp* ambayo inawasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum kuweza kufika kwa urahisi, na kwa zile skuli zetu za zamani ni kwamba tulikuwa na mpango na tushafanya kurekebisha kuweka *ramp* katika skuli zetu ili kuona kwamba huduma hii wanafunzi wetu wanaweza kusoma vizuri zaidi kwa kuweza kufika katika madarasa yao.

Lakini vile vile kwa upande wa vyoo mheshimiwa yaani tuna mipango ambayo inaendelea ya kujenga vyoo kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum na vyoo hivyo tumeshajenga katika skuli nyingi, tunashirikiana na wadau wenzetu pia katika ujenzi wa vyoo hivi, lakini huko katika skuli zetu hizi ambazo tumesema mpya basi zote unakuta kuna choo maalum kwa wanafunzi wanao mahitaji maalum. Nakushukuru mheshimiwa.

**Mhe. Aza Januar Joseph:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia swali la nyongeza, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba wizara imejipanga vipi kuhakikisha kuwa katika skuli hizi zote ambazo zina mahitaji maalum ufuatiliaji wake uko vipi kuhakikisha kwamba wanafunzi hao wanashirikishwa katika michezo. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba kumjibu Mhe. Aza Januar Joseph swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Kitengo chake cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha inakuwa inafuatilia katika skuli mbali mbali ambapo kuna wanafunzi wana mahitaji maalum. Miongoni mwa mambo ambayo yanafuatiliwa mbali ya masomo yao tu, lakini wanaangalia pia masuala mazima ya michezo katika skuli. Kwa hiyo, ni kusema kwamba wanafunzi wetu hawa na wao wanapata fursa kama wanafunzi wengine ya kucheza, kushiriki, kuchanganyika na wanafunzi wenzao wote kama walivyo wanafunzi wengine. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Nam. 47**

**Changamoto ya Masharti Magumu Yanayowekwa na Wamiliki wa Skuli Binafsi**

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:**

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la kuanzishwa skuli binafsi hapa Zanzibar. Hata hivyo, baadhi ya skuli hizo masharti yao ni magumu ya kujiunga hasa kwa vile wanataka wanafunzi wenye uwezo mkubwa wa ufahamu, hivyo hali hiyo inapelekea kuwanyima haki ya kujiunga katika skuli hizo wananchi wa Zanzibar.

(a) Je, serikali ina utaratibu gani wa kuzifuatilia na kuzikagua skuli hizo.

(b) Kwa nini baadhi ya skuli hizo ada yao inapangwa kulinganisha na fedha za Marekani.

(c) Hivi serikali ina jua kwamba baadhi ya skuli hizo, zinawatolesha faini wazazi wanaochelewa kulipa ada za watoto wao.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) - Alijibu:**

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 47 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwama zipo skuli huweka masharti magumu kwa watoto kujiunga na skuli hizo. Lengo la skuli hizi si kuwanyima wanafunzi haki ya kujiunga katika skuli hizo ila ni kuangalia uwezo wao wa kufahamu ili wanafunzi hao wapate maendeleo mazuri hasa ukizingatia wazazi wao hutumia fedha kwa ajili ya masomo yao. Kesi hizi zikijitokeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali huzungumza na wamiliki na walimu wakuu kuondoa kasoro hizi. Aidha, serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inayo utaratibu wa kuzikagua skuli zote za binafsi kwa kila mwaka.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kwamba baadhi ya skuli za binafsi ada yao inapangwa kulinganisha na fedha za Marekani. Skuli ambazo hutumia utaratibu huu ni zile skuli za Kimataifa (*International Schools*). Kwa hapa Zanzibar skuli hii ni moja tu ndio ambayo inajuulikana rasmi kuwa ni skuli ya kimataifa ambayo huandikisha watoto wenye asili kutoka nchi mbali mbali, hasa ukizingatia wazazi wao wanakuwa wengine wale ambao wanafanya kazi katika balozi zetu mbali mbali. Skuli hiyo ni skuli ya Kimataifa ya Zanzibar (*Zanzibar International School*) iliyopo Mazizini Unguja. Mzazi anayemuandikisha mtoto wake katika skuli hiyo ni maamuzi yake mwenyewe ya kukubaliana na utaratibu unaotumika wa uendeshaji wa skuli hiyo ikiwemo utaratibu wa malipo ya ada ya masomo kwa fedha za kigeni.

(c) Mhe. Spika, serikali haina taarifa ya wazazi kutoleshwa faini kwa sababu ya kuchelewa kulipia ada za masomo za watoto wao. Aidha, gharama za skuli zinazolipwa ni zile ambazo zimeorodheshwa kwenye mkataba baina ya skuli na mzazi/mlezi. Hata hivyo, suala hili tumelipokea na tutalifuatilia kwa karibu zaidi ili kuhakikisha kama zipo kasoro hizo zinaondolewa kwa mujibu wa sheria za usajili wa skuli hizo. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa Mhe. Waziri umekiri kwamba zipo baadhi ya skuli huweka masharti magumu kwa wanafunzi kujiunga. Pia umekiri kuzungumza na wamiliki wa baadhi ya skuli hizo ili kuondoa kasoro hizo, kwa kuwa kadhia hiyo bado inaendelea. Je, kuna utaratibu gani wa kisheria mnauchukua kwa skuli ambazo bado zinaendelea kukaidi maelekezo ya wizara kwa kuendelea na utaratibu huo.

b) Kwa kuwa Mhe. Waziri pia umekiri kwamba ni maamuzi ya mzazi kukubali au kukataa utaratibu wa malipo ya ada ya masomo kwa fedha ya kigeni. Je, wizara imechukua hatua gani kuwaelimisha wananchi kuhusu haki yao hiyo kukataa au kukubali ada ya fedha za kigeni. Je, serikali haioni kuwaachia skuli hizo kutumia utaratibu wa kulipa kwa fedha za kigeni kunadhoofisha fedha yetu ya ndani.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, kama ambavyo nilisema katika jibu la msingi ni kwamba kuweka masharti hayo haina maana ya kuwanyima haki wengine kuweza kujiunga, bali ni katika kutaka kuona kwamba kunawekwa viwango vizuri kwa wanafunzi ambao wanasoma ili wapate maendeleo mazuri zaidi katika elimu zao.

Mhe. Spika, na katika hili ni kwamba pale ambapo panajitokeza changamoto kama ambavyo nilijibu awali, serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakuwa inazungumza na skuli ile kama kuna malalamiko yoyote ambayo mzazi ameyafikisha. Jambo hili limekuwa likifanyika katika siku zote za utaratibu wa kazi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, na kama endapo skuli yoyote itakuwa imevunja taratibu za kisheria basi kama ambavyo ilivyo skuli imesajiliwa kwa mujibu wa sheria, basi ni sheria hizo hizo ambazo

zinatumika kwa vile vifungu ambavyo vimepangwa kuona kwamba inatolesha faini ama adhabu kwa skuli ambayo itakuwa imekiuka taratibu hizo.

Mhe. Spika, suala la kuelimisha jamii kuhusu fedha za kigeni, kama nilivyojibu katika swali letu la msingi ni kwamba skuli hizi zinajulikana na kama nilivyosema ni skuli ya *International School* ambayo inachukua wanafunzi kutoka mataifa mbali mbali. Kwa mfano, Mhe. Spika tuna balozi nyingi Zanzibar ambazo zinafanya kazi na wazazi wao ambao wanafanya kazi hizo za ubalozi, malipo ambayo wanalipwa wao wanalipwa kwa dola hatutawatendea haki sana kumwambia kwamba alipe *Tanzania Shillings* kwa sababu tayari skuli imeshawekwa kama ni skuli ya kimataifa. Lakini kwa zile skuli zetu nyengine malipo yanafanyika kwa pesa za *Tanzania Shillings*, hata kama skuli kwa mfano wanataka kulipa kwa dola lakini mzazi analipa kwa *Tanzania Shillings* kwa ile *rate* ambayo itakuwa imewekwa. Lakini kwa skuli hizi ambazo tunasema *International School* tayari kwamba ni skuli ya kimataifa kwa hiyo fedha ya kimataifa ndio ambayo inatumika, na hata katika mitaala ya masomo yao ni kwamba inafuata mitaala ile ile ya kimataifa kwa maana ya *Cambridge curriculum*.

Mhe. Spika, katika kutoa taaluma kwa wananchi serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inatoa taaluma na itaendelea kuwanasihi wazazi kwamba unataka kumpeleka mtoto wako katika skuli yoyote basi angalia kwanza skuli hiyo na masharti yake ndipo upeleke mtoto wako. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante Mhe. Spika, nimeyasikia majibu ya Mhe. Waziri wakati anajibu na amesisitiza kwamba kwa Zanzibar skuli moja tu ndio inatambulika kwamba inatoza ada kwa dola za Kimarekani. Je, Mhe. Waziri uko tayari kupokea majina ya skuli zaidi ya moja ambazo ziko Zanzibar na sio *International School* kwa vigezo ambavyo umevitaja ambazo zinatoza ada kwa dola ya Kimarekani.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante Mhe. Spika, napenda kumshukuru sana Mhe. Omar Said Shaaban vile vile nimpongeze kwa kula kiapo leo, karibu sana katika Baraza letu.

Mhe. Spika, nimwambie kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ipo tayari kupokea orodha ya skuli hizo na tutazifanyia kazi. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Juma Ali Khatib:** Ahsante Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri je anafahamu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Hussein Ali Mwinyi kwamba walitoa agizo maalum kuwa malipo yote ya fedha kwa mujibu wa taratibu za serikali yawe ni malipo ya fedha za Tanzania. Sasa haoni kwamba anakwenda kinyume na maagizo ya Marais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, na hata jana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alisisitiza kwamba malipo yote yawe ni fedha za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sio pesa za kigeni. Je, unasemaje Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Juma Ali Khatib

swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, nikiri kwamba serikali yetu ama wizara haipingi wala haikatai kufuata maagizo yoyote ambayo yanatolewa na viongozi wetu, na huo ndio utaratibu na hiyo ndio sheria yetu ilivyo na ndio utaratibu wote unavyotakiwa.

Mhe. Spika, kwa suala la skuli ya *International School* ni suala ambalo tutalizungumza ikionekana kwamba lazima ilipe kwa Tanzania Shillings, lakini kama italipa kwa *rate* ambayo itakuwa ipo katika soko halitakuwa ni tatizo kubwa Mhe. Spika, muhimu ni kwamba malipo yatakuwa yanafanyika kwa mujibu wa makubaliano ambayo yatakuwa yamefikiwa. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Nam. 42**

**Ujenzi wa Kiwanja cha Mpira Kilichopo Kangani**

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha – Aliuliza:**

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa juhudi inazozichukua za kuimarisha viwanja vya michezo hususan ujenzi wa kiwanja cha mpira wa miguu kilichopo Kangani katika Jimbo la Mtambile kisiwani Pemba. Pamoja na juhudi hizo, kumekuwa na changamoto nyingi katika utekelezaji wa azma hiyo.

(a) Je, ujenzi wa kiwanja cha mpira wa miguu cha Kangani tayari umekamilika.

(b) Kama ujenzi umekamilika, je, tayari kiwanja hicho kimeshakabidhiwa Wilaya kwa matumizi.

(c) Kwa sasa kiwanja hicho kinaonekana kimezungukwa na majani, je, ni lini majani hayo yatakatwa.

**Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Alijibu:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo na kabla ya kujibu swali naomba nitoe maelezo mafupi.

Mhe. Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi inazochukuwa za kuimarisha viwanja vya michezo hususan ujenzi wa kiwanja cha mpira wa miguu kilichopo Kangani katika Jimbo la Mtambile kisiwani Pemba, pamoja na juhudi hizo kumekuwa na changamoto nyingi tu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba nijibu swali kama ifuatavyo.

(a) Kiwanja cha Kangaani tayari kimekamilika na tayari kinaweza kutumika kwa kuchezewa michezo mbali mbali.

(b) Ujenzi umekamilika tayari na kiwanja hicho kimeshakabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya na yeye tayari ameshawakabidhi wananchi na wameshaanza kukitumia.

(c) Kweli kiwanja kilizungukwa na majani lakini wizara imeweza jitihada kabla ya kukikabidhi kwa kuagiza wafanyakazi wake kuweza kukifyeka na kiwanja hicho kimekabidhiwa wakati kimeshafyekwa na kimeweza kutumika katika shughuli mbali mbali za kimechezo katika mwezi wa Oktoba. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ametwambia kama kimeshakabidhiwa na kimeshaanza kufanyiwa kazi. Sasa hivi *league* za Zanzibar zinaendelea nataka nimuulize Mhe. Waziri tu wameshapanga katika kucheza *league* hii ya Zanzibar katika kiwanja kile.

**Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mohamed Mgaza Jecha swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, kwa mujibu wa taratibu za mpira wa miguu wa Zanzibar ambazo zinasimamiwa na *ZFF* (*Zanzibar Football Federation*) zina sheria zake na zina mipango yake ambayo imepangwa, wizara haihusiki moja kwa moja juu ya kupanga *league* zichezwe uwanja gani na wapi. Hivyo, nitaomba Mhe. Spika kulitolea ufafanuzi kwamba mipango yote ya mpira wa miguu na kucheza inapangwa na mamlaka hii ya *ZFF* na sio wizara.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri, Makamu Mwenyekiti wa UVCCM Zanzibar kwa majibu yake matamu, manono. Mhe. Spika, lakini katika jibu lake amesema kwamba kiwanja cha Kangani tayari kimeshakabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya na ujenzi umekamilika, na katika maendeleo ya kisasa ya kuendeleza soka letu la Zanzibar na ulimwengu kwa ujumla viwanja vinajengwa katika hali ya kileo ikiwemo huduma mbali mbali za vyoo na kubadilisha nguo kwa ajili ya wachezaji pamoja na waamuzi. Je, kiwanja hicho huduma hizo zipo na kama hazipo kuna mpango gani wa kujenga huduma hizo ili kuendana na hali ya kisasa na kuzidi kuendeleza soka letu la Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Nassor Salim Ali kwa swali lake zuri. Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika kuzingatia inasimamia vyema sera ya michezo imejipanga vizuri katika bajeti ya mwaka huu kuweza kutekeleza ile azma za kuboresha viwanja vyote vya michezo vya kiwilaya.

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba viwanja hivi vya Wilaya vimetengenezwa katika matengenezo ya awali ambayo ni kuweka kifusi, kuweka dongo, kupandisha majani ili viwanja viweze kuchezeka kwa michezo ya awali. Kwa hivyo, natambua kwamba kuna huduma nyingi za kimsingi ikiwemo vyoo na huduma nyengine, naomba kumuwahidi mheshimiwa kwamba katika mpango wetu wa mwaka huu tutalizingatia hilo na viwanja vyote vya Wilaya vitakuwa vinaweza kuchezeka.

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pia kwa vile ametwambia kwamba kiwanja cha Kangani Wilaya ya Mkoani kimeshakamilika, na serikali imejipanga kujenga viwanja hivi kwa kila Wilaya. Je, kwa upande wa Kaskazini Pemba uwanja wa Kishindeni ni hatua gani umefikia kwa sasa.

b) Ni kiasi gani cha fedha ambacho kimetumika au kitatumika kugharamia uwanja huo. Ahsante mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumpongeza Mhe. Maryam Thani Juma kwa swali lake zuri na naomba kumjibu swali lake la nyongeza. Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Micheweni kiwanja cha Kishindeni naomba kumjuilisha kwamba pia nacho kipo tayari na tumeweza kukikabidhi kwa Mkuu wa Wilaya na wameshaanza kukitumia. Vile vile kipo katika hali moja na kiwanja cha Kangani kwa sababu ndio mpango wa *phase I* ambao ulikuwa unaelekeza.

Mhe. Spika, lakini kwa faida ya mheshimiwa naomba kumueleza kwamba kiwanja hiki kimeweza kutumia takriban shilingi milioni 250 katika ujenzi huu wa awali ambapo tulitumia Kampuni ya ***Kim Investment Company Limited*** iliyopo Pemba ambayo hiyo ilikuwa ni *phase I*. Vile vile naomba kumjuilisha mheshimiwa kwamba kiwanja hiki sasa hivi tayari kinatumika na vijana wameanza kukitumia. Ahsante sana.

**Nam. 18**

**Changamoto ya Kukosekana kwa Maji Safi Kijiji cha Nungwi na Fukuchani**

**Mhe. Abdalla Abasi Wadi – Aliuliza:**

Kwa muda mrefu jimbo langu la Nungwi lina matatizo ya maji safi hususan katika vijiji vilivyopo Shehia ya Nungwi na Fukuchani na Mhe. Mwakilishi aliyepita alilipigia kelele sana suala hili.

(a) Je, wizara ina mpango gani juu ya kadhia hii.

(b) Je, serikali haioni umuhimu wa kuharakisha huduma hii ili kuwapa moyo wapiga kura wa jimbo la Nungwi.

(c) Kwa kuwa suala hili limeombwa tangu miaka mitano iliyopita, wananchi wa jimbo la Nungwi unawaahidi nini hasa ukizingatia kauli mbiu ya Rais inayosema “yajayo ni neema tupu”.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati - Alijibu:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali Nam. 18 liloulizwa na Mhe. Mwakilishi lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara kupitia Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) inaendelea na zoezi la kupitia mtandao wa maji kutoka katika vyanzo mbali mbali, vyanzo vitatu vinavyohudumia eneo la

Nungwi kwa kusawazisha mivujo mingi inayotokana na hujuma za watu mbali mbali, pamoja na kuondoa bomba zilizoziba na zilizooza ili huduma hiyo iweze kuwafikia wananchi.
(b) Mhe. Spika, wizara kupitia Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) inaendelea na zoezi hilo kwa kushirikiana na viongozi wa siasa wa Jimbo la Nungwi, na Mkoa na wasamaria wema ili kuharakisha huduma hiyo iweze kupatikana vyema.

(c) Mhe. Spika, kwa kutambua kuwa mji wa Nungwi umekuwa na mahitaji ya maji yameongezeka, Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*) imelizingatia suala hilo la kupitia mradi mdogo wa *Exim Bank* kupitia mkopo wa India kwa ujenzi wa tangi na kulaza bomba kwa baadhi ya maeneo, ili wananchi wa Shehia za Nungwi waweze kufaidika na huduma za maji kama ilivyoahidiwa.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, nilikuwa nina swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kumekuwa kuna *attendance* kwa maeneo ya miji ambayo inafanya shughuli za utalii upatikanaji wa huduma ya maji mara nyingi sana miradi hii huwa inanufaisha zaidi maeneo tu ya uwekezaji. Sasa je, wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba huduma hii ya maji inawanufaisha wawekezaji lakini bila ya kupoteza umuhimu wa wananchi wetu katika kupata huduma maeneo yote takriban ukienda maeneo ya Paje, Jambiani, Michamvi, Chwaka, Uroa, Kiwengwa, Nungwi, Matemwe, Pwani Mchangani kadhia hii ipo. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri atusaidie kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba huduma hii ya maji inapatikana kwa maeneo ya wawekezaji bila ya kuathiri upatikanaji wa huduma hii muhimu kwa maisha ya wananchi wetu waliotuchagua na kutupa idhini ya kuongoza serikali.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mheshimiwa Wizara ya Maji na Nishati kupitia Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) ina mpango wa kufikisha huduma hii ya maji katika maeneo yote ya Zanzibar ikiwemo katika maeneo ya watumiaji wakubwa ambao ni hawa walioelezwa wenye uwekezaji wa utalii.

Mhe. Spika, kupitia mradi mdogo wa India ambao unategemewa kuanza utekelezaji wake katika mwaka huu wa fedha, utarahisisha kupeleka huduma hii muhimu katika maeneo hayo ambayo Mhe. Mjumbe ameyaeleza.

**Utaratibu**

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe. Spika, hoja yangu ni kwamba wenzetu hawa ambao wanafanya miradi ya uwekezaji wanakuwa wana *facility* kubwa za kuweza kuya-*pump* na kuyavuta maji. Sasa wananchi wetu ambao wanasubiri maji katika utaratibu ule wa bomba la kawaida hayafiki, ndio swali langu lilipo.

Je, serikali ina mpango gani kwa kuiona kadhia hii ili wananchi wetu waweze kupata maji, vyenginevyo serikali itakuwa inapeleka miradi ya maji inawanufaisha wachache na wananchi wetu wanaendelea kutumia maji kwa kufuata ndoo. Hilo tu Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante, nadhani serikali imeshalisikia litafanyiwa kazi. Mhe. Ali Suleiman Mrembo.

**Mhe. Ali Suleiman Ameir:** Nikushukuru Mhe. Spika, lakini nimshukuru pia Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Wananchi wa Jimbo la Pangawe ni miongoni mwa wananchi ambao wana tatizo la ukosefu wa maji safi na salama ambapo inasababishwa na uchakavu wa miundombinu pamoja na baadhi ya watendaji wa Mamlaka ya Maji.

Je, Mhe. Waziri yuko tayari kufuatana na mimi kwenda kuiangalia miundombinu hiyo kwa lengo la utatuzi wa uchakavu wake.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza. Kwanza nikiri kwamba kweli kuna matatizo ya miundombinu chakavu ambayo inapelekea upotevu wa maji, lakini nimuahidi kwamba niko tayari kufuatana naye mguu kwa mguu kupita katika jimbo lake kitongoji kwa kitongoji kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto hii. (*Makofi*)

**Mhe. Asha Abdalla Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Pamoja na kuondoa mabomba yalioziba na mabomba chakavu, na tunafahamu kwamba wananchi wa Jimbo la Mahonda hususan Mahonda, Kazole na Mfenesini kuna miundombinu ya maji ambayo ilitolewa wakati wa ujenzi wa barabara ya Mkokotoni – Bububu. Je, ni lini miundombinu hiyo itarejeshwa ili wananchi wapate huduma hiyo.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la Mhe. Asha Abdalla Mussa la nyongeza. Mheshimiwa nikiri kwamba ujenzi wa barabara katika eneo hilo la Mahonda uliathiri miundombinu ya maji na wizara kupitia Mamlaka ya Maji (*ZAWA*), kupitia mradi mkubwa wa uwekaji wa mabomba pamoja na ujenzi wa matangi utakaoanzia Fumba hadi Mahonda utarekebishao miundombinu hiyo na upatikanaji wa maji utaendelea kupatikana kama kawaida. Kwa sasa tutaendelea kuwapatia maji kwa huduma ya mitandao ambayo tuko nayo ambayo tumeanza kuirejesha mheshimiwa.

**Nam. 52**

**Matengenezo ya Barabara za Ndani**

**Mhe. Haji Shaaban Waziri** – Aliuliza:

Tunaipongeza serikali kwa jitihada zake za kuhakikisha miundombinu ya barabara inakuwa imara na kupitika kwa urahisi. Je, serikali inatumia vigezo gani katika kuhakikisha barabara zisizopitika zinajengwa kwa wakati.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** – Alijibu:

Ahsante Mhe. Spika, kabla sijaendelea kujibu swali lake naomba kumshukuru Mhe. Haji Shaaban Waziri kwa kuipongeza serikali kwa jitihada zake na kuhakikisha kwamba

miundombinu ya barabara inakuwa imara na kupitika kwa urahisi. Tunamshukuru sana kwa kuziona jitihada zetu.

Mhe. Spika, sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, vigezo vinavyotumiwa na wakala wa barabara katika kujenga barabara ni pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, ahadi za viongozi pamoja na maagizo mbali mbali yanayotolewa na serikali.

**Mhe. Haji Shaaban Waziri:** Ahsante Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Kiboje – Kizimbani ni barabara ambayo ina ahadi ya muda mrefu tokea Rais Amani Abeid Karume kulikuwa kuna ahadi ya kutengeneza barabara hiyo. Mhe. Waziri amesema miongoni mwa hayo ni ahadi pamoja na ilani na hata ukiangalia ilani zilizopita nyingi zilizungumzia kujenga barabara hiyo. Sasa anambie je, lini barabara hiyo itaanza. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo. Katika jibu langu lililopita nimejibu kwamba miongoni mwa vigezo ni maagizo mbali mbali yanayotolewa na viongozi wa serikali. Katika suala la ujenzi wa barabara huwa tunapokea maagizo mbali mbali wakati tayari tumeshapanga kwamba mpango kazi huu tutajenga barabara moja, mbili, tatu, lakini ndani ya mpango huo huwa tunapokea maagizo kutokana na haja ambazo zinatokezea. Kwa hivyo, tunafuata maagizo yanayotokana na serikali. (*Makofi*)

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Ahsante Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi naomba kumuuliza swali dogo tu Mhe. Waziri pamoja na kumpongeza kwa majibu yake mazuri juu ya barabara ya Kizimbani – Kiboje.

Mhe. Spika, kama tunavyotambua kwamba miradi ya barabara ni miradi yenye gharama kubwa na ujenzi wake unatumia fedha nyingi sana za walipa kodi. Kama tunakumbuka vizuri barabara ya Amani – Dunga tulizindua mwaka 2013 kwa maana ya kwamba ni kipindi ambacho takriban miaka sita mpaka saba hadi leo hii. Barabara hii imetumia gharama kubwa sana fedha za wananchi lakini hali yake kwa hivi sasa haiko vizuri.

Je, wizara ina mpango gani wa kuihami barabara hii ili isije ikaharibika tukarudi kwenye gharama kubwa za ujenzi kinyume na matarajio ya serikali na kinyume na matarajio ya wananchi.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza. Katika ujenzi wa barabara tunajua serikali inatumia gharama kubwa sana na serikali inakuwa haina uwezo wa moja kwa moja kujenga hizo barabara, isipokuwa zinafanya mazungumzo na wafadhili mbali mbali kwa kukopa kwa kupitia *BADEA*, *SAUD FUND*, *WORLD BANK* na wengineo. Kwa hivyo, tumo katika muendelezo huu kwa hizo fedha kwa ajili ya kuzijenga barabara zote hizo ikiwemo barabara ya Kizimbani – Kiboje. Kwa hivyo, barabara ya Kizimbani – Kiboje itakuwa ni miongoni mwa mpango kazi wetu wa miaka mitano. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwenye majibu yake mama Mhe. Waziri amesema kwamba vigezo vya ujenzi wa barabara hizi ni ahadi za viongozi na Mhe. Spika, kama unakumbuka kwamba barabara kongwe ya Wete/Chake Chake kuna mikataba ambayo imesainiwa kwa ajili ya ujenzi huo. Je, kwa sasa ni hatua gani ambayo imefikia kutokana na ujenzi huo wa barabara ya Wete – Chake Chake.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Maryam Thani wa Jimbo la Gando swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Naomba kumwambia tu katika ujenzi wa barabara ya Wete – Chake Chake utaanza hivi karibuni, kwa sababu kulikuwa kuna matatizo ya kimkataba na tayari mkataba umeshakaa sawa kwa hivyo wakati wowote tutaendelea kujenga barabara hiyo *In Shaa Allah*. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa nazidisha muda kidogo ili tumalize swali lililobaki halafu tuende kwenye masuala mengine. Karibu.

**Nam. 22**

**Uvuvi wa Kati wa Bahari Kuu kwa Wavuvi Wadogo Wadogo**

**Mhe. Hassan Hamad Omar** – Aliuliza:

Kufuatia kauli ya Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi ya kutaka kuifanya Zanzibar kuwa ya uchumi wa buluu ambao kwa kiasi kikubwa itakuwa ni pamoja na uvuvi wa kati na bahari kuu.

(a) Je, serikali ina mpango gani katika kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo (hasa wa Kojani) ili kufikia katika uvuvi wa aina hiyo.

(b) Wavuvi wengi wadogo wadogo wa Zanzibar wanaovua uvuvi wa asili kwa taaluma ya kurithishana kizazi baada ya kizazi. Je, wizara yako ina mpango gani katika kuwapa taaluma wavuvi hawa ili kuendeleza uvuvi kufikia uchumi wa buluu.

(c) Kwanini wizara imekuwa na miradi ya kutunza mazingira ya bahari lakini imeshindwa kuwa na miradi ya kuendeleza wavuvi kitaaluma na kuwawezesha (mikopo).

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi** - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali imeanza kutekeleza mipango ya kuwapatia mafunzo ya kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo ili wafikie katika uvuvi wa uchumi wa buluu kwa kuwaunganisha na taasisi za kifedha ambazo zimekubali kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu. Wizara tayari imeshafanya mazungumzo na taasisi za kifedha ikiwemo *Equity Bank*,

*CRDB* na *NMB Bank* kwa ajili ya kuwapatia mikopo wavuvi hao. Tayari vikundi 112 (59 Pemba na Unguja 53) vimeshawasilishwa kwenye mabenki hayo kwa kuanza kupewa elimu.

(b) Mhe. Spika, serikali ina mpango wa kuwapatia taaluma wavuvi wadogo wadogo wa Zanzibar wanaovua uvuvi wa asili kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali kupitia makongamano na warsha. Aidha, serikali imekamilisha ujenzi wa vyuo vya elimu ya amali huko Mtambwe Pemba na Makunduchi Unguja, ambapo mbali na taaluma nyengine vyuo hivyo vitakuwa na mtaala wa fani ya uvuvi kwa madhumuni ya kuendeleza wavuvi. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imeunda kitengo kinachoshughulikia uvuvi wa kienyeji kwa ajili ya kuwapatia elimu wavuvi hao.

(c) Kama nilivyoeleza hapo awali katika jibu langu, wizara ina miradi ya kutunza mazingira na bahari na kuwaendeleza wavuvi kitaaluma kwa kuwawezesha kupata mikopo nafuu na kuwapatia mafunzo. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, nashukuru sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini nina swali la nyongeza. Mheshimiwa kumekuwa na kadhia kubwa sana kwa wavuvi wadogo wadogo ambao ni wavuvi asilia na Mhe. Rais wa Zanzibar anatangaza uvuvi wa kuelekea uchumi wa buluu ambapo wavuvi wanataka wapate taaluma ya kutosha, lakini kuna kadhia ya kuwakamata mara kwa mara wanapokuwa uvuvini.

Mhe. Spika, ndani ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na kuna wataalamu wanapenda kuwaona ng’ombe na watu wa kilimo wanaona bwana shamba anakwenda kuelekeza kule, lakini hatujawahi kuona hata siku moja katika Idara au Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwenda kwenye *site* baharini kuonesha namna gani samaki wa kibua, mbono na samaki wengine wanavuliwa namna gani.

Mhe. Waziri naomba kumuuliza ni siku gani wataalamu wake watafika kule baharini kwenda kuwaona wavuvi jinsi wanavyovua na kuleta samaki juu ili kuwasaidia watu.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, vijana wangu wana taaluma ya uvuvi, wanatoa taaluma hiyo katika makongamano mbali mbali, hatuwezi kuingia katika bahari kila siku na mtu mmoja mmoja tunachokifanya ni kwamba tunatoa elimu kwa njia ya makongamano katika vikundi mbali mbali. Hizo ndizo taratibu tunazozifuata mheshimiwa.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa wavuvi wengi sana umewagusa itabidi nianze na wavuvi kwanza.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mheshimiwa pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri pamoja na wataalamu aliokuwanao katika wizara yake lakini wavuvi wengi wanalia sana kuhusu masuala ya kunyanyaswa baharini hususan wavuvi wa majongoo na kome, nadhani anawajua. Majongoo yana thamani zaidi kuliko hata karafuu mara nyingi huwa nazungumza.

Je, Mhe. Waziri wizara yake ina mpango gani kuhakikisha kwamba tunakwenda katika uchumi wa buluu pamoja na majongoo kuhakikisha kwamba biashara ile ya majongoo yakiwemo Pauni, Barango, Spinyo, Kijino inarudi mwanzo hapa Zanzibar ili kuhakikisha kwamba uchumi wa buluu tunakwenda huko unakotakiwa. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Kwanza nikiri kwamba suala la majongoo ni uvuvi ambao unaweza kuzidi hata karafuu kwa kipato, nikiri hicho. Nataka nimueleze kwamba tayari wizara yangu imeanza kutoa elimu ya masuala ya uvuvi wa majongoo kwa vikundi mbali mbali na naomba nimuarifu Mhe. Mwakilishi kwamba tarehe 27 mwezi huu tuna kongamano kubwa sana la uvuvi wa majongoo namualika namuomba afike hapo. (*Makofi)*

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimpongeze waziri kwa majibu yake mazuri. Ni hivi karibuni tu mwezi uliopita walikamatwa wavuvi 40 katika eneo la Fumba kwa kutuhumiwa kuvua katika maeneo ya hifadhi. Wavuvi wale 36 waliachiwa manahodha wanne wakalala Kituo cha Polisi kwa muda wa siku moja na siku ya pili wakaachiwa. Je, kinachotakiwa pale Mhe. Waziri samaki wale walikaa kwa muda wa masaa sita na wengine wakaharibika ni kuzuwia mitego au kuwaruhusu wale wanne wasilale ndani.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mheshimiwa suala hili la kukamatwa wavuvi mimi nalielewa na hiyo kesi anayoizungumza naielewa, ni kweli baadhi ya wavuvi wamekamatwa na baadhi wamewekwa ndani, lakini suala la samaki kuwekwa masaa sita taratibu za kisheria ni lazima zifuatwe mheshimiwa. Kwa hivyo, wale wamewekwa pale na *in fact* Mhe. Mwakilishi alikuja ofisini kwangu na nikamueleza, wamewekwa pale ili kuwaruhusu mahakimu wafike pale watoe ruhusa ya kwamba wauzwe. Kwa hivyo, tunakwenda kulingana na taratibu na sheria za serikali na tumefanya hivyo kwa mujibu wa sheria na taratibu.

**Mhe. Spika:** Ahsante. Mheshimiwa itabidi ustahamili kidogo nifanye upendeleo kwa wavuvi. Mhe. Haji Omar Kheir. *(Makofi)*

**Mhe. Haji Omar Kheir:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kufanya upendeleo huo kwa kutuona sisi wavuvi. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kabla ya kuuliza swali la nyongeza naomba nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa *signing* pamoja na waziri wake kwa *signing* ambayo imefanyika juzi ya kulishughulikia suala hili la uvuvi au suala la uchumi wa buluu kupitia uvuvi hasa kwa miundombinu ambayo itajengwa pale Mpigaduri.

Baada ya maelezo hayo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mhe. Waziri anajua kwamba yako maeneo tengefu katika visiwa vya Zanzibar ambayo yamekusudiwa kujenga *Cage* kwa ajili ya kuvuna samaki baharini. Kama anajua ni maeneo yepi, lakini mimi nalijua moja kati ya maeneo hayo ni eneo la Popo kule Tumbatu, na kama ni hivyo ndivyo serikali ina mpango gani wa kuweza kuwafuata wavuvi wa maeneo ya Tumbatu na maeneo jirani, Nungwi na kwengineko kwenda kuwapa taaluma juu ya shughuli ile muhimu

ambayo itawasadia wananchi kwa maana ya wavuvi. Lakini vile vile, katika jambo ambalo limeelezwa sana katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

**Mhe. Spika:** Jaribu kufupisha Mheshimiwa.

**Mhe. Haji Omar Kheri:** Ahsante ni Uchumi wa Buluu, na katika uchumi huo nimshukuru sana Mhe. Rais jana ameelezea kwa mara nyengine tena ni pamoja na mafuta, gesi asilia na mazao ya baharini.

Je, serikali kwa sababu inayatambua yale maeneo ambayo tayari rasilimali hizo zipo, atakubaliana na mimi Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa sababu Tumbatu ni eneo moja ambapo rasilimali hizo zote zipo kufuatana na mimi tukaandaa mpango wa kwenda kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa Uchumi wa Buluu. Ahsante sana.

**Mhe: Spika:** Ahsante Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Haji Omar Kheri swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza niseme kwamba, tunapokea shukurani hizo kwa niaba ya serikali lakini nataka nimueleze Mheshimiwa Mwakilishi kwamba, tunaelewa kwamba yapo maeneo tengefu ambayo yanaweza kutumika kwa kufuga samaki, na hilo eneo la Popo tunalielewa. Serikali tayari ina mpango wa kusaini mkataba, bado hatujasaini tuna mpango wa kusaini mkataba wa kuweka shughuli za kufuga samaki katika eneo la Popo.

Swali la Tumbatu Mheshimiwa, wizara yangu inafanya utafiti sio Tumbatu tu maeneo yote ya Zanzibar tunajaribu kufanya utafiti wapi maeneo ambayo tunaweza yatakidhi masuala ya ufugaji wa samaki. Kwa hivyo, Tumbatu, Muwambe, Chokocho tutafika, na sehemu zote tutafika kufanya utafiti wa ufugaji wa samaki. Nashukuru Mheshimiwa.

**Mhe. Spika:** Ahsante, kabla hujaondoka nimpe nafasi ya mwisho ya upendeleo Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Mhe. Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kuniona lakini Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendeleza Azma ya Uchumi wa Buluu Zanzibar.

Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi iliyozungukwa na bahari lakini tumekumbwa na kadhia ya kula samaki wanaoagizwa kutoka nje ya nchi. Mhe. Spika, hii ni aibu kwa Zanzibar kwa nchi ya bahari kula samaki wa peduu. Sasa Mhe. Spika, nimepata wasi wasi kidogo na majibu ya Mhe. Waziri anayesema kwamba tayari wavuvi wa Zanzibar amewaunganisha na Taasisi za Kibenki ili kupatiwa mikopo. Taasisi za kibenki kama tunavyojua jukumu lake ni ku-*make profit* hazitizami mnyonge kumuendeleza.

Sasa Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri lini wataanza utaratibu au mradi maalumu wa kuwapatia taaluma wavuvi wetu wa Zanzibar na vifaa ili tuepuke kula samaki wa peduu Zanzibar.

**Mhe. Spika:** Ahsante, Mhe. Waziri majibu.

**Mhe. Waziri wa:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Nimesema hilo nililolizungumza la kwamba suala la benki ni moja ya *alternative* ambazo tulikuwa tunazitumia lakini zipo njia nyingi za kuwasaidia wavuvi wetu wadogo wadogo.

Moja ni kwamba, wapo wawekezaji kutoka nje tayari wamefika Zanzibar na wamekuja ofisini kwangu wanataka kushirikiana na wavuvi wadogo wadogo wawapatie boti, dhana za kuvua kwa makubaliano maalumu. Wanavua, wanauzia samaki wale wawekezaji kwa bei ya soko na zile gharama za boti pamoja na vifaa zitakatwa kidogo kidogo mpaka wamalizie suala hilo.

Kwa hivyo, ziko njia nyingi Mheshimiwa sio tu benki zipo njia nyingi ambazo kuwa tayari tunazungumza na wawekezaji lakini suala la uwekezaji katika masuala haya ya boti ndogo ndogo ni eneo endelevu linaendelea kidogo kidogo.

Katika suala letu tulilosaini juzi moja ya kiwanda kitajengwa katika mradi huu tulizungumza ni Mradi wa Kutengeneza Boti Ndogo Ndogo kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo. Kwa hivyo, ile bei za boti ambazo tunazitegemea kuzitengeneza hapa Zanzibar zitakuwa ni nafuu na serikali zitaweza kutoa mikopo kwa wavuvi wadogo wadogo. Kwa hivyo, njia nyingi Mheshimiwa ni suala endelevu tunakwenda kidogo kidogo.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako na ndio changamoto wizara ni mpya, maswali ni mengi lakini tunahisi utayamudu wala usione shida. Nashukuru sana.

Waheshimiwa Wajumbe, maswali yamemalizika na kabla hatujaendelea nina matangazo. Tangazo lilokuwepo ni la wageni, wageni wetu wa leo tarehe 10/02/2021. Kwanza ni wageni kutoka Chama cha *ACT* Wazalendo na wageni hao ni kama ifuatavyo:-

1. Ndg. Salim Bimani (Naibu Katibu Mkuu wa *ACT* Wazalendo) karibu sana Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa.
2. Ndg. Hassan Jani Massoud (Mjumbe wa Kamati Kuu ya *ACT* Wazalendo) karibuni sana.

Wageni wanaofuata ni wageni wa Mhe. Kombo Mwinyi Shehe ni Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi *ACT* Wazalendo, wageni hao ni:

1. Ndg. Suleiman Kombo Mwinyi ni mtoto wa Mheshimiwa, karibu
2. Ndg. Mohammed Rajab Ibrahim (Naibu Katibu Mkuu Vijana *ACT* ).

Karibuni sana, wageni wengine ni wa Mhe. Habibu Ali Mohamed wa Jimbo la Mtambwe *ACT* Wazalendo, wageni hao ni:

1. Ndg. Malik Juma Mohammed (Katibu wa Fedha na Udhamini Ngome ya *ACT* Vijana) karibu sana.
2. Ndg. Janet Fusi (Katibu Ngome ya Wanawake *ACT* Wazalendo) karibu sana.

Wageni wengine ni wageni wa Mhe. Omar Said Shaaban nao ni:

1. Alye Pili Khamis (Mama Mzazi wa Mheshimiwa) karibu sana mama uone namna ambavyo Mheshimiwa anapiga kazi humu ndani ya Baraza.

2. Ndg. Massoud Salim Mohammed *(Managing Partner* Said *Attorney and Associates)* ni mshiriki mwenziwe katika Kampuni hii ya Mawakili. Karibuni Baraza la Wawakilishi.

Katibu baada ya shughuli hiyo, shughuli inayofuata tafadhali.

## TAARIFA

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Taarifa Mhe. Spika, wageni wangu wapo juu. *(Makofi/Vicheko)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, wageni wako katika orodha yetu hawamo, lakini niandikie halafu nitawatambua wala haina shida.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Lakini mtu wa mwanzo kutaja wageni ni mimi.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa utaratibu wa wageni hawaji mezani kwa Spika moja kwa moja waheshimiwa tunaomba utulivu kidogo. Utaratibu wa wageni hawaji mezani kwa Spika moja kwa moja wageni wanaratibiwa na Idara yetu ya Uhusiano, halafu baadae wanachapishwa humu na kuletwa hapa. Sasa kama Spika hakuwapata hapa kupitia njia hiyo siwezi kusoma kitu ambacho hakipo nimekupa fursa ya upendeleo Mheshimiwa kwamba niandikie majina ya hao wageni wako yaje hapa mezani wakati tukiwa tunaendelea na hii shughuli, nitasimama kwa ajili ya kuwatambua Mheshimiwa wala hamna tatizo lolote Mheshimiwa.

Katibu shughuli inayofuata.

## UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kwenye *order paper* tunaendelea na shughuli za uchaguzi sasa hivi, na uchaguzi wetu wa mwanzo ni uchaguzi wa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, tuna wagombea wawili ambao wote hao watapigiwa kura ya ndio na hapana.

Mgombea wa mwanzo ni Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na mgombea wa pili ni Mhe. Shaaban Ali Othman. (*Makofi*)

Kabla sijampa katibu kwa ajili ya hizi shughuli, nitawaomba mgombea mmoja mmoja aje huku mbele ajieleze na ataulizwa maswali yasiyozidi matatu na baada ya hapo tutaendelea na shughuli za upigaji kura.

**Katibu:** Mhe. Spika, kama ulivyoeleza sasa hivi tunaendelea na Uchaguzi wa Wenyeviti wa Baraza, na utaratibu uliokuwepo ni wewe Mheshimiwa kuwaita wagombea hao wawili ambao ndio waliojitokeza kupitia ofisini kwangu. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Shaaban Ali Othman, mmoja baada ya mwengine kujieleza na baada ya kujieleza wanatakiwa waulizwe maswali kama yatakuwepo, na kama yatakuwa hayapo utaratibu utakaofuata ni wewe kutoa ruhusa kuendelea kuwapigia kura ambavyo, kura zetu zimekusanya majina ya wagombea wote hawa wawili na watapigiwa kura ya ndio au hapana kwa kila mmoja.

Mhe. Spika, baada ya hapo utaratibu utakaofuata ni kuzihesabu hizo kura na kuzitolea matokeo yake. Kura zitapigwa kwa utaratibu wa kura za siri, Mheshimiwa naomba kuendelea na zoezi hili.

**Mhe. Spika:** Ahsante, kwa mlahaka huo sasa naomba kwa heshima na taadhima nimkaribishe Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ili aje ajieleze. Karibu Mheshimiwa. (*Makofi*)

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Ahsante, Mhe Spika kwa kunipa nafasi hii nisimame mbele ya hadhara hii au mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kusema machache na kuomba ridhaa kwa wajumbe hawa waliokuwepo hapa, wanichague niwe Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, niliosimama mbele yenu naitwa Mwanaasha Khamis Juma ni Mwakilishi wa Jimbo la Dimani. Nawaomba sana mnipe ridhaa ili niweze kufanya kazi pamoja na nyinyi kwa kumsaidia Mhe. Spika kwa kuliendesha Baraza hili Tukufu. Waheshimiwa Wajumbe, nawaomba sana kura zenu za ndio ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante, maswali waheshimiwa, yapo maswali sasa tuanze na nyuma kabisa Mhe. Shaib Hassan Kaduara Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante, Mhe. Spika kwa kunipa fursa hii, Mheshimiwa inaonekana huku nyuma inakuwa hunioni mara nyingi naona mpaka ulitaka kuweka miwani. *(Kicheko).*

Naomba nimuulize mgombea wa nafasi hii Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, kwa vile namuelewa sana amekuwa mwenyekiti wangu katika Kamati ya *LAAC.* Mheshimiwa iwapo tutakupa ridhaa hii unatuahidi kitu gani yale mazuri ambayo uliokuwa unatufanyia *LAAC* tunaweza tukayapata katika uwenyekiti wako? Ahsante sana.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii Mheshimiwa kwa swali lako zuri. Mheshimiwa nadhani kikubwa nitakachokupatia au ninachotaka tushirikiane katika kuliendesha hili Baraza. Pia nikuombe sana Mheshimiwa mazuri utakayoyapata humu ikiwa ni kumsaidia Spika ni kufuata taratibu za sheria pamoja na kanuni

ambazo tumejiwekea sisi wenyewe basi hili nadhani litakuwa kwako ni zuri sana na kufuata. Kwa hiyo naamini utapata yale ambayo unahisi yanastahiki kupatiwa katika chombo hichi. (*Makofi*)

**Mhe. Harusi Said Suleiman:** Ahsante Mhe. Spika, mimi naomba nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru katika kipindi cha Baraza La Tisa uongozi wa Mhe Mwanaasha Khamis Juma ulivyokuwa mzuri. Mheshimiwa alituongoza kwa ujasiri kutokana na mashirikiano yako wewe uliyompa pamoja na Mhe. Naibu Spika.

Mimi napenda nimuulize swali moja, kajipanga vipi katika uongozi wake wa uwenyekiti tutakapomchagua kukusaidia Mhe. Spika na Mhe. Naibu Spika katika uongozi wake. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Mhe. Spika Ahsante, naomba nimjibu Mhe. Harusi Said Suleiman kwa kwamba nimejipanga vipi. Mheshimiwa swali langu au jawabu langu litakuwa sawa sawa na lile nilomjibu Mhe. Shaib Hassan Kaduara. Kujipanga kwangu ni kufuata Taratibu na Sheria za Kanuni za Baraza katika uendeshaji wangu. Kwa hivyo, nadhani na yeye amesema kwamba wewe ulisaidia sana kutuongoza sisi wasaidizi wako basi nadhani kupitia ile miongozo ambayo Spika ataiongoza basi nadhani ndio mipango yangu ambayo nimeipanga.

**Mhe. Spika:** Ahsante, Mhe. Suleiman Makame Ali swali lako la mwisho la nyongeza.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Mwenyekiti wa Baraza, Mhe. Mwenyekiti umesema kwamba, utafuata Taratibu na Kanuni za Baraza. Ni kweli, kanuni tumezitunga wenyewe humu ndani na sheria tunazifuata sisi wenyewe lakini, kanuni hiyo hiyo *time* nyengine inatunyima mnapokaa pale kwenye kiti hususan kwenye kupitisha vifungu. Sasa nataka nijue, Je, wajumbe haki yetu utailindaje kuhakikisha kwamba tunapata haki yetu ya wajibu ambayo kwamba tunastahiki kupata humu ndani ya Baraza.

**Mhe**. **Mwanaasha Khamis Juma: A**hsante Mhe. Spika, naomba nimjibu swali lake Suleiman Makame Ali. Mheshimiwa, ndani ya hizo kanuni zetu za Baraza zina taratibu hata kukipa fursa kitu kinachoendesha pale kuona jambo hili linafaa au halifai kwa idhini ya Spika na nikisema idhini ya Spika, ni sawa sawa na yule mtu yeyote atakayekaa katika kile kiti. Kwa maana hiyo, kanuni hizo hizo zimetupa mamlaka waendeshaji katika kile kiti kuona kipi kinafaa na tunaweza tukakifanya na kipi hakifai kinawezekana tusikifanye. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwanaasha kwa hayo majibu, maswali matatu yamemalizika. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Shaaban Ali Othman na yeye aje ajieleze. (*Makofi*)

**Mhe. Shaaban Ali Othman:** Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu. Lakini pili, niwashukuru wajumbe wenzangu hasa wajumbe wapya ambao umetoka kuwaapisha mda mchache uliopita.

Kabla ya kujieleza, Mheshimiwa kwa ridhaa yako napenda kwanza nishukuru na kumpongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushindi mkubwa wa kishindo alioupata katika uchaguzi mkuu uliopita pamoja na

yeye nimpongeze Maalim Seif Sharif Hamad Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Mhe. Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, niliosimama mbele yenu naitwa Shaaban Ali Othman ni Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mpendae nimesimama kwa nia moja tu kuomba ridhaa ya kuchaguliwa na nyinyi kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi kwa kipindi hichi.

Mhe. Spika, nimejishauri na nimekubaliana na nafsi yangu kwamba kwa mashirikiano yenu ninaweza kuwa mmoja kati ya wachache wa viongozi ambao wanaweza kuliongoza Baraza hili. Kwa hiyo, kwa mnasaba wa maelezo hayo niwaombe ndugu wajumbe wakiongozwa na wewe Mhe. Spika, kuniamini na kunipa kura za ndio ili tuweze kushirikiana katika Muhimili huu Mkubwa wa nchi yetu. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Shaaban Ali Othman, Waheshimiwa Wajumbe kama kuna maswali. Namuona Mhe. Omar Said Shaaban, atauliza swali la kwanza.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante Mhe. Spika, kwa nafasi ya kuuliza swali kwa mgombea. Mhe. Mgombea kuna msemo wa kiingereza unaosema *let the majority have their way and the minority have their say*. Baraza hili la Kumi ni la mchanganyiko wa vyama zaidi ya kimoja tofauti na ilivyokuwa Baraza la Tisa na kwa bahati mbaya sababu ambazo nisingependa kuzieleza, chama kimoja kina wawakilishi wachache ndani ya Baraza. Hebu tunaomba *commitment* yake, ni vipi ataongoza Vikao vya Baraza huku akihakikisha Baraza haliwi *dominated* na wajumbe au kutoa fursa kwa wajumbe wa chama kimoja na kuhakisha hata wale wachache anawapa fursa waweze kutoa mchango wao. Ahsante.

**Taarifa**

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Spika, Taarifa kidogo.

**Mhe. Spika:** Naam, inahusu nini Mheshimiwa.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mzungumzaji aliezungumza kwamba katika kipindi kilichopita, yaani ametofautisha kwamba vyama vilivyokuwemo ndani na vile vilivyokuwepo kwa kipindi kile. Nilitaka nikumbushe tu kwamba katika Baraza lilopita tulikuwa na vyama zaidi ya vinne. (*Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante kwa kuweka sawa *hansard*. Mhe. Shaaban Ali Othman naomba ujibu.

**Mhe. Shaaban Ali Othman:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nilijibu tu swali la Mhe. Omar Said Shaaban. Kwanza napenda kumshukuru sana Mhe. Shamata Shaame Khamis kwa kunisaidia kujibu, lakini kwa ufafanuzi ni kwamba licha ya kuwa tuko kwenye Baraza ambalo lina vyama tofaufi vya kisiasa, uwepo wangu hapa na kwa mujibu wa nafasi nilioiomba nitaongozwa zaidi na Kanuni za Baraza kuliko utashi wa kisiasa ama chama cha siasa nnachotokana nacho.

Kwa majibu hayo naomba nimtoe hofu  Mhe. Mwakilishi kwamba asitarajie kubaguliwa kwa uchache wake wala asitarajie kupendelewa kwa chama tawala kwa wingi wao. Zaidi kanuni ndio zitatumika katika kutuongoza wote kwa pamoja. *(Makofi)*

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** *Bismillah Rahman Rahiim,* Mhe. Spika, mimi nitaomba nimuulize swali Mhe. Shaabani Ali Omar kwa kuwa kwenye fomu yake mimi pia ndie niliemdhamini na Mhe. Panya Ali Abdalla, na mimi sidhamini mtu bure bure. Mhe. Shaabani Ali Omar atakapokuwa kwenye kiti atachukua hatua gani kwa mjumbe yoyote atakaefanya fujo.
**Mhe. Shaaban Ali Omar:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf swali lake, swali lake halitofautiani sana na swali la Mhe. Omar Said Shaaban, na majibu yangu yatakuwa yanafanana. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf, Kanuni zinazotuongoza ndani ya Baraza ndizo zitakazotoa hukumu kwa yoyote atakaekwenda kinyume na kanuni hizo.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa. Aa kuna Mhe. Hassan Khamis Hafidh nae, haya.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Mhe. Spika, naomba sana nikushukuru kwa kuniona lakini namshukuru ndugu yangu kwa kuthubutu kugombea hii nafasi kadhalika kwa mujibu yake mazuri. Mhe. Spika, naomba kumuuliza kwamba anapokuwa mwenyekiti, nafasi anayoigombea pia anakuwa ni *presiding officer* kuiwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Mabunge ya Jumuiya ya Madola, wanaita *CPA.*

Sasa naomba kumuuliza kwamba amejipangaje katika kuliwakilisha Baraza hili Tukufu katika Mabunge hayo ya Jumuiya ya Madola.

**Mhe. Shaaban Ali Omar:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yake napenda nimjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh swali lake, kikubwa ni kwamba katika kufikia hilo ambalo amelieleza, mimi kwa nafasi yangu nitajikita zaidi kwenye kijifunza kwa viongozi ambao wapo na wamenitangulia. Kwa hivyo, kupitia kwao na ushirikiano wao watakaonipa nnaamini yale yote ambayo wanayauliza yatapata majibu yaliyo sahihi. (*Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Shaabani Ali Othman, unaweza ukarudi kwa ajili ya kukaa. Waheshimiwa kabla hatujaingia kwenye kugawana kura. Katibu nitahitaji kupata idadi ya wajumbe waliokuwemo na baada ya hapo, kura zigaiwe na kura hizi ni za ndio na hapana kwa wajumbe, na baada ya hapo tutafanya hesabu. Kwa hiyo, Katibu tulikuwa tunaomba usimamie hili suala la hesabu tupate idadi yao halafu muanze kugawa kura.

**Katibu:** Sawa Mhe. Spika, nitaomba wahudumu wangu wa hesabu wajumbe waliokuwepo na baadae kwa ruhusa yako tuendelee na zoezi ambalo umelitaja.

**Mhe. Spika:** Kwa wale wajumbe ambao wapo nje ningewataka warudi ndani pia. Waheshimiwa Wajumbe zoezi la kuhesabu pamoja na kugawa kura likiendelea naomba nikamilishe lile ombi la Mhe. Hassan Hamad Omar la kutambuliwa wageni wake ambao wapo *Gallery* na wageni wenyewe ni Mhe. Kombo Rashid Ali, alikuwa Mgombea wa Ubunge Jimbo la Kojani, pia naomba nimtambue Ndugu Omar Mohammed Ali, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Wavuvu Kojani, karibu sana. Ahsanteni sana karibu.

**Katibu:** Mhe. Spika, baada ya zoezi la hesabu, tumepata wajumbe 71 ukiwemo na wewe Mheshimiwa. Tunaomba tuzigawanye.

**Mhe. Spika:** Ahsante, kura zigaiwe.

(*Hapa Wajumbe walipiga kura* )

**Mhe. Spika:** Katibu naomba tuvione visanduku hivyo vya kutumbukizia. Haya sasa vipitishwe kwa ajili ya kuanza kukusanya hizo kura. Waheshimiwa Wajumbe nyote mmeshapata kura na mmeshatumbukiza kwenye visanduku.

Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu orodha hii ni kubwa, mimi ningeshauri kwamba hizi kura sasa, nimruhusu katibu pamoja na watendaji wake wakazihesabu lakini wakati zoezi hilo linafanyika tuendelee na hizi chaguzi nyengine kwa ajili ya kuokoa muda. Vyenginevyo, tukiakhirisha sasa hivi, halafu turudi tufanye uchaguzi mwengine, tuakhirishe tena turudi, hii *process* itachukua muda mrefu. Kwa hivyo, naomba mniridhie kwamba watendaji wetu kupita katibu, lakini nitawaomba wagombea kama wataiamini meza ili ikafanye hiyo kazi kwa niaba yao au kama wanataka na wao wenyewe waende, mimi nitakuwa sina pingamizi.

Wagombea, mnaiamini meza.

**Wagombea:** Ndio.

**Mhe. Spika:** Ahsante, kwa hiyo, katibu nafikiri unaweza ukawaruhusu watendaji wako wakafanye hiyo hesabu ili na sisi tuweze kuendelea na zoezi linalofuata.

**Katibu:** Sawa Mheshimiwa, kwa ruhusa yako nazitoa hizi kura ili tuendelee na zoezi kama ulivyosema.

## UCHAGUZI WA NAFASI TANO ZA WAWAKILISHI KUINGIA KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Katibu:** Mhe. Spika, uchaguzi unaofuata ni nafasi ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano kutoa Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wenyewe ni;

Mhe. Ameir Abdalla Ameir
Mhe. Bakar Hamad Bakar
Mhe. Bahati Khamis Kombo
Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
Mhe. Suleiman Haroub Suleiman

Mhe. Spika, majina hayo ya wajumbe watano ndio ambao wamechukua *form* katika Afisi yangu na ndio walioridhiwa na chama kuendelea na Uchaguzi wa Wabunge hao. Mheshimiwa naomba tuendelee.

**Mhe. Spika:** Ahsante, naomba sasa nimkaribishe mmoja mmoja katika wajumbe hao ili waje wajieleza hapa na baadae wakishakukamilika wote watano nao tutawapigia kura kama utaratibu ambao unakwenda na kura hiyo itakuwa ni ya ndio na hapana kwa sababu watu wenyewe ni watano tu.

Kwa hivyo, naomba nimkaribishe mtu wa mwanzo, Mhe. Ameir Abdalla  Ameir , aje ajieleze na utaulizwa maswali yasiopindukia matatu.

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezimungu kwa kutujaaliwa kuwa wazima wa afya na kuwepo hapa leo, lakini kabla sijasema mengi au machache kidogo napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar ambae ameanza kwa kasi nzuri kabisa na hata tunaona Hotuba yake ya Mwanzo tu imeanza utekelezaji wake katika nyanja tofauti tofauti. Naomba tumpongeze kwa pamoja na sote.

Pili, nimshukuru Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla ambae na yeye hii kasi anayokuja nayo si ya *4G* ni ya *18G*. Naomba tumpongeze kwa hilo na yeye.

Vile vile, nimpongeze Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na nikupongeze wewe pia Mhe.  Spika kwa uteuzi huo na unatuongoza vizuri Mungu azidi kukupa wepesi.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Zaidi leo nimesimama hapa mbele yenu...

**Mhe. Spika:**  Mheshimiwa usitumie zaidi ya dakika tatu.

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Nimesimama mbele yenu kuomba ridhaa moja ya kuomba Uwakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwaombe wajumbe kunichagua ili niweze kuwawakilisha. Ahadi yangu kwenu ni uajibikaji, uadilifu na utekelezaji wa yale yote ambayo mtanipa niyapeleke kwa ajili ya kuyatetea. Ahsante, nnawashukuru sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante Waheshimiwa. Mswali kutoka kwa wajumbe, maarufu hakuna, naomba ukakae. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Bakar Hamad Bakar.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Ahsante, nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, kwa jina ni Bakar Hamad Bakar, ni Mwakilishi wa Jimbo la Wawi, nimesimama mbele hapa kuomba ridhaa ya wajumbe ukiwemo na wewe kuchaguliwa kwa nafasi ya ubunge katika nafasi hizi tano katika kwenda kuliwakilisha Baraza hili Tukufu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika pamoja na wajumbe naomba kura zenu za ndio niwe Mwakilishi wenu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mhe. Spika:** Ahsante , Maswali Waheshimiwa. Swali lipo Mhe. Omar Said Shaaban.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa fursa ya kuuliza swali. Nataka kumuuliza Mgombea anataka ridhaa yetu tuweze kumgipia kura akawe mwakilishi wa Baraza ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano. Swali langu kweke ni kwamba hebu atuambie ni nini Ajenda ya Baraza la Wawakilishi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Mhe. Spika, ajenda, kinachotuunganisha kikubwa Baraza hili pamoja na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muungano wetu. Nnaamini yale ambayo tutayajadili yatahusu muungano wetu wa nchi zetu mbili na si chengine.

**Mhe. Spika:** Swali jengine, ahsante Mhe. Bakar Hamad Bakar.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Nashkuru sana, ahsanteni sana.

**Mhe. Spika:** Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Bahati Khamis Kombo.

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naitwa Bahati Khamis Kombo ni Mwakilishi wa Jimbo la Chambani Mkoa wa Kusini Pemba. Ndugu Wajumbe wenzangu nimesimama mbele yenu kuomba ridhaa ya kura zenu ili niweze kwenda kusimamia na kutekeleza yale yote mazuri ambayo mtanipa katika Baraza letu hili tukufu, lakini pia kuitetea Zanzibar.
Mhe. Spika, naomba ridhaa zote za kura za Wajumbe wetu. Ahsanteni sana.

**Mhe. Spika:** Maswali?

**Wajumbe:** Hakuna.

**Mhe. Spika:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nimwite Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis nae aje kujieleza.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa kuomba ridhaa ya Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako hili kutekeleza shughuli ambayo tumeipanga asubuhi hii ya leo. Aidha Mhe. Spika, niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu na hasa wale ambao leo asubuhi wamekula kiapo kwa kuweza kuja kushirikiana na sisi katika kueteleza majukumu ya kitaifa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jina langu naitwa Mwantatu Mbarak Khamis nimesimama hapa ya kuomba ridhaa za Waheshimiwa Wajumbe wanipe ridhaa ili nikawakilishe Baraza letu tukufu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima Waheshimiwa Wajumbe naomba kura zenu za ndio. Ahsante. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante naomba maswali Waheshimiwa.

**Wajumbe:** Maarufu.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis unaweza kwenda kupumzika.

Naomba nimwite sasa Mjumbe wetu wa mwisho Mhe. Suleiman Haroub Suleiman (Bapee).

**Mhe. Suleiman Haroub Suleiman:** Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, leo hii kukutana hapa tukiwa wazima, afya na siha. Kwa jina naitwa Suleiman Haroub Suleiman ni Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki lakini kwa leo hii sina mengi ya kuzungumza hapa ni miongoni mwa wagombea wa nafasi ya Ubunge kuliwakilisha Baraza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania. Hivyo, basi niko hapa mbele ya Wajumbe kuomba ridhaa ya kura ya ndio ili niweze kuliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante maswali.

**Wajumbe:** Maarufu

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Suleiman Haroub Suleiman.

Katibu naomba kura zigaiwe na hesabu yetu kama imebadilika.

**Katibu:** Mheshimiwa bora turuhusu tu wahesabu tena kwa sababu kuna ingia toka ya Wajumbe ni vyema tukajiridhisha idadi yao.

**Mhe. Spika:** Naomba mhesabu.

**Katibu:** Bahati nzuri wamefanya hiyo hesabu wako 72 pamoja na wewe mwenyewe Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante.

**Katibu:** Naomba niendelee na kuwagaia kura zao.

**Mhe. Spika:** Ahsante naomba sasa katibu kura zikusanywe.

**Katibu:** Mhe. Spika, zoezi la kuhesabu kura limemalizika kwa ruhusa yako naomba nitoe masanduku ya kura ili tuendelee na zoezi la kuzihesabu na kukupatia matokeo.

**Mhe. Spika:** Ahsante. Masanduku yanaweza yakatoka sasa. Wagombea ubunge nadhani meza mnaiamini au vipi. Naam zoezi linalofuata katibu.

**Katibu:** Mhe, Spika, zoezi linalofuata ni uchaguzi wa Umoja wa Wajumbe Wanawake wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar (UWAWAZA)

**Mhe. Spika:** Ahsante. Endelea.

**Katibu:** Mhe. Spika, katika kuratibu uchaguzi wa Umoja wa Wanawake wa Baraza la Wawakilishi Afisi yangu imepokea majina nafasi za uchaguzi huo pamoja na Wajumbe ambao wameonesha nia ya kugombea hizo nafasi.

Nafasi ya kwanza ni ya Mwenyekiti wa UWAWAZA ambayo amechukuwa fomu Mhe. Dr. Saada Salum Mkuya. Nafasi ya pili ni nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa UWAWAZA Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis amechukuwa fomu ya nafasi hiyo na nafasi nyengine ni nafasi ya Katibu wa UWAWAZA ambapo Mhe. Anna Athanas Paul amechukuwa fomu ya nafasi hiyo.
Nafasi nyengine ni nafasi ya mtunza Hazina ya UWAWAZA ambapo Mhe. Panya Ali Abdalla amechukuwa fomu kwa ajili ya nafasi hiyo na kumalizia kuna nafasi za Wajumbe wa Kamati Tendaji ya UWAWAZA ambapo Wajumbe wanne Mhe. Bahati Khamis Kombo wa pili Mhe. Mwanajuma Kassim Makame wa tatu Mhe. Rukia Omar Ramadhan na wa nne Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma Wajumbe hawa wamechukuwa fomu kwa ajili ya nafasi ya Wajumbe wa Kamati Tendaji ya UWAWAZA. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha kwako kwa utaratibu unaofuata.

**Mhe. Spika:** Ahsante, Katibu. Naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe tuendelee na huu uchaguzi. Kwa hiyo, naomba niwaite ili waje wajieleze. Naomba kwa sababu ya hii orodha niwaite wote waje wajieleze na halafu tutampigia kura moja baada ya mwengine. Lakini naomba nianze na Mhe. Dr. Saada Mkuya Salum kwa nafasi ya Uenyekiti wa UWAWAZA ili aje ajieleze hapo

**Mhe. Dr. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mbele yenu naitwa Saada Mkuya Salum na ni Mwakilishi wa Kuteuliwa katika nafasi ya Rais wa Zanzibar na nimechukua nafasi hii ya kugombea Uenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Wawakilishi Zanzibar.

Sasa kwa taadhima naombeni mnipe kura zenu nyote wanawake na wanaume katika Baraza hili la Wawakilishi ili tuweze kusimamia ajenda ya usawa wa kijinsia katika Baraza Tukufu hili lililokuwepo.

Mhe. Spika, nakuomba kura yako Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nakuomba kura yako ahsanteni pamoja na Waheshimiwa wote.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana, Waheshimiwa maswali.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Spika, kwa kuwa wanaume na sisi tumetakiwa kupiga kura nimesema na mimi ni haki yangu pia kuuliza swali.

Mhe. Spika, mimi nilitaka kujua tu kuwa Mhe. Mwenyekiti kwa matokeo mbali mbali ambayo yanakuwa yakijitokeza katika Baraza letu inaonekana kwamba mara nyingi haki za wanaume bado hatujaona zikijiridhisha sana katika utetezi wao katika Jumuiya hii ya Umoja wa Wanawake na badala yake wanajikita zaidi katika kuzungumzia zaidi ya wanawake lakini wakisahau kama na wanaume hawaendi bila ya wanawake. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Dr. Saada Mkuya Salum:** Nakushuru sana Mhe. Spika, lengo la Umoja wa Wanawake wa Wawakilishi Zanzibar labda chimbuko la kuundwa kwake kwanza kulikuwa tunaonekana kama mifumo yetu hii hususan katika mabaraza yetu ya kutunga sheria yamekuwa ni *malel dominated* kwa hivyo, hilo lipo na linaokana.

Kwa hivyo, chimbuko lake ni kuhakikisha kwamba sauti za wanawake zinasikika. Sasa *opinion* ya Mheshimiwa yeye inawezekana kabisa haku-*balance* vizuri lakini leo mimi nilikuwa nauliza suala la uvuvi Mheshimiwa nilikuwa nimesimama mara nyingi pale lakini kwa sababu Mheshimiwa aliona kama ni mwanamke anaweza kuwa asiwe mvuvi lakini inaonekana kuna hiyo *notion.* Lakini sisi vile vile katika *strategic plan* ya UWAWAZA tuna maeneo ambayo tuta-*encourage* vile vile wanaume washiriki na ndio maana kikanuni hizi nafasi zikaletwa katika Baraza ili zipigiwe kura kuona kwamba kunakuwa kuna ushiriki wa wanaume vile vile katika sheria zetu ambazo tutaleta pamoja na mipango ya maendeleo hapa.

Kwa hivyo, namumba Mhe. Shamata Shaame Khamis na Waheshimiwa Wajumbe wanaume wasiwe na wasi wasi mimi niko imara na nitahakikisha kwamba maeneo yote tuna-*cover* sawa sawa, hata maeneo ya ujenzi na maeneo ya uvuvi na kadhalika. Ahsante Mhe. Spika, nashukuru sana.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mhe. Spika, mimi nitaomba nimuulize maswali mawili Mheshimiwa Mwenyekiti.

**Mhe. Spika:** Tufanye moja tu Mhe. Mjumbe, swali moja tu uliza.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mhe. Spika, tumeona kwamba wanawake au Waheshimiwa Wanawake kila kitu wanataka wao wawe juu dunia hii kwamba sisi wanaume ndio kila kitu, sisi wanaume hata kwenye dini ndio tunatakiwa tuwe viongozi. Sasa kupitia wewe Mhe. Mwenyekiti, utafanyaje kuwawaweka wanawake kwenye nidhamu ya kufuata lile lile suala la dini mnataka kuja juu kila kitu kwanini?

**Mhe. Dr. Saada Mkuya Salum:** Ahsante namshukuru Mheshimiwa kwa swali lake. Tumeingia sana katika *content* ya dini lakini Mhe. Spika, uki-*analyze* vizuri Mwenyezi Mungu ameonesha uongozi wa mwanamme juu ya mwanamke sawa. Lakini kuna umuhimu mkubwa wa mwanamke katika uongozi vile vile tukienda katika dini yetu ya kiislamu kwa mfano Bibi Aisha mke wa Mtume (SAW) ame-*play very big roll* kuhakikisha dini yetu vile vile na mchango wake mwanamke na elimu iliyokuwepo leo imechangiwa kikubwa na uhifadhi mkubwa ambao aliokuwa nao mwanamke hata dini yetu hii imesimama leo tukawa tunayo sisi imetolewa na mchango vile vile mkubwa wa wanawake.

Kwa hivyo, kwenye suala la uongozi tunachokitaka haki pamoja na taratibu ziwe zinatizama maswala ya kijinsia katika maeneo yetu. Hatuwezi hapa leo tukaleta sheria ambayo haina hata kidogo mwanamke mchango wake kule, tumeona tu karibuni kuna Bodi za Wakurugenzi kwa mfano ziumeundwa Waheshimiwa mawaziri lakini utaona Wajumbe wote wanaume hivi hakuna *content* ya mwanamke katika masuala hayo.

Kwa hiyo, hilo ndio tunalotaka kusimamia tukisimama hapa hatusemi kwamba sisi tunataka kila kitu, tunataka usawa wa kijinsia na mazingatio ya kijinsia katika sera zetu pamoja na sheria zetu. Nakushukuru Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante kuna suali jengine kwa Mhe. Suleiman Haroub Suleiman.

**Mhe. Suleiman Haroub Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa mgombea lakini pia nilikuwa na suala dogo sana naomba nimuulize. Kama nyie UWAWAZA na wewe ndie Mwenyekiti wa UWAWAZA sisi akina baba tutafaidika vipi na UWAWAZA.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Ahsante sana Mhe. Spika, kuna muda Mheshimiwa mmoja alitania kama masihara tu alisema na yeye atataka kuhakikisha kunakuwa kuna chama cha mababa kinaitwa UBABAZA lakini naomba nimuhakikishie Mhe. Suleiman, niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi wa jinsia ya kiume kwamba wasiwe na wasiwasi sisi letu ni kusimamia usawa wa kijinsia na bahati nzuri bahati nzuri hata mimi *personal sprit* yangu ni kuona kwamba hata zile semina ambazo tutakuwa tunazipata pamoja na mafunzo, tuwashirikishe pamoja na wanaume kwa sababu kama sisi tutakuwa tunasimama tunagombea tu haki za wanawake lakini wanaume ambao ndio wamo katika mifumo hawaelewi umuhimu wa mwananmke itakuwa ni kazi moja ngumu sana. Kwa hivyo, Mtafaidika hili ni jambo letu sote na tunaomba tushirikiane katika utekelezaji wake.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Saada Mkuya Salum nakushukuru sana unaweza ukarudi ukakaa na hayo majibu yako ni ushahidi tosha kwamba UWAWAZA walifanya kazi kwenye kura za maoni na wamepata mwenyekiti sahihi kabisa sasa kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa UWAWAZA naomba nimkaribishe Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis ili aje ajieleze.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuja kujieleza mbele ya Baraza lako tukufu kwa nafasi ……….

**Mhe. Spika:**Waheshimiwa naomba utulivu kidogo tumsikilize Mheshimiwa endelea Mhe. Mwantatu.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis**: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuja kujieleza mbele ya Baraza lako tukufu kuja kujieleza mbele ya Baraza lako tukufu kwa nafasi ambayo niliyoiomba ya Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake ndani ya Baraza la Wawakilishi. Jina langu Mwantatu Mbarak Khamis, nimegombea nafasi hii ili niweze kuongoza na kusimamia maendeleo ya wanawake na wanaume ndani ya Baraza la Wawakilishi. Mhe Spika, kwa heshima na taadhima naomba kura yako pamoja na wajumbe wa Baraza lako tukufu wote wanipe kura ya ndio ili niweze kushirikiana nao katika kuendeleza maendeleo yetu ahsante.

**Mhe Hassan Khamis Hafidh:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kuniona namshukuru sana Mheshimiwa alaegombea umakamu wa UWAWAZA. Ni matumaini yangu Mheshimiwa kabla hajagombea nafasi hii amefanya utafiti na kujua changamoto zinazowakabili wanawake wenziwe. sasa nataka kujua changamoto gani zinazowakabili wanawake wenziwe na atafanya vipi kuzitatua changamoto hizo kuwa fursa.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hassan kwa swali lake dogo ambalo ameniuliza. Nimegombea kwa kuwa na mimi ni mwanamke nazielewa changamoto tosha zinazowakabili wanawake ndani ya Baraza lakini hata nje Baraza kwa hivyo, kwa upande wa ndani ya Baraza UWAWAZA kuna program nyingi za kuwawezesha wanawake changamoto kubwa kupata kujengewa uwezo. Kwa hivyo, tumejipanga tutawajengea uwezo wanawake ndani ya Baraza la Wawakilishi waweze kusimama kutetea haki za wanawake na wanaume lakini pia kuweza kusimamia program ambazo zinakuja ndani ya Baraza la Wawakilishi ikiwemo miswada ya kisheria tutangalia imezingatia vipi masuala ya jinsia. Vile vile kuwajengea uwezo wajumbe wanawake wanapokuwa ndani ya kamati wanapopitia taarifa waweze kuangalia masuala ya jinsia kama yamezingatiwa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya kijamii.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mhe. Spika, wewe Mhe. Spika, mwanamme, Naibu Spika mwanamke, Mwenyekiti tumechagua leo mwanamke na mwanamme Mawaziri wanawake wapo na wanaume wapo, swali langu hivi vitengo vilivyowaletea huu UWAWAZA lengo lao nini? Lakini cha pili hamuna lengo la kuwapindua wanaume nyinyi.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Mhe. Spika, naomba arejee lile la mwisho sijalilisikia vizuri.

**Mhe. Spika:** naomba urejee suala lako la mwisho

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Ninichosema Mhe. Spika, kama *fairness* tayari ishaonesha kwa Mhe. Rais kashateua wanamama wengi nimetoa mfano kwako Mhe. Spika, wewe Mwanamme Naibu Spika, mwanamke Mwenyekiti Mwanamme Mwenyekiti Mwanamke tuna wajumbe mawaziri wanawake na wakiume bado wanashadidia wanataka kuwa juu zaidi ninachouliza aloanzisha huu UWAWAZA lengo lao nini na si mashetani hawa wanataka kutupindua wanaume.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Spika nakushkuru naomba kumjibu Mhe. Mjumbe ni kwamba kuanzishwa kwa UWAWAZA kumekuja kutokana na kuonekena kwamba wanawake wengi wanakuwa wako nyuma na wanaume wanakuwa wanatuzidi katika mambo mbali mbali kwa hivyo, UWAWAZA utaweza kusaidia kuwajengea Wajumbe wanawake kujiamini zaidi na kuweza kushindana na wajumbe wanawake ndani ya Baraza la Wawakilishi ili ule uwezo uwe sawa kwa hivyo, zaidi UWAWAZA imekuja kuleta usawa ndani ya Baraza la Wawakilishi.

**Mhe. Spika:** Ahsante, Mhe. Mwanatatu naomba ukakae naomba sasa nimkaribishe Mhe. Anna Athanas Paul kwa nafasi ya Katibu wa UWAWAZA aje ajieleze.

**Mhe. Anna Athanas Paul:** Ahsante Mhe. Spika, kwa nafasi hii ahsante waheshimiwa wote mliopo mbele hapa mimi niliyesimama mbele yenu naita Anna Athanas Paul nimegombea nafasi ya Katibu katika UWAWAZA nimekuja mbele yenu kwa heshima nyingi kuomba kura zenu mnichangue niweze kuwa Katibu wa Jumuiya ya UWAWAZA.

**Mhe. Spika:** Ahsante Waheshimiwa maswali, maswali maswali lipo moja kutoka kwa Mhe. Nadir.

**Mhe**. **Nadir Abdullatif Yussuf:** Mhe. Spika, mimi nimpongeze Mhe. Anna namuamini sana kamanda lakini hebu atuambie akiwa yeye Katibu ndio mtendaji wa UWAWAZA amejipanga vipi katika suala lao la wanawake anataka kujipanga vipi na kutukandamiza sisi wanaume atuambie.

**Mhe. Spika:** Mhe. Nadir, lengo si kukandamiza wanaume nafikiri unaiweka vibaya sana halafu Mhe. Anna zungumza chochote anataka kusikia sauti yako.

**Mhe. Anna Athanas Paul:**Ameuliza wanaume tunataka kuwafanya nini……
Mhe. Spika: kuwakandamiza, vipaumbele vyako.

**Mhe. Anna Athanas Paul:** Sisi ni kuwajengea uwezo wanawake ndio lengo la UWAWAZA ile *capacity building* kwa ajili ya wanawake wawakilishi kwa sababu kwa kipindi kirefu tunaonekena Baraza linaongozwa zaidi na wanaume sasa tunatamani pia kumuona Spika mwanamke katika Baraza. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsate Mhe. Anna, waheshimiwa tunaomba utulivu, naomba waheshimiwa. tusikilizane kidogo. Nadhani hakuna tatizo ni kweli tokea tumeanzisha hili Baraza maspika tumekuwa wanaume ikitokea fursa ya Spika mwanamke nafkiri hiyo itakuwa ni nzuri tu Mheshimiwa hiyo haina tatizo. Haya nadhani maswali yamekwisha upande wako Mheshimiwa naomba sasa nimkaribishe Mhe. Panya Ali Abdalla yeye ni kwa nafasi ya Mtunza Hazina wa UWAWAZA.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuweza kufika hapa lakini kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima tukaweza kukutana katika Baraza hili tukufu, lakini pia kupitia kikao chako hichi kitukufu basi tunaombea kheri wezetu waliopata mitihani ya maradhi Mwenyezi Mungu awaponyeshe ili na wao waweze kushiriki kwenye shughuli mbali mbali lakini waliofika mbele ya haki Mwenyezi Mungu awarehemu kwa rehema njema.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nimesimama hapa kwa kuomba ridhaa ya wajumbe wote wa Baraza kupitia nafasi ya muweka hazina wa UWAWAZA baada ya kusema hayo nashukuru ahsante.

**Mhe. Spika:** Maswali Waheshimiwa, lipo swali moja Mhe. Suleiman Makame Ali.

**Mhe. Suleiman Makame Ali**: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nimulize swali dogo Mtunza fedha wa UWAWAZA Mhe. Spika, katika maelezo yao wote wamesema wanataka kuwajengea uwezo UWAWAZA na UBABAZA na tumeona mara ile ilikuwa wakitualika kwenye mikutano mbali mbali lakini jumuiya hii mara nyingi inategemea ufadhili kutoka kwa wahisani je, mara hii mtajipamgaje kuhakikisha kwamba wale wahisani watakapozuia mifuko yao nyinyi wenyewe mnasimamaje kwa miguu yenu kuhakikisha kwamba jumuiya yenu inaendelea.

**Mhe. Panya Ali Abdulla:** Ahsante sana Mhe. Spika lengo la UWAWAZA ni kuwasaidia wanawake na wanawake ambapo ukimsaidia mama maana yake umesaidia jamii nzima, lakini hata tukiangalia hizo programu zinazoletwa ziko programu zinasema *he for she*. Kwa hivyo, hizo zitaweza kusaidia wanaume na kama alivyosema mwenyekiti wetu kwa sababu tunakuwa tanawalika wanaume kupitia program zetu hizo ili na wao waweze kunufaika na yale mafunzo ambayo sisi tunayapata.

**Mhe. Spika:** Ahsante nashukuru Mhe. Panya Ali Abdalla unaweza kwenda kukaa. Waheshimiwa sasa naomba kuwaita wafuatao kwa nafasi Wajumbe wa Kamati Tendaji ya UWAWAZA naanza Mhe. Bahati Khamis Kombo ambae atafuatiwa na Mhe. Mwanajuma Kassim Makame.

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naitwa Bahati Khamis Kombo nimesimama mbele yenu kuomba ridhaa ya kura zenu kwa ajili ya kushirikiana na wenzangu katika kamati tendaji. Mhe. Spika, pamoja na wajumbe wenzangu wote naomba kura zenu zote za ndio.

**Mhe. Spika:** Maswali, Ahsante Mhe. Bahati unaweza kwenda kupumzika naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwanajuma Kassim Makame ambae atafuatiwa na Mhe. Rukia Omar Ramadhan.

**Mhe. Mwanajuma Kassim Makame:** Ahsante sana Mhe. Spika, mimi naitwa mwanajuma Kassim Makame ni mwakilishi viti maalum kutoka Mkoa Kaskazini Unguja nimesimama hapa kwa niaba ya lengo moja tu kwa wajumbe wote mliopo hapa mbele yangu pamoja na Mhe. Spika, naomba kura zenu zote au ridhaa zote mnipe mimi Mwanajuma Kassim Makame.

**Mhe. Spika:** Maswali waheshimiwa, Ahsante Mhe. Mwanajuma unaweza kwenda kupumzika naomba sasa nimkaribishe Mhe. Rukia Omar Ramadhan ajieleze.

**Mhe. Rukia Omar Ramadhan:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuweza kukutana katika Baraza letu tukufu Mhe. Spika Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi niliyesimama mbele yenu naitwa Rukia Omar Ramadhan ni mwakilishi wa wananchi wa jimbo la Amani naomba kura zenu za ndio ili niwe Mjumbe wa Kamati Tendaji ya UWAWAZA.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mheshimiwa, maswali, Ahsante sana Mhe. Rukia ramadhan naomba sana nimwite Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma.

**Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma:** Ahsante Mhe. Spika, kwa nafasi hii kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuipata nafasi hii adhimu ya kuweza kusimama mbele ya ukumbi huu kuja kuomba kura.Mhe. Spika, mimi Salha Mohammed Mwinjuma ni Mwakilishi ninaewakilisha vijana kutokea Kusini Unguja na nimesimama hapa kuja kuomba ridhaa na mimi niwe miongoni mwa wajumbe wa Kamati Tendaji ya UWAWAZA kwa heshima zote kabisa naomba kura zenu za ndio waheshimiwa ili niweze kuwa miongoni mwa wajumbe hao kwenda kuwawakilisha wenzetu nakushukuru.

**Mhe. Spika**: Maswali, Ahsante sana Mhe. Salha. Katibu kuhusu utaratibu sasa wa ugawaji wa kura.

**Katibu:** Mhe. Spika, pia naomba tena ruhusa yako nifanye zoezi la kuwahesabu pamoja na kuzigawa kwa sababu pia naona kuna *movement* zinaendelea kwa hivyo, tujiridhishe katika idadi yao halafu tutaendelea kugawa kura.

**Mhe. Spika:** *Inshaallah* tunaomba uwahesabu na tunawapigia kwa utaratibu gani katibu elezea namna ya kuwapigia kura tunawapigia kwa mmoja mmoja au tunawapigia wote.

**Katibu:** Mhe. Spika, tutawapigia mmoja baada ya mwengine tutaanza na mwenyekiti na wanaofuata tunapiga kura ya mwenyekiti tutazikusanya halafu tutakuja ya Makamu halafu tunakusanya na wengine kama itakavyokuwa isipokuwa kwa wajumbe wa nafasi ya Kamati Tendaji wao tutawapigia kwa pamoja kwa sababu wapo wanne.

**Mhe. Spika:** Ahsante, hesabu mpe Katibu.

**Katibu:** Mhe. Spika, idadi ambayo tumeipata hivi sasa ni wajumbe 70 ukiwemo na wewe tunaomba tuzigawe kura zetu.

**Mhe. Spika:** zoezi la kugawa kura lianze na kura inayogaiwa ni kura ya Mwenyekiti kwa sasa hivi.

*(Hapa Waheshimiwa Wajumbe waligaiwa karatasi za kura)*

**Mhe. Spika:** Kura zianze kukusanywa kwa wale ambao washapiga.

Waheshimiwa Wajumbe, wakati tunaendelea na hili zoezi la kupiga kura kuna baadhi ya matokeo ambayo yapo tayari, lakini kwa umuhimu wake inabidi tuyatangaze kabisa kwanza sasa hivi, halafu tuendelee na upigaji kura na hayo ni yale matokeo kwa nafasi ya Waheshimiwa Wajumbe wanaokwenda kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Kwa hivyo, namuomba Katibu ili atupe matokeo na tuweze kuyaridhia, kwa sababu wajumbe hao watahitajika sasa kuanza safari ya kuelekea Dodoma. Kwa hivyo, lazima tuyatowe kabisa sasa hivi matangazo. Katibu.

## MATOKEO YA UCHAGUZI WA WABUNGE WATANO

**Katibu:** Mhe. Spika, naomba nitangaze matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge Watano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, uliofanyika tarehe 10 Februari 2021.

Mhe. Spika, wajumbe waliopiga kura kati ya wajumbe wote waliohudhuria ni 72. Kura halali ni 72, kura zilizoharibika ni hapana na matokeo ya kura hizo ni:

Mhe. Ameir Abdalla Ameir ni kura 72. *(Makofi)*
Mhe. Bakar Hamad Bakar kura 72 *(Makofi)*

Mhe. Bahati Khamis Kombo kura 72 *(Makofi)*
Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis kura 72 *(Makofi)* na
Mhe. Suleiman Haroub Suleiman kura 72 *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hivyo Mhe. Ameir Abdalla Ameir, Mhe. Bakar Hamad Bakar, Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis na Mhe. Suleiman Haroub Suleiman wamechaguliwa kuwa wabunge watano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2020/2025. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha kwako na Baraza lako Tukufu*(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante Katibu. Waheshimiwa Wajumbe, kama mlivyosikia matokeo kwamba sasa tumepata wawakilishi wetu watano ambao wataliwakilisha Baraza la Wawakilishi kwenye Bunge la Jamhuri. Nami kwa nafasi yangu naomba niwatambuwe, ambao ni:

Mhe. Ameir Abdalla Ameir
Mhe. Bakar Hamad Bakar
Mhe. Bahati Khamis Kombo
Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
Mhe. Suleiman Haroub Suleiman *(Makofi)*

Mimi nichukuwe nafasi hii kuwapongeza, lakini sasa pia ninawaruhusu waanze safari ya kuelekea Dodoma kwa ajili ya kuweza kufanikisha kiapo cha uaminifu. Ahsanteni sana tunaendelea.

## MATOKEO YA WENYEVITI WA BARAZA

**Katibu:** Matokeo ya Waheshimiwa Wenyeviti pia tayari, kama utaniruhusu.

**Mhe. Spika:** Hawa wengine nadhani tungemaliza kuwapigia kura, halafu tutayatangaza hayo mengine.

**Katibu:** Sawa Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Katibu.

## UCHAGUZI WA MAKAMU MWENYEKITI WA UWAWAZA

**Katibu:** Mhe. Spika, Mwenyekiti tayari tumeshampigia. Sasa hivi Makamu Mwenyekiti wa UWAWAZA kumpigia kura.

Mhe. Spika, tunaomba ruhusa ya kuyatoa masanduku ya nafasi ya Mwenyekiti wa UWAWAZA pamoja na kuhesabu tena kura, bado ingia toka ya wajumbe inaendelea. Kwa hivyo, tujiridhishe tena kwenye idadi yao katika nafasi hii ya Makamu Mwenyekiti wa UWAWAZA. Naomba tufanye hesabu.

**Mhe. Spika:** Ahsante, naomba wajumbe wahesabiwe.

**Katibu:** "Karima mwite mhudumu mmoja aje kuhesabu", upo.

**Mhudumu:** Nipo.

**Katibu:** Haya, sawa endelea.

Mhe. Spika, wajumbe ambao wapo hivi sasa kwa ajili ya kupiga kura nafasi ya Makamu Mwenyekiti ni 61 ukiwemo wewe mwenyewe. Tunaomba ruhusa ya kugawa kura hizo pamoja na kuzikusanya itakapokamilika.
**Mhe. Spika:** Ahsante, endelea. Kura zigaiwe.

Wahudumu naomba kura zikusanywe kwa wale ambao washapiga.

Naam, Katibu nafikiri tunaweza tukaendelea.

**Katibu:** Mhe. Spika, tunaomba tuondoke na masanduku ya kura. Tuendelee na nafasi ya Katibu wa UWAWAZA kwa kumpigia kura.

**Mhe. Spika:** Ahsante, masanduku yaondolewe na tuanze utaratibu pia wa kugawa kura. Idadi nikidhani kuwa itakuwa imebaki ile ile, haijazidi wala kupungua.

**UCHAGUZI WA KATIBU WA UWAWAZA**

**Katibu:** Mhe. Spika, wajumbe waliopo kwa ajili ya kumpigia kura Katibu wa UWAWAZA ni 59, tunaomba tuzigawe kura hizo pamoja na kuzikusanya.

**Mhe. Spika:** Ahsante, zoezi la kugawa kura liendelee.

Wahudumu, kura zianze kukusanywa kwa wale ambao tayari wameshapiga.

Katibu kura inayofuata.

**UCHAGUZI WA MTUNZA HAZINA WA UWAWAZA**

**Katibu:** Mhe. Spika, nafasi inayofuata ni nafasi ya Mtunza Hazina wa UWAWAZA. Wahudumu wangu wanaendelea kuzikusanya, naomba kidogo dakika chache wamalizie ili wagawe kura za Mtunza Hazina kwa ajili ya kupigiwa kura.

**Mhe. Spika:** Tunaomba sasa muwakabidhi wahudumu kura waanze kugawa za Mtunza Hazina.

Katibu, endelea.

**Katibu:** Mhe. Spika, wajumbe waliopo sasa hivi kwa ajili ya kumpigia kura Mtunza Hazina ni 61 ukiwemo na wewe Mhe. Spika. Tunaomba tuzigawe.

**Mhe. Spika:** Kura za kumpigia Mtunza Hazina zigaiwe, wakati hizi zilizopigwa za Katibu wa UWAWAZA zikiondolewa.

Kura zianze kukusanywa kwa wale ambao tayari wameshapiga.

**Katibu:** Siti, anzeni kukusanya kura.

**Mhe. Spika:** Anzeni kukusanya kura.

**Mhe. Spika:** Naomba tuharakishe kidogo.
**Katibu:** Mheshimiwa naomba tuondoke na masanduku hayo pamoja na kuendelea na nafasi ya Wajumbe wa Kamati tendaji ya UWAWAZA kwa kumalizia na idadi yetu ni 62, ndio ?
Ilikuwa 61 ameongezeka mmoja sasa hivi ni 62 pamoja na wewe Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante masanduku yatolewe, naomba sasa kura zigaiwe, kura zikusanywe kwa waliokamilisha. Katibu kura zinaweza kwenda kuhesabiwa.

**Katibu:** Mheshimiwa naomba tuondoke na masanduku ya kura ili tuweza kuendelea na zoezi la kuhesabu kwa waliobakia.

**Mhe. Spika:** Ahsante, Waheshimiwa wakati tunasubiri matokeo naomba niwasomee matangazo mawili ambayo yamenifikia.

Kwanza kabisa naomba niwatangazie wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kikao na Kamati ya Bajeti mara baada ya kuakhirishwa shughuli zetu leo, kikao kitakuwa ukumbi mkubwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum ndie aliyeleta hili tangazo.

Pili, ni kukukumbusheni Waheshimiwa jana kwenye *Briefing* tulisahau kukupeni taarifa iliyohusu mchango wa Watoto Mayatima wenye Virusi vya UKIMWI kulikuwa kuna mchango ambao ulikuwa unaombwa kutoka kwa kila Mjumbe shilingi 100,000 kwa ajili ya kuwachangia wale watoto kwa sababu hapo wanapoishi hivi sasa hivi wanatakiwa ndani ya mwezi huu wahame sasa lile eneo lao jipya ambalo wanafanyiwa maarifa linajengwa ndiko wanakotakiwa kwenda kuhamishiwa. Sasa michango yetu hii itasaidia katika kuharakisha hilo zoezi kwa hiyo, tunatakiwa kila Mjumbe tuchangie shilingi 100,000 kwa ajili ya kufanikisha shughuli hiyo.

Baada ya matangazo hayo sasa nasubiri matokeo kutoka kwa Katibu.

**Katibu:** Mhe. Spika, matokeo ambayo yapo tayari kwa hivi sasa ni matokeo ya Wenyeviti wa Baraza, Mwenyekiti wa UWAWAZA pamoja na Makamu Mwenyekiti wa UWAWAZA kama utaniruhusu nitaweza kuweza kuendelea huku tukiwa…

**Mhe. Spika:** nadhani unaweza kuendelea kuyatangaza hayo ambayo tayari ushayapata.

## MATOKEO YA UCHAGUZI WA WENYEVITI

**Katibu:** Mhe. Spika, matokeo ya uchaguzi wa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar uliofanyika tarehe 10/ 02/2021 ni kwamba Wajumbe waliopiga kura kati ya Wajumbe wote waliohudhuria ni 71 kura halali ni 71, kura zilizoharibika hapana. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma amepata kura 67 na Mhe. Shaaban Ali Othman amepta kura 69. Kwa hivyo, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Shaaban Ali Othman wamechaguliwa kuwa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2020/2025.

Mhe.Spika, niendelee.

**Mhe. Spika:** Ahsante, Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wetu wapya ambao bila shaka watakuwa katika shughuli za kuendesha kiti hapa. Shughuli zetu za Baraza la Wawakilishi mimi niwatakie kila la kheri na mafanikio mema. Lakini nilikuwa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tuwape ushirikiano mkubwa kama ambavyo mnanipa mimi Spika ili kuweza kufanikisha kuendesha shughuli zetu kwa uweledi zaidi na kikubwa zaidi ni kwamba tunaongozwa na kanuni na bila shaka hatuna mashaka nao katika shughuli za kanuni na tutamsaidia pia Mhe. Shaaban Ali Othman na tuna matumaini makubwa kwamba atafanya vizuri sana hii shughuli kwa sababu ya mashirikiano ambayo tutakuwa tunampa. Baada ya matangazo hayo, sasa nimpe tena Katibu kwa nafasi yengine.

**Katibu:** Mhe. Spika, uchaguzi uliyokuwa unaendelea ni wa jumuiya ya UWAWAZA na kwa bahati nzuri matokeo yao yote kwa nafasi ambazo wamegombea yameshapatikana naomba niendelee kutaja matokeo hayo kwa kila nafasi.

Mhe. Spika, matokeo ya uchaguzi wa UWAWAZA uliofanyika tarehe 10/02/2021 ni kwamba wajumbe wote waliohudhuria wakati wa kupiga kura ni 70, Wajumbe waliopiga kura kati ya Wajumbe wote waliohudhuria 70, kura zilizomkubali Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum ni 70, kura zilizomkataa hapana na kura zilizoharibika hapana. Hivyo, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa UWAWAZA kwa kipindi cha mwaka 2020/2025, ahsante Mheshimiwa.

Matokeo mengine ni ya uchaguzi wa Mwakamu Mwenyekiti wa UWAWAZA uliofanyika tarehe 10/02/2021, wajumbe wote waliohudhuria wakati wa kupiga kura ni 60, Wajumbe waliopiga kura kati ya wajumbe wote walihudhuria 60, kura zilizomkubali Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis ni 60 na kura zilizomkataa na zilizoharibika hapana. Hivyo, Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis amechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa jumuiya ya UWAWAZA kwa kipindi cha mwaka 2020/2025.

Mhe. Spika, matokeo ya uchaguzi wa Katibu wa UWAWAZA uliyofanyika leo 10 Februari, 2021 ni kwamba Wajumbe wote waliohudhuria kupiga kura ni 61, waliopiga kura kati ya Wajumbe wote ni 61, kura zilizomkubali Mhe. Anna Athanas Paul ni 61, kura zilizomkataa na zilizoharibika hapana. Hivyo, Mhe. Anna Athanas Paul amechaguliwa kuwa Katibu wa UWAWAZA kwa kipindi cha mwaka 2020/2025.

Matokeo mengine ni ya uchaguzi wa mtunza hazina wa UWAWAZA uliyofanyika leo tarehe 10/02/2021, kwamba wajumbe wote waliohudhuria wakati wa kupiga kura ni Wajumbe 60 na waliopiga kura katika Wajumbe hao pia ni 60, kura zilizomkubali Mhe. Panya Ali Abdalla ni 60,

zilizomkataa na kuharibika hapana. Kwa hivyo, Mhe. Spika, napenda kulitaarifu Baraza lako kuwa Mhe. Panya Ali Abdalla amechaguliwa kuwa Mtunza Hazina wa UWAWAZA kwa kipindi cha mwaka 2020/2025.

Mwisho, matokeo ya uchaguzi wa Wajumbe wa Kamati tendaji ya UWAWAZA uliyofanyika tarehe 10/02/2021, Wajumbe waliopiga kura kati ya Wajumbe wote ni 60, waliohudhuria ni 60, kura halali ni 60, kura zilizoharibika hapana. Mhe. Bahati Khamis Kombo ni 59, Mhe. Mwanajuma Kassim Makame ni 60, Mhe. Rukia Omar Ramadhanni 60 na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma 60. Hivyo, napenda kutaarifu kwamba Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mhe. Mwanajuma Kassim Makame, Mhe. Rukia Omar Ramadhan na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma wamechaguliwa kuwa wajumbe wa kamati ya tendaji ya UWAWAZA kwa kipindi cha mwaka 2020/2025. Ahsante Mhe. Spika, napenda kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Katibu, Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukue nafasi hii sasa kuipongeza timu nzima hii ya UWAWAZA ambayo tumeipigia kura kuiridhia hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi, nikianza na Mhe. Mwenyekiti wa UWAWAZA Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum. Pia nichukue nafasi hii pia kumpongeza kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, nimpongeze pia Mhe. Anna Athanas Paul kwa nafasi ya Katibu wa UWAWAZA, nimpongeze Mhe. Panya Ali Abdalla kwa nafasi ya Mtunza Hazina wa UWAWAZA bila ya kuwasahau Wajumbe wanne kwa nafasi ya Kamati Tendaji ya UWAWAZA ni Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mhe. Mwanajuma Kassim Makame, Mhe. Rukia Omar Ramadhan na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma.*(Makofi)*

Waheshimiwa hongereni sana, kama kawaida jumuiya hii inakuwa na mashirikiano ya karibu sana na Wajumbe wanaume ndani ya Baraza. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba mashirikiano hayo yaendelee kwa sababu ndio na ridhaa yetu safari hii imepita. Baada ya matangazo hayo ya pongezi sasa nirudi kwa katibu kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Ripoti ya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2019/2020

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Spika, katika jitahada za kuimarisha Utawala bora katika nchi yetu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa ada za kuimarisha utawala bora katika nchi yetu. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitunga na kupitia sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4, 2015. Sheria hii imeweka viwango vya maadili kwa viongozi wa umma ambavyo vinapaswa kuvizingatia wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kwa umma.

Aidha, sheria hii ndio ilioanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Tume ya Maadili, ambayo imepewa jukumu la kusimamia maadili ya viongozi wa umma. Mhe. Spika, Tume ya Maadili katika kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa sheria hiyo imepewa jukumu la kutoa elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili, kupokea, kusajili na kuhakiki tamko la mali na madeni kutoka kwa viongozi wa umma. Jukumu jengine ni kupokea

malalamiko na kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma mbali mbali za uvunjaji wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma.

Mhe. Spika, kama zilivyo taasisi nyengine za Utawala bora Zanzibar kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria, Tume ya Maadili ya viongozi wa umma inatakiwa kuandaa na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa kazi zake kila mwaka kupitia kifungu cha 29(1) cha sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Mwenyekiti wa Tume ya Maadili anatakiwa ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha husika kuandaa na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa kazi za Tume kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
Kadhalika, sheria imempa Mamlaka Mhe. Rais, kwa kumuelekeza Waziri anaehusika na maadili ambaye kwa sasa ni Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora kuiwasilisha ripoti hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, ripoti hii ya nne ya utekelezaji wa kazi za tume 2019/ 2020 tangu kuanzishwa kwake. Ripoti iliwasilishwa kwa aliekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, Mnamo Tarehe 25 Septemba, 2020, na alinielekeza kuiwasilisha katika Baraza la Wawakilishi wakati huo. Hata hivyo, ripoti hiyo haikuweza kuwasilishwa kwa wakati kwa sababu Baraza la Wawakilishi lilikuwa limeshavunjwa wakati huo. Hiki ndio kikao cha kwanza cha kazi za Baraza la Wawakilishi, hivyo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameniagiza kuiwasilisha katika Baraza lako tukufu. Kutokana na maelekezo hayo niliyoagizwa na Mhe. Rais ninaomba kuiwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi, Ripoti ya Utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili 2019/2020 ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako wapate fursa ya kuisoma na hatimae kutoa maoni na ushauri.

Mhe. Spika, ripoti hii inaeleza maeneo makuu matano ambayo eneo la kwanza linazungumzia maelezo ya Mwenyekiti, Utangulizi unaohusisha dira, dhamira, Maadili ya msingi na lengo kuu.

Pili, inazungumzia Muundo wa Tume ambalo linachambua Idara za Tume, Watumishi wa Tume, Majukumu ya Tume, Mamlaka na uwezo wa Tume.

Eneo la tatu linazungumzia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa 2019/ 2020.

Nne, linazungumzia utekelezaji halisi wa kazi za Tume na Maadili zilizopangwa 2019/2020. Miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na kupokea na kusajili tamko la mali na mdeni kutoka kwa viongozi wa umma. Shughuli hii inahusisha uchapishaji, usambazaji na uchambuzi wa fomu ya tamko la mali na madeni, kutangaza majina ya viongozi wa umma katika gazeti rasmi la serikali, Ufuatiliaji na Usimamiaji wa taarifa za viongozi wasiojaza na waliochelewa kuwasilisha fomu za tamko la mali na madeni.

Shughuli nyengine ni utayarishaji wa mfumo wa kielektroniki wa kusajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma. Uhakiki wa taarifa za mali na madeni kwa viongozi wa umma na kupokea na kufanya uchunguzi wa tuhuma na malalamiko ya ukiukwaji wa sheria za maadili kwa viongozi wa umma.

Mhe. Spika, katika kusimamia jukumu la kupokea na kufanya uchunguzi wa tuhuma za malalamiko ya ukiukwaji wa sheria za maadiili naomba kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:

Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Tume ya Maadili ilipokea na kushugulikia jumla ya malalamiko 20 dhidi ya viongozi wa umma. Malalamiko hayo yalihusu maeneo mbalimbali ikiwemo matumizi mabaya ya madaraka, malalamiko tisa, mgongano wa kimaslahi malalamiko matatu, rushwa na ubadhirifu wa mali za umma malalamiko matano, kashfa na matumizi ya lugha za matusi malalamiko mawili na upendeleo katika ajira lalamiko moja.

Mhe. Spika, katika kuyafanyia kazi malalamiko hayo 20, moja linahusiana na kesi ya madai na hilo lipo mahakamani, malalamiko kumi na tano yanaendelea kufanyiwa kazi na lalamiko moja limefutwa baada ya kubaini kuwa halina hoja ya msingi na malalamiko menginge matatu yanashugulikiwa. Malalamiko yaliyowasilishwa Tume ya Maadili, yamehusisha Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za SMZ, Wateule,Mawaziri na viongozi wa Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, shughuli nyengine zilizotekelezwa kwa mwaka 2019/ 2020 ni kujenga uwezo na uelewa kwa wananchi na viongozi wa umma kwa Unguja na Pemba kuhusu maadili ya viongozi wa umma. Maadhimisho ya siku ya maadili ni kuwapatia mafunzo ya kitaaluma watumishi wa Tume. Kukuza na kuimarisha ushirikiano na uhusiano kitaifa, kikanda, kimataifa na vikao vya tume.

Mhe. Spika, eneo la tano linahusiana na hali ya mapato na matumizi, vikwazo na utatuzi wake, mikakati ya Tume kwa mwaka 2020/2021, mapendekezo, hitimisho na uwasilishaji wa ripoti. Mhe. Spika, matarijio yangu ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe wamepata muda wa kutosha, uliowawezesha kuisoma na kuipitia ripoti hii na nina imani kubwa kuwa wapo tayari sasa kwa ajili ya kutoa maoni yao ambayo yataisaidia wizara yangu pamoja na Tume ya Maadili ya viongozi katika utekelezaji wa kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Naomba sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya kusimamia Viongozi Wakuu ili aje asome hotuba ya maoni. *(Makofi)*

**Mhe. Mtumwa Peya Yussuf (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kusoma hotuba ya maoni kuhusu ripoti ya nne ya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili 2019/ 2020.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uzima na afya njema ya kutuwezesha kufika hapa katika Mkutano huu wa pili wa Baraza la Kumi katika hali ya uzima na afya, amani na utulivu wa kuweza kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Mhe. Spika, pia nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa. Hali ambayo imeendelea kuipa nafasi serikali na wananchi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Napenda kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla tuendelee kudumisha ukamilifu amani na utulivu kwani bila ya hivyo hakuna maendeleo.

Mhe. Spika, aidha napenda kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar na kushinda kwa asilimia 76 katika uchaguzi uliofanyika tarehe 25 Oktoba ,2020.

Pia tunampongeza kwa mwanzo mzuri wa utekelezaji wa majukumu yake kwa kusimamia kwake Misingi ya Utawala wa Sheria na Utawala Bora. Hii ni nia njema ya kuwa na uwazi, uwajibikaji na utawala bora katika ripoti hii ambayo ina inaakisi matokeo ya kazi za msingi zinazofanywa na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kipindi kilichoanishwa katika ripoti hii.

Mhe. Spika, napenda pia kumpongea Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua Mhe. Hemed Salum Abdulla, kuwa Makamu wa Pili wa Rais, ambapo kwa muda mfupi tu baada ya kuteuliwa tayari amedhibitsha kuwa ni kiongozi mpenda haki na hodari katika kutekeleza majukumu yake na mwenye nia ya kuiletea nchi yetu maenedeleo.

Aidha, Kamati inampongeza Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Mhe. Haroun Ali Suleiman kwa kuteuliwa kushika nafasi kwa mara nyengine. Vile vile, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Uwasilishwaji wa Ripoti ya nne ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa Mwaka 2019/2020.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na kwa kuzingatia matakwa ya Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba kwa ruhusa yako niwataje wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | - | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Suleiman Makame Ali | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Salma Mussa Bilal | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Machano Othman Said | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zaina Abdulla Salum | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Salma Muhsin Haji | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Haji Jecha Salum | - | Katibu |
| 10. | Ndg. Amina A. Hemed | - | Msaidizi |

Mhe. Spika, vile vile nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa, viongozi na watendaji wote wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kazi zao nzuri na ngumu wanazozifanya

katika kusimamia haki na uadilifu wa viongozi wa umma hapa Zanzibar. Licha ya kuwa na changamoto mbali mbali zinazojitokeza na kukabiliana nazo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba kutoa Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Ripoti ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma wa Zanzibar mbele ya Baraza lako Tukufu kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Kamati imeipongeza sana juhudi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kuweza kuwasilisha Ripoti yao hii kwa mara ya nne mfululizo tokea kuanzishwa kwake na kuweza kuonesha mafanikio mbali mbali yaliofikiwa. Kwa mafanikio haya ni imani yangu kuwa yamepatikana kwa ujasiri na moyo wa kujitolea kwa watendaji na viongozi wote wanaounda tume hii.

Mhe. Spika, kwa ujumla, kamati yetu imeridhika na ripoti ya utekelezaji wa kazi ya Tume na Maadili kwa mwaka 20219/2020 kwa kuzingatia msingi wa kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa kipindi kilichotajwa hapo juu, ambapo kazi hizo zilitekelezwa kwa kuonesha ufanisi wa hali ya juu kabisa.

Mhe. Spika, kupitia ripoti hii Tume imeeleza mikakati mbali mbali ambayo inatelelezwa kwa lengo la kutoa elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa maadili. Kwa kutumia mikutano ya viongozi wa umma pamoja na kutumia mabaraza ya vijana, tume imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuifikia jamii katika kutoa elimu. Kamati inapongeza sana juhudi hizi kwa vile jamii nzima inafikiwa na kupata elimu juu ya kuwa na viongozi bora na utumishi wenye maadili mema jambo ambalo ndio msingi mkuu wa mafanikio katika jamii yenye kuhitaji utawala bora na maendeleo kwa ujumla.

Mhe. Spika, kuwepo kwa tovuti ya Tume ya Maadili, kumezidi kuimarisha upatikanaji wa utoaji wa taarifa mbali mbali ambazo zinahusiana na utendaji wa kazi za tume. Aidha, Kamati inaridhia mpango wa tume kuweka tovuti ambayo viongozi na wahusika wote wanaojaza fomu, wanaweza kujaza katika mtandao na hivyo kupunguza kutumia muda mrefu kujaza fomu hizo.

Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa, taarifa zinazowekwa katika mtandao huo ziwe katika hifadhi salama na zenye kuaminika ili kuepuka kutumiwa vibaya kwa taarifa hizo na wadukuzi.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, kamati ina ishauri serikali kuanzisha mfumo mpya wa *Data base* ambao unahifadhi taarifa zote za mali za viongozi wa umma kama vile; nyumba, ardhi, magari na kadhalika, kwa wanaopaswa kujaza fomu hizi na tamko la mali na madeni kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mali hizo kwa serikali. Lakini pia zinasaidia tume kukusanya taarifa za wateja wake kiuhakika na zenye ukamilifu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa kumi na tatu, unaonesha jedwali la uhakika kwa viongozi wa umma kwa Mwaka 2019/20 asilimia inaonesha kushuka hadi kufikia asilimia 61 tofauti na mwaka uliotangulia ambao walihakiki kwa asilimia 140. Hii inatokana na ugumu wa kuwafikia wahakikiwa kutokana na changamoto ya mripuko wa homa ya mafua *Corona*, ambapo Wizara ya Afya ilizuia mikusanyiko ya watu. Kamati pia inaipongeza sana Tume kwa juhudi

walizozichukua sambasamba na serikali kuongeza kasi yao kwa kuwaajiri watendaji wapya katika kipindi hichi, jambo lilioongeza kasi ya utendaji na ufanisi wa majukumu yao.

Mhe. Spika, kamati inahimiza kutatuliwa kwa vikwazo vinavyoikabili tume kwa vile kukosekana kwa taarifa za baadhi ya viongozi wanaoteuliwa, wanaobadilishwa nafasi za uongozi wanaostaafu na wanaohamishwa kutoka Taasisi moja kwenye nyengine ambapo kupelekea kukosekana kwa taarifa sahihi za viongozi hao. Aidha, Kamati inawataka viongozi ambao ni wazito kutoa taarifa za wenzao wakati wa ujazaji wa fomu za tamko za mali na madeni kwani kufanya hivyo ni kuenda kinyume na sheria.

Mhe. Spika, Tume inakabiliwa na tatizo kubwa hasa wakati wa kufanya uhakiki na uchambuzi wa mali na madeni na viongozi wa umma kwa mali nyingi kukosa kuhaulishwa hali inayopelekea kutopatikana kwa taarifa sahihi za mali hizo.

Mhe. Spika, Kamati inawahimiza viongozi wote wa umma na wale wadau wetu wanaojaza fomu hizi za tamko na mali za maadili kuhakikisha kwamba wanahaulisha mali zao katika njia halali za kisheria ili kuepusha kupatika taarifa zisizo sahihi. Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa inatoa pongezi zake za dhati kwa kazi nzuri ya Tume ya Maadili ya viongozi wa umma ya kuhakikisha inasimamia madili na viongozi na imepata mafanikio mengi, yenye kukamilisha dira na dhamira ya tume hii katika muda mfupi tokea kuanzishwa kwake. Hivyo, lengo kuu lililokusudiwa litafikiwa endapo misingi mikuu ya maadili itazingatiwa ambayo ni uadilifu, usiri, utaalamu, uwajibikaji na kufanya kazi kwa mashirikiano.

Mhe. Spika, Tume ya Maadili imejitahidi sana katika kurahisisha utendaji wa kazi zake unakuwa kwa kasi na kwa haraka ambapo inatarajia katika robo ya nne ya Mwaka wa Fedha kuanza rasmi uingizaji wa taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma kuwa ni kielektroniki, ki-*digitalize* kama inaiomba tume kuhakikisha kuwa lengo hilo linafikiwa.

Mhe. Spika, Kamati inapenda kutoa shukran na pongezi kwa wananchi kwa kutambua azma na mantiki ya kuanzishwa Tume ya Maadili. Vile vile kwa tume ya maadili kwa kuwapatia elimu wananchi wa Zanzibar inayowawezesha na kuwashajihisha kuongezeka idadi ya uwasilishwaji wa malalamiko yanayohusiana na ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma kama Jedwali Nam.4 inavyoonesha. Kamati inashauri, utaratibu wa utoaji wa elimu kwa wananchi na viongozi uwe endelevu na uhusishe rika na jinsia zote.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nilipokuwa nawasilisha hotuba hii na pia nizidi kuwashukuru wajumbe wa Kamati yetu kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia pamoja na kuwa na msimamo na umakini kwa wanachokisimamia.

Aidha, nawaomba Wajumbe wa Baraza hili tukufu waifahamu vyema ripoti hii ili waweze kutoa michango yao itakayoimarisha utekelezaji wa majukumu ya tume. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mtumwa Peya kwa niaba ya Mwenyekiti. Waheshimiwa Wajumbe hii ripoti inachangiwa, ingawa sijapata jina lolote la mtu ambae anahitaji kuchangia

lakini hata angekuwepo muda tulionao sasa hivi haumtoshi mchangiaji yoyote kuchangia, kwa sababu muda uliobaki ni mdogo sana kwa maana hiyo tutaendelea nayo mchana. Kwa maana ya baada ya laasiri saa kumi na moja.

Kwa hivyo, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa kwa ushirikiano ambao tumekua nao katika hichi kipindi cha awali, chaguzi tulizozifanya na niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wapya ambao wameapa. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii sasa kusitisha shughuli za Baraza mpaka saa kumi na moja barabara za jioni leo.

*(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

(*Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, nina jina moja tu hapa na nategemea mengine yatafuata kwa ajili ya kuchangia na naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yusuf:** *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Spika, naomba kuchangia kwa ufupi tu mambo machache kwenye Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ripoti ya nne ya mwaka 2019/2020. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kukipa chama changu Chama cha Mapinduzi imani ya kunichagua tena na kunileta tena ndani ya Baraza la Wawakilishi. Lakini vile vile niwashukuru wananchi wangu wote wa Jimbo la Chaani walionichagua kuweza kufika leo hapa kuwakilisha katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nitaizungumzia tume kwa uchache kabisa kwenye aya namba mbili katika maadili ya msingi wamesema kwamba uadilifu, kufanya kazi kwa uwazi bila ya upendeleo, kuhifadhi na kutunza taarifa zote za siri ikiwemo taarifa zinazohusiana na mali na madeni ya viongozi wa umma. Mhe. Spika, mimi nimpongeze Mwenyekiti wa Tume ya Maadili pamoja na watendaji wake wote kwa kufanya kazi vizuri sana na kufanya kazi kwa uweledi kama walivyosema kwenye kitabu hiki. Hadi hivi leo mimi na wenzangu waliokuwa wanaendelea miaka mingi humu ndani taarifa zetu zote tulizokuwa tukizipeleka katika chombo hichi hatujasikia hata Mwakilishi mmoja kwamba hata kama anamiliki baiskeli ama gari nje ya eneo lile.

Mhe. Spika, nimesema nichangie hii inaonesha dhahiri kitengo kile kina viongozi waliobobea lakini pia viongozi waliokuwa waaminifu sana katika kazi zao. Nimeamua kuwasifu kwa sababu hizi kazi zinaonesha kwa vitendo, hata unapokwenda kwenye ofisi yao maadili yao ni mazuri wana hekima na hata kama ulikosea kama kiongozi wanakufahamisha kwa njia ambayo wanahisi wao inafaa kistaarabu kufahamishika.

Mhe. Spika, kuna ukurasa namba tano kupokea tuhuma na taarifa za uvunjaji wa maadili kutoka kwa wananchi na vile vile kufanya uchunguzi juu ya madai hayo ya uvunjaji wa maadili kutoka kwa kiongozi yeyote wa umma. Mimi hapa ningependa nizungumze machache kwa sababu kama tunavyofahamu sisi wanasiasa hatutakiani mema huko nje na watu humtafutia sababu

mwanasiasa ili akosee au aende njia ambayo iliyokuwa sio apate matatizo huko anakokwenda kwenye suala lake la siasa.

Kwa wale ambao watakaokuwa wanapeleka taarifa ya kiongozi yeyote wa siasa inawezekana ikawa ya kupandikizwa, chuki au ya kutumwa. Sasa kwa wale ambao wanapeleka taarifa zile juu ya viongozi wa umma iwe sisi iwe mwengine yeyote ahakikishe yule anayepeleka taarifa wanamdhibiti vizuri awe na uhakika na alichokisema na pindipo taarifa zile alizopeleka ni za uwongo au alikusudiwa mtu kwa lengo fulani basi wale watu wafungwe na wachukuliwe hatua za kisheria. Kama nilivyosema kwamba namuamini sana Mwenyekiti wa Tume hii pamoja na watendaji wake kwa sababu pia nimefanya kazi kwenye kamati hii kwa muda wa miaka miwili na nusu nafahamu utendaji wao na namfahamu Mwenyekiti utendaji wake na kwa ujumla waliobakia.

Mhe. Spika, niende kwenye suala jengine ambalo la masula la ukiukaji wa maadili kwa viongozi wa umma. Tulio wengi hatufahamu kwa wingi kabisa kwamba jambo tukifanya tutakuwa tumevunja taratibu za uongozi wa umma. Ningemuomba Waziri Mhe. Haroun Ali Suleiman na nimpongeze kuteuliwa tena kuwa Waziri Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri, lakini tutengenezewe vitabu maalum japo vidogo venye kurasa kumi au tano ambavyo vitatueleza mambo yote ambayo viongozi wa umma utakapofanya jambo hili basi utakuwa umekiuka maadili na halitakiwi kiongozi kama wewe kulifanya kwa sababu vipo vitu tunavijua na vipo vitu hatuvijui. Mhe. Waziri tunaomba sana mtutayarishie kitabu chochote kiwe cha rahisi tu zisitumike pesa nyingi lakini kieleze kitabu kile vitu gani tukivifanya itakuwa tumekiuka maadili.

Mhe. Spika, suala la kuchelewa kujaza fomu. Ni kweli kuna baadhi ya viongozi inatokezea kuchelewa kujaza fomu kwa sababu maalum na sababu zenyewe wengine hatupati kwa muda au labda binaadamu yule aliyepelekewa zile risiti au zile fomu amesahau kumpatia Mjumbe au inawezekana zimewekwa sehemu Mjumbe kachelewa kuzipata. Sasa ningeomba sana Tume ya Maadili inavyotumia hekima zake kila siku basi iendelee kutumia hekima zile kwa sababu sifikirii kama kuna kiongozi ndani ya Baraza la Wawakilishi sizungumzii kwengine pengine wanafanya kwa makusudi, lakini ndani ya Baraza la Wawakilishi sifikirii kama atatokea kiongozi kufanya makusudi kwamba asiende kujaza fomu na asiende kuripoti kama ilivyotakiwa kwa mujibu wa sheria. Sasa vitu ambavyo vinatufanya muda mwengine tuchelewe ni kwamba mtu alisafiri nje ya nchi, kuna vitu vinajitokeza alichelewa kuipata na mazingira tofauti.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo linaleta utata kwenye fomu hizi, ni jambo la familia yetu tukiacha sisi wenyewe Waheshimiwa Wawakilishi. Humu ndani tuna Wawakilishi wa kike na wa kiume. Tusitegemee kama wake zetu watakubali tuwajazie vitu vyao kwenye fomu hizi, huko nyumbani zinaruka ngumi wanasema unataka uijue mali yangu ujaze fomu yangu upeleke ripoti silipwi mshahara, *passport* ya *diplomatic* mliyokuwa nayo nyinyi sisi hatupewi hatutambuliki, hatuna *service* yeyote tunayoipata kutoka serikalini. Kwa nini vitu vyetu mnataka mviandike? Unahusika kwenye serikali ni wewe bali sio sisi. Mhe. Spika, ningeomba sana ni vyema kwa wale ambao wake zetu waliokubali mfano tutaandika, lakini kwa wale ambao hawajakubali inawezekana kuna wanaume wanapigwa mangumi nyumbani maana kuna wanawake wamesomea *boxing, karate,* wanawake wababe usifikirie kama mwanamme atakwenda pale atapewa vitu. Tunamuomba sana Mwenyekiti wa Tume ya Maadili atakapoona kwamba kuna

fomu upande wa wake zetu hazijaandikwa vizuri ajue kuwa kuna matatizo hayo na inafika wakati tunagomewa. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, mimi niseme wazi kabisa kwamba tumshukuru sana Mwenyezi Mungu kutupatia Rais Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini tushukuru sana kutupatia Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Hemed Suleiman Abdalla na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Naamini kwa kazi nzuri waliyoanza na spidi kubwa waliyoanza wizara hii na kitengo hichi cha Maadili ya Viongozi wa Umma kitapiga hatua sana na kitafika mbali na malengo yao yatatimia. Kwa siku ya leo sio siku ya kuwakataza au kuwagombeza au kuwashauri kitu nahisi ni mapema sana, lakini niseme wazi kwamba uchunguzaji huu uende kwa wajumbe wote au watendaji wote wa serikali hususan ngazi za kati kwenda juu isiwe peke yetu Wawakilishi na baadhi ya watu. Kama wanataka kuchunguza, wanataka kumiliki watu ili mambo yaende vizuri basi waajiriwa wote wa serikali hususan kipato cha kati kati kwenda juu na wao vile vile wapeleke hizi ripoti serikali iweze kuona inafanya nini, baada wakishakuweka *system* iliyokuwa nzuri hata watendaji wa chini ndipo lengo ambalo amelitaka Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi tutafikia. Mhe. Spika, badala ya hayo leo sitaki kuzungumza sana nikushukuru sana na mimi ripoti yangu ndio hiyo niliyoichangia kwa leo, ahsante sana. Naunga mkono asilimia mia moja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, naomba sasa nimwite Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum na Mhe. Omar Said Shaaban ajiandae.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ripoti ya nne. Nachukua fursa hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri kutokana na kuwasilisha ripoti hii ambayo ipo *very comprehensive* na ina maelekezo mengi. Mimi nina machache tu ya kuzungumza kuhusiana na ripoti hii. Kwanza na mimi niungane na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kuwapongeza sana wenzetu wa Tume ya Maadili ya Viongozi wamekuwa *very cooperative actually* mimi ni mara yangu ya kwanza kujaza fomu lakini nilipofika pale kiukweli mapokezi yao, maelekezo yao, hata *communication* pia ilikuwa ni nzuri ni ya hali ya juu, unajisikia maana yake ipo *very friendly*. Kwa hiyo, mimi nawapongeza na tunaomba basi hilo liendelee.

Mhe. Spika, jambo la pili kuhusiana na ukurasa wa kumi na tano Mhe. Waziri anasisitiza viongozi waharakishe kuhaulisha mali hususan zile ambazo hazihamishiki. Lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri ugumu unaotokea katika kuhaulisha hususan kwenye ardhi. Nadhani ni vyema sasa tume yako ikakaa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuona urahisi wa kuhaulisha ardhi na hili si tu kwa upande wa viongozi lakini katika jamii ya wananchi kwamba kuhaulisha ardhi limekuwa ni jambo gumu mno. Kwa hiyo, ndio maana hata wananchi wanauziana kienyeji halafu tena kunaweza kukatokea migogoro lakini kwa sababu kumekuwa na ukiritimba pamoja na mambo mazito ambayo yanaendelea pale Wizara ya Ardhi. Kwa hivyo, tunaomba ili hili jambo liwe jepesi kwa wananchi wote tuangalie utaratibu bora zaidi kuhakikisha kwamba wananchi wanahaulisha ardhi.

Kwanza, kuhaulisha mbali, lakini vile vile hata ile *evaluation* inayofanyika. *Evaluation* wanafanya wao wenyewe Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi halafu unakuja wewe ndio unapewa hiyo pesa uende ukalipe. Hakuna mtu atakayeweza kufanya hivyo. Kwa hiyo,

tunaomba uangaliwe utaratibu mzuri zaidi na elimu imetolewa sana lakini utendaji ndio ambao unarejesha nyuma katika zoezi hili.

La pili Mhe. Spika, kuna maelekezo ya jadweli ambayo yanakwenda sambamba na jadweli namba nne katika ukurasa huu wa kumi na tano kuhusiana na mambo ambayo yanapelekea, yameripotiwa kuhusiana na huo ukiukwaji wa maadili ya viongozi ikiwemo malalamiko yanayohusiana na ubadhirifu wa mali za umma, udhalilishaji wa kijinsia, uonevu, upendeleo katika ajira, kashfa na matumizi ya matusi na mgongano wa kimaslahi. Lakini tumesahau sasa hivi tunapokwenda katika suala zima la sayansi na teknolojia tunaona baadhi ya viongozi wengine wateuliwa kabisa na Mhe. Rais wanaingia huko *you tube* wengine kuweka kwenye *snap chat*, wengine kwenye *instagram* wanafanya mambo ya ajabu kweli.

Sasa hilo limeendelea kwa muda mrefu mpaka sasa inakithiri wananchi wanadhania ingawa inawakera lakini wanaona labda ile ndio *fashion.* Sasa tunashindwa kupambanua lipi jambo la mtu binafsi kufanya kutumia mitandao ya kijamii na lipi linambana yeye kama kiongozi wa umma. Tunaomba Mhe. Waziri sasa hivi teknolojia imekua ni mambo gani hasa yanawafanya viongozi wa umma wasiwe katika matumizi yasiyo sahihi ya mitandao ya kijamii. Utaona tu kiongozi wa umma anacheza taarab wengine wanaimba kabisa mtu kajiweka kwenye *you tube* yaani unasema huyu kiongozi. Ile peke yake inasababisha taswira nzima ya viongozi katika serikali inakuwa inaondoka.

Anayekuwepo pale wakati wote anakuwa ni *representative* wa Serikali lakini hatujaona Tume ya Maadili kuchukua hatua yoyote katika maeneo yale. Kwa hiyo, tunaomba wakati tunaokwenda matumizi wa sayansi na teknolojia hususan matumizi ya mitandao ya kijamii yawe vile vile yamejikita ikiwa kama *factor* moja ya kuangaliwa kupima maadili ya viongozi wa umma. *Otherwise* mimi nashukuru nadhani ripoti imekaa vizuri zaidi na naiunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, naomba sasa nimwite Mhe. Omar Said Shaaban na Mhe. Shaib Hassan Kaduara ajiandae.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante sana Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu leo. Lakini pili, nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa chama changu cha *ACT* Wazalendo kwa imani kubwa waliyokuwa nayo na kupendekeza jina langu kwa Mhe. Rais. Pia nimshukuru Mhe. Rais kwa kuridhia kuniteuwa kuwa mwakilishi wa chombo hiki kikubwa, ahsante sana. Naomba niipongeze Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kisheria kwa kuandaa ripoti hii na ambayo hatimae tunayo leo tunaijadili.

Mhe. Spika, mimi nitachangia kwa ufupi ripoti hii na hasa kwenye mambo mawili makubwa. Mhe. Spika, muundo wa tume yetu ulivyo kimsingi umefika wakati sasa tume waone kuna haja ya kuufanyia marekebisho. Muundo wa tume kwa mujibu ulivyo unaanzisha tume peke yake na imeipa mamlaka tume yenyewe kupokea taarifa, yenyewe kuchunguza taarifa na yenyewe kutoa hukumu juu ya taarifa zinazowasilishwa. Yaani yenyewe inachunguza na kuhukumu nafikiri ifike wakati sasa muundo wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ubadilishwe na waanzishe Baraza au chombo tofauti cha kujitegemea ambacho tume baada ya kupokea na kuchunguza

taarifa itapeleka kwenye hicho chombo kwa ajili ya kutolewa maamuzi kama kiongozi huyo wa umma amekiuka maadili au laa.

Mfumo wetu huu tuliokuwa nao unakiuka misingi muhimu ya kisheria inayokatazwa kisheria ya mtu kuwa *judge of his own cause* kwa maana ya kuwa hakimu wa jambo lake mwenyewe alilolianzisha. Kwa hivyo, mimi nafikiri Mhe. Spika, tuombe Mhe. Waziri walione hili na siku za mbele waone haja ya kuleta mabadiliko ya sheria kuanzisha chombo kinachojitegemea na Tume yenyewe iwe na jukumu tu la kupokea malalamiko ya kuyachunguza na hatimae kuyapelekea kwenye chombo tofauti ambacho kitatoa maamuzi kwamba huyu kiongozi wa umma amekiuka maadili au laa.

Jambo la pili ambalo ningependa kulichangia kwenye hili hili suala la Maadili ya Viongozi wa Umma. Tumeona Tume imefanya kazi zake na mimi binafsi naipongeza lakini kwa mujibu wa matakwa ya sheria moja kati ya mambo ambayo ni uvunjifu wa maadili kwa kiongozi wa umma ni kujiingiza kwenye mambo yenye mgongano wa kimaslahi. Ifike wakati sasa tume na kupitia Waziri Mhe. Spika, waje na kanuni kutoa tafsiri ya vitendo gani vina *attract* mgongano wa kimaslahi kwa viongozi wa umma. Nasema haya kwa sababu tumeona yanajitokeza katika maeneo mengi ambapo viongozi wa umma wanajihusisha na mambo ambayo wana maslahi nayo binafsi na naamini kanuni hizo sheria inampa Waziri uwezo wa kutunga kanuni. Sasa tume kupitia kwa Waziri ione haja ya kuja na kanuni zitakazo-*identify* matendo gani ambayo yatahesabika kwamba haya kiongozi wa umma akiyafanya yana-*attract* mgongano wa kimaslahi na hivyo hatatakiwa kuyafanya.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi niseme tu kwanza niipongeze tume kwa kutekeleza wajibu kisheria kutuletea ripoti hii na niungane na Waheshimiwa Wajumbe waliopita kwa kweli tume wanajitahidi sana katika kuhudumia wateja wao. Sisi binafsi ambao mara ya kwanza tumekuwa tukijaza fomu hizi mapokezi na namna ambavyo wanawafuata wateja wao na kuhakikisha ya kwamba wana-*comply* na sheria ni jambo ambalo kwa kweli linatakiwa liigwe na taasisi nyingi za serikali, ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Omar Said Shaaban, naomba sasa nimwite Mhe. Shaib Hassan Kaduara.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ndani ya Baraza lako hili. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uhai na uzima ndani ya muda huu wa alaasiri.

Mhe. Spika, naomba kuchangia Tume hii ya Maadili Sheria Nam. 4 ya mwaka 2015. Mimi naona tume yetu haikupewa meno mazima ya kutafuna, tumeona awamu tofauti tofauti zilizopita baadae tukaja tukasikia kuna ubadhirifu huu na kiongozi huyu amefanya hivi na huyu amefanya hivi, yote haya najua kutokana na umahiri wa wafanyakazi wa tume hii najua kwamba hayo mambo wameyaona na wameyachunguza. Lakini kutokana na kwamba haina meno vizuri sheria iliyowapa mamlaka ya kuwepo hii tume. Kwa hivyo, wao bado sio waamuzi wa kumhukumu mtu. Mimi ningeomba tume hii ingepewa nguvu ya ziada ili ikaendelea kuwalea viongozi katika maadili vile vile ikaweza kusimamia maadili yetu ndani ya viongozi yasije yakatiririka chini yakasababisha matatizo kama tuliyokuwa nayo sasa hivi.

Mhe. Spika, baada ya tanbihi hiyo na mimi naomba niunge mkono hoja hii vile vile niendelee kuwapongeza ndugu zetu hawa waendelee kufanya kazi kwa uadilifu na jitihada kubwa kwa kulijenga taifa letu, ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Shaib Hassan Kaduara. Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili aweze kuhitimisha hii hoja.
**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, awali ya yote nikushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia alaasiri ya leo kuendelea na kikao chetu hichi. Mhe. Spika, waliochangia ni waheshimiwa watano naomba niwatambue na kuwataja rasmi.

1) Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
2) Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
3) Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum
4) Mhe. Omar Said Shaaban
5) Mhe. Shaib Hassan Kaduara

Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa maoni yao na mengi kama walivyosema wenyewe ni maoni tumeyapokea na nishukuru sana kwa pongezi ambazo wamepata wafanyakazi wa Tume ya Maadili. Kwa kweli tulikuwa na wasi wasi pengine watu watasema baadhi ya taarifa zao pengine zimevuja na zimesikika pahala fulani kwa sababu hali ya mitandao ilivyo inatisha wakati mwengine.

Mhe. Spika, Mhe. Saada Mkuya Salum amezungumza vizuri sana mitandao siku hizi inapenya popote pale ina ncha kali. Lakini nashukuru sana viongozi wote waliosimama wamepongeza na Mwenyekiti yupo pale anasikia na mimi kama Waziri ninayesimamia masuala haya nimesikia nashukuru na tutaendelea kuwa pamoja na kuwapa moyo wafanyakazi wetu ili wafanye kazi vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kubwa zaidi lililozungumzwa ni ushauri kama nilivyosema Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf nikurejeshe kidogo mwaka 2015 Sheria Nam. 4 ukiisoma imeeleza maeneo yote ambayo hayafai kwa kiongozi wa umma kuyafanya, siwezi kuyataja yote ni mengi wakati mwengine hata zile lugha tunazozungumza hapa Barazani zinakuwa nje ya maadili. Sasa wakati mwengine hata hizo lugha zinaweza kufikia kwamba matumizi mabaya ya lugha yanaweza yakaleta tafsiri nyengine wewe hukuwa na nia mbaya, lakini katika kuzungumza tu inatokezea wakati mwengine. Lakini kuna masuala mengi sana mheshimiwa kazungumza kweli sheria zinazungumza wakati nyengine Mhe. Shaib Hassan Kaduara kazungumza vile vile hapa yeye kazungumza suala la kutoa meno.

Nataka nitoe ufafanuzi kidogo tume hii ya maadili sio kwamba haina meno tume inafanya kazi na ripoti zake zote inaziwasilisha kwa Mhe. Rais, yule ambaye yupo kwenye mamlaka ya Rais basi anapelekewa Mhe. Rais ndio mwenye maamuzi, kuna teuzi zinafanywa na mawaziri, kuna washauri wa mawaziri, kuna wakurugenzi wanateuliwa na mazaziri wale ambao ni mamlaka ya kuteuliwa basi wakiteuliwa huwa basi wanapelekwa ili wahusike kuchukua hatua hizo. Nashukuru sana kwamba tume hii imeendelea kufanya kazi na wale wote ambao wamekwenda

kinyume na maadili basi viongozi wahusika waliitwa na wamechukuliwa hatua ama kuonywa au kupewa maelekezo mengine. Lakini mambo haya ni ya siri na hatuwezi kuyatoa hadharani na moja katika ya *ethics* ya tume hii ni kutunza siri za viongozi wote na nashukuru mpaka dakika hii hilo limewezekana.

Kwa hivyo, mambo ni mengi sana yaliyozungumzwa kwa ufupi ni ushauri na tumeupokea. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum umezungumza suala baadhi ya viongozi ambao wameteuliwa na Rais pengine wanatumia vibaya mitandao, kuna sheria ile ya matumizi ya mitandano ya *TCRA* nadhani sheria ile inawabana wale kwa sababu kila sheria ina wajibu wake. Kwa mfano, Mhe. Shaib Hassan Kaduara kazungumza kwamba tume ipewe meno kuna mambo yaliyoonekana katika tume iliyopita baadhi ya watendaji walifanya, lakini kuna mambo katika kuzuia rushwa na wahujumu uchumi wao ndio walipewa meno yale na tayari taarifa tunazo hatuwezi kutaja hadharani wale wote ambao wamechukuliwa hatua ndio waliosimamishwa kazi wanajulikana sasa hivi na uchunguzi unaendelea na karibu taarifa zao zitapatikana.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nawashukuru wajumbe wote waliochangia niwatakie kila la kheri na nawaahidi tutaendelea kuimarisha imani kwa wao ili waiamini tume yetu tuweze kufanya kazi vizuri. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji wale wote wanaopokea taarifa hiyo ya ripoti ya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2019/2020 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2018/2019**

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya leo. Naomba sasa niwasilishe Ripoti rasmi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2018/2019.

Awali ya yote, naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kutimiza majukumu yetu ya kila siku. Pia napenda kuchukua fursa hii kupitia kwako Mhe. Spika, kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi namna anavyosimamia masuala ya udhibiti wa fedha za serikali na kujenga nidhamu ndani ya serikali hasa katika matumizi ya serikali, hivi sasa taasisi zetu zote ziko makini katika kusimamia suala hilo. Nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa jitihada zako unazozichukua katika kuimarisha misingi ya utawala bora katika Baraza la Wawakilishi, ambapo jitihada hizi zimepelekea kuimarika kwa uwajibikaji na nidhamu kwa uendeshaji wa vikao vya Baraza la Wawakilishi kwa kipindi chote hicho.

Mhe. Spika, aidha, nachukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza hili la Wawakilishi kwa kipindi chengine cha miaka mitano, namuomba Mwenyezi Mungu akujaalie hekima, busara na upeo katika uendeshaji kazi za Baraza la Wawakilishi pamoja na shughuli nyengine za Baraza na Serikali kwa ujumla. Aidha, nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na viongozi wote walioteuliwa katika nafasi mbali mbali za kuchaguliwa. Nawatakia kila la kheri katika kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa hatua walizochukua katika kufanyia kazi ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka yote ambayo hatua mbali mbali zimechukuliwa na Serikali katika kuimarisha watendaji, uwajibikaji, nidhamu katika matumizi ya fedha na rasilimali za umma.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuchukua nafasi hii kuwasilisha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo ofisi imefanikiwa kukamilisha ukaguzi wa hesabu za Serikali na Mashirika pamoja na taasisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kukagua hesabu za mwaka wa fedha 2018/2019 kwa Wizara na Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Natumai kwamba ripoti hizi zitapokelewa na kufanyiwa kazi ili kuweza kupata hali halisi ya mwenendo wa utendaji wa kazi wa Serikali pamoja na udhibiti wa masuala ya fedha na rasilimali za umma kwa lengo la kuimarisha uwazi, uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali hizo. Kuimarika kwa uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma kumepelekea kuimarika kwa utawala bora katika ukusanyaji wa mapato na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.

**Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

Mhe. Spika, Mdhibiti anakuwa anazindua hesabu za Serikali na anawajibika kikatiba katika kukagua hesabu za Mawizara, Taasisi za Serikali pamoja na Mashirika ya Umma na baadae kutoa taarifa ya ukaguzi kwa hesabu hiyo kila mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 112 cha Katiba ya Zanzibar kifungu namba 3 ya mwaka 1984. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hukabidhi ripoti hizo kwa Mhe. Rais kwa mujibu wa kifungu hicho cha katiba.

a) Mhe. Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zinazohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo.

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanywa ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wetu wa Serikali ya Zanzibar, hesabu za Mahakama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vinavyoainishwa katika katiba hii na hesabu zote zinazohusika katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 112 sehemu ya 5 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Zanzibar anawajibika kufanya mambo yafuatayo:-

a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa katika Mfuko Mkuu wa Hazina na Serikali ya Zanzibar matumizi yake yanaidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba matumizi hayo na masharti hayo yametekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Vile vile Mhe. Spika, atahakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zinazohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo ya fedha.

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahakama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoainishwa na katiba hii na hesabu zote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi.

**Uwasilishaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 112 sehemu ya 5 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kuwasilisha taarifa ya ukaguzi mara atakapomaliza kufanya kazi hiyo ya ukaguzi, taarifa ambazo zinaonesha hali halisi ya mwenendo mzima wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma kwa kipindi kilichokaguliwa.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kutoa mchango mkubwa kwa kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha na rasilimali za umma na kuhakikisha kwamba kunakuwa na utawala bora nchini na hatimae kuleta maendeleo endelevu kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar, kuimarika kwa ukaguzi wa hesabu kunapelekea kuimarika kwa utawala bora nchini. Kazi ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ni muhimu sana katika kuimarisha utawala bora katika matumizi ya rasilimali za umma ambayo inahitaji uadilifu, uwazi, uwajibikaji, ushirikishwaji wa watu na usawa wenye kufuata sheria ili kuleta ufanisi, tija na maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

**Upeo na Madhumuni ya Ripoti ya Ukaguzi**

Mhe. Spika, ripoti hizo zimekusanya taarifa za ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pia ikiwemo Mawizara, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi mbali mbali za Serikali kwa kuzingatia taarifa za mapato na matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo pamoja na michango mbali mbali kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019.

Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ukaguzi wa hesabu uliofanyika umejumuisha hesabu za Mawizara, Mashirika, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo jumla ya hesabu 94 ziliwasilishwa na kukaguliwa, kati ya hizo Wizara na Taasisi zake hesabu 65, Mamlaka ya Serikali za Mitaa hesabu 11, Mashirika na Mamlaka hesabu 18.

Mhe. Spika, hesabu za mwisho za mwaka wa fedha 2018/2019 za Mawizara, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimewasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa muda uliotakiwa kwa mujibu wa sheria. Uwasilishwaji huo umefanywa kwa kuzingatia sheria na usimamizi wa fedha za umma Nam. 12 ya mwaka 2016 kifungu cha 119(1) ambapo taasisi zote za Serikali zinawajibika kutayarisha na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwaka zinazojumuisha mapato na matumizi ya taasisi husika. Mafanikio makubwa yamepatikana katika uwasilishwaji wa hesabu za mwisho za mwaka kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi na kupelekea kufanyika kwa kazi za ukaguzi kwa wakati na kwa mujibu wa sheria.

**Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 kumekuwa na mafanikio makubwa katika usimamizi wa kusimamia mapato pamoja na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali ukilinganisha na mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 mapato yaliyokaridiwa kukusanywa jumla ya Shs. 1,305,228,722,000/= yamekadiriwa na makadirio hayo yalitarajiwa katika vianzio mbali mbali ikiwemo mikopo, misaada kibajeti na mashirika ya maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni, 2019 jumla ya Shs. 1,119,423,045,000/= zimekusanywa ambapo ni sawa na asilimia 85. 11

**Mapato Yanayotokana na Makusanyo ya Kodi**

Mwaka 2018/2019 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikadiria kukusanya jumla ya Shs. 711,500,000,000/= mapato hayo yanatokana na kodi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019 makusanyo halisi yanayotokana na kodi yalikuwa Shs. 650,108,425,000/= ikiwa ni sawa na asilimia 91.37 ya makadirio. Kumekuwa na upungufu wa Shs. 61,391,575,000/= sawa na asilimia 8.63 ya makadirio.

Ukaguzi umebaini kwamba makusanyo yanayotokana na kodi yameongezeka kutoka Shs. 602,755,650,000/= kwa mwaka 2017/2018. Hadi kufukia Shs. 650,108,425,000/= kwa mwaka 2018/2019 ikiwa ni ongezeko la Shs. 47,352,775,000/= sawa na asilimia 7.86 ya ongezeko.

**Ukusanyaji wa Mapato katika Mawizara na Taasisi za Serikali:**

Kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali zilikadiriwa kukusanya jumla ya Shs. 66,128,722,000/=. Hadi kufikia 30 Juni, 2019 makusanyo halisi yalikuwa Shs. 66,619,342,000/= ambapo ni sawa na asilimia 100.74 ya makadirio hivyo kuonesha ongezeko la makusanyo ya Shs. 490, 620,000/= sawa na asilimia 0.74 ya ongezeko.

Ukaguzi umebaini kwamba makusanyo hayo yameongezeka kutoka Shs. 48,955,585,000/= kwa mwaka 2017/2018 hadi kufikia Shs. 66,619,342,000/= kwa mwaka 2018/2019 ikiwa ni ongezeko la Shs. 17,663,757,000/= sawa na asilimia 36.08 ya ongezeko. Ongezeko la makusanyo limetokana na jitihada mbali mbali zilizochukuliwa na serikali katika kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato hayo.

**Taarifa ya Matumizi**

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitarajia kutumia jumla ya shilingi 1,315,228,772,000/= kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kati ya fedha hizo bilioni 727,128,772,000/= ni kwa kazi za kawaida na shilingi bilioni 588,100,000,000/= zilikadiriwa kutumika kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia Juni 2019 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitumia shilingi 1,134,499,079,000/= kati ya hizo bilioni 704,419,217,000/= zilitumika kwa kazi za kawaida na bilioni 430,970,862,000/= zilitumika kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 serikali ilikadiria kutumia shilingi i 727,128,000,772/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ambapo jumla ya shilingi bilioni 704,419,217,000/= zimetumika kwa kazi za matumizi ya kawaida sawa na asilimia 96.88.

**Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Maendeleo**

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 serikali ilikadiria kutumia shilingi 588,100,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Hadi kufikia Juni 30, 2019 jumla ya shilingi bilioni 430,970,862,000/= zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 73 ya makadirio.

**Deni la Taifa**

Mhe. Spika, ukaguzi umebaini kwamba deni la serikali katika kipindi cha mwaka fedha unaoishia tarehe 30 Juni umeongezeka kutoka shilingi bilioni 512,527,686,419/= kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hadi kufikia bilioni 841,201,658,229/= kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo deni la hilo limejumuisha deni la ndani la shilingi billion 167,801,078,000/= na deni na nje shilingi bilioni 673,400,580,629/=kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama inavyoonesha kwenye jadweli hapo chini.

**Muhtasari wa Mambo Yaliyobainika**

Mhe. Spika, katika ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya hesabu 94 zilikaguliwa na kutolewa maoni ya ukaguzi. Taasisi zilizokaguliwa zilipata hati za ukaguzi ambazo hati 93 zilizokaguliwa, zinazoridhisha zilitolewa kwa wizara na taasisi mbali mbali na hati moja isiyoridhisha imetolewa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Katika ukaguzi huo zilijitokeza dosari mbali mbali za kiutendaji ambapo baadhi ya dosari hizo zilirekebishwa baada ya kupatiwa maelezo na vielezo kuhusiana na hoja mbali mbali za ukaguzi zilizotolewa kwa taasisi zilizokaguliwa.

Hata hivyo, kulijitokeza baadhi ya dosari ambazo hazikuweza kurekebishika kutoka na kukosekana kwa maelezo au vielezo kuhusu hoja za ukaguzi zilizobainika na kupelekea kupatikana kwa hoja za ukaguzi ambazo hazikujibika, baadhi ya hoja hizo ni kama hivi zifuatavyo:

**Dosari za kiutendaji zilizobainika katika ukaguzi**

Katika ukaguzi wa hesabu ya mwaka 2018/2019 kumejitokeza dosari za kiutendaji ambazo zimefanyika kuathiri utendaji wa taasisi zilizokaguliwa pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali.

Dosari hizo ni kama zifuatazo:

1. Mfumo wa udhibiti wa ndani

2. Utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Uondoshaji wa Mali za Umma na Sheria za Hatua za Umma

3. Usimamizi wa matumizi

**Mfumo wa Udhibiti wa Ndani**

Mfumo wa Udhibiti wa Ndani taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na usimamizi wa fedha ambazo unahitajika kuwa imara ili kuweza kusaidia Taasisi ya Umma kuweza kufanya kazi zake kwa uweledi na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi umebaini udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani na baadhi ya taasisi za wizara kutokuwa na kamati za ukaguzi wa ndani na kutokufanya kazi kwa kamati hizo, kutokufanya kazi kwa kamati za ndani *audit committee* kunaweza kupelekea dosari ya kiutendaji kushindwa kuchukuliwa hatua za awali pale panapojitokeza. Aidha, ukaguzi umebaini vitengo vya ukaguzi wa ndani *Internal Audit Unit* kwa baadhi ya taasisi na wizara zilizokaguliwa hazikuwasilisa ripoti za ukaguzi wa hesabu katika kipindi cha ukaguzi pamoja na kushindwa kukutana na kamati ya ukaguzi wa ndani kwa lengo la kufanyia kazi ripoti ya ukaguzi na kutoa mapendekezo kwa uongozi katika taasisi husika.

**Utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma pamoja na Sheria ya fedha za Umma**

Ukaguzi umebaini kutofuatwa kikamilifu kwa Sheria ya Manunuzi na Uendeshaji wa Mali ya Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Fedha ya Umma namba 12 ya mwaka 2016 kwa baadhi ya taasisi na wizara jambo ambalo limefanyika kujitokeza kwa dosari za ukiukwaji na taratibu za manunuzi kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Manunuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma, pamoja na kukiukwa taratibu za malipo kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Fedha za Umma.

**Usimamizi na Matumizi**

Ukaguzi umebaini dosari katika usimamizi wa matumizi ya mali za taasisi ya serikali kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa usimamizi wa matumizi kumepeleka ukaguzi kushindwa kusibitisha uhalali wa matumizi hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

**Mambo ya Kuzingatia katika Ukaguzi uliofanyika Wizara ya Fedha na Mipango Mfuko Mkuu wa Serikali**

Mhe. Spika, katika ukaguzi uliofanyika katika Mfuko Mkuu wa Serikali umebainika kufanyika kwa matumizi mbali mbali ambayo taratibu za manunuzi hazikufuatwa ipasavyo kwa kukosekana kwa vielelezo na maelezo kuhusiana na matumizi hayo. Hivyo, ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo, hali iliyopelekea ukaguzi kutoa angalizo katika matumizi yafuatayo:-

Malipo ya deni yaliyolipwa na Mfuko Mkuu wa Serikali yasiyo na uthibitisho ya shilingi milioni 57,476,732/=. Ukaguzi umebaini kufanyika kwa malipo ya shilingi 57,476,732/= kwa Fahmi Khalifa.

Mfuko Mkuu wa Serikali umemlipa Fahmi Khalifa kiasi cha shilingi 57,476,732/= kupitia hati ya malipo nambari 117/9 ya tarehe 19/9/2018 ikiwa malipo ya awamu ya mwisho ya deni la ununuzi wa vifaa mbali mbali vya ujenzi vilivyotumika Chuo cha Mafunzo.

Ufisadi uliobainika ni kukosekana kwa barua kutoka Chuo cha Mafunzo inayothibitisha uwepo wa deni hilo, aidha mkataba wa malipo kati ya Fahmi Khalifa na Chuo cha mafunzo haukupatikana kwa ukaguzi hali iliyopelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Mhe. Spika, dosari katika malipo adhabu ya kushindwa kulipa madeni riba ya dola 505,243 sawa na wastani wa shilingi bilioni 1,157,365,736/= katika mwaka 2018/2019 ukaguzi umebaini kwamba hesabu za huduma Mfuko Mkuu wa Serikali umelipa jumla ya dola 505,443 sawa na wastani wa bilioni 1,157,995,736/= malipo hayo ni kwa ajili ya adhabu yaani *interest* zilizotonzwa na kampuni ya *Hassan Son's* kwa kutoa huduma ya serikali na kuchelewa kulipa madeni hayo kwa muda mrefu.

Hadi ukaguzi umekamilika mkataba baina mtoa huduma kampuni ya *Hassan Son's* na serikali haikuweza kupatikana, hivyo asili ya malipo hayo hazikupatikana kwa ukaguzi. Kufanya hivyo

ni kwenda kinyume na Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma sheria nambari 11 ya mwaka 2016. Aidha taarifa za kuwepo kwa deni hilo hazikupatikana kwa ukaguzi kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Hitimisho**

Kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru kwa dhati Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa juhudi zako na mikakati uliyochukua katika kusimamia uwajibikaji na uwazi katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali za serikali na kuhakikisha kwamba sheria mbali mbali zinafuatwa ipasavyo na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na wajibikaji katika usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha.

Ni dhahiri kabisa juhudi zako ulizozichukua katika kuimarisha utawala bora zimeleta mabadiliko makubwa katika utendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuleta ufanisi katika kazi za ukaguzi na hatimaye kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji kwa matumizi ya raslimali za umma.

Mhe. Spika, mafanikio hayo yametokana na uwajibikali mzuri na watendaji kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo pamoja na kufuata ushauri na mapendekezo yanayotolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pia udhibiti mzuri wa mapato na matumizi ya fedha za raslimali za umma.

Jitihada zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa ufuatiliaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimesaidia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa uwajibikaji katika utendaji wa shughuli za serikali na kupelekea kuirimarika kwa utendaji kazi wa taasisi za serikali.

Mhe. Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa kamati zote za Baraza la Wawakilishi kwa jitihadi zao zilizochukuliwa na kusimamia uwajibikaji katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Aidha, shukrani za pekee ziwaendee Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali *(PAC)* pamoja na Kamati ya Sheria na Utawala ya Idara Maalum kwa jitihada mbali mbali wanazochukua katika kutoa maelekezo, ushauri na maoni kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa ofisi pamoja na serikali kwa ujumla.

Maelekezo, ushauri, maoni yao na mchango uliotolewa na Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizo zote za Baraza la Wawakilishi yamesaidia sana kiasi kikubwa kuimarisha utekelezaji wa ripoti hii.

Nawashukuru viongozi na watendaji wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na watendaji wa taasisi mbali mbali za serikali kwa mashirikiano yao mazuri waliyotupa wakati wa kutekeleza majukumu hayo.

Mhe. Spika, naomba nikuhakikishie kwamba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itaendelea na jitihada zake za kuongeza ufanisi katika utendaji wake wa kutumia viwango vya taaluma vya ukaguzi wa kitaifa na kimataifa, ili tuweze kwenda sambamba na mabadiliko ya kazi ya ukaguzi yanayotokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla kwa kusimamia uwajibikaji, uwazi na matumizi ya rasilimali yao ili kufikia lengo la kuwa na utawala bora nchini na kuleta maendeleo ya nchi na ustawi kwa ujumla kwa wananchi wetu wa Zanzibar. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri na Waheshimiwa sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Mashirika na Serikali za Mitaa ili aje na yeye awasilishe. Karibu Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wajumbe, niwakumbusheni kwamba nimepata karatasi nyingi za watu wanaomba kuchangia hizi ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatutazichangia tutauliza maswali tu, tutaruhusu muulize maswali tutakuja kuzichangia katika mkutano mwengine unaofuata. Ahsante Mhe. Mwenyekiti karibu.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma (Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Mashirika na Serikali za Mitaa):** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika yaani *(LAAC)* kuhusu uwasilishaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Serikali za Mitaa na Mashirika kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika**,** awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wetu.

Mhe. Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika *(LAAC)* Kuhusu Uwasilishaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Serikali kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, pia, naomba kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 katika Mkutano wa Februari. Hii ni kutokana na kuwa Ripoti hizi mara kadhaa huwasilishwa katika Mkutano wa Baraza unaohusiana na mambo ya bajeti.

Mhe. Spika, shukrani za pekee zimfikie Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na watendaji wake wote wa Ofisi hiyo kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya na kufuatilia fedha za umma.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kwa mashirikiano yao wanayonipatia wakati wote wa kazi za Kamati ikiwa ni pamoja na wakati wa kuzipitia, kuzichambua na kuzijadili taarifa hizi muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa nguvu ili tuweze kutekeleza vyema majukumu tuliyopewa.

Mhe. Spika,naomba kuwataja kwa majina Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya *LAAC* kama ifuatavyo:-

| Na | Jina | Uwakilishi/ Utumishi | Nafasi |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mwakilishi, Jimbo la Dimani | Kaimu Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Shaib Hassan Kaduara | Mwakilishi, Jimbo la Chake Chake | Kaimu Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ali Abdulgulam Hussein | Mwakilishi, Jimbo la Jang’ombe | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | Mwakilishi, Jimbo la Wawi | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mwakilishi, Nafasi za Wanawake | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Rukia Omar Ramadhan | Mwakilishi, Jimbo la Amani | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Shadya Mohammed Suleiman | Mwakilishi, Nafasi Maalum za Wanawake | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Nasra Awadh Salmin | Afisa, Baraza la Wawakilishi Zanzibar | Katibu |
| 9. | Ndg. Othman Ali Haji | Afisa, Baraza la Wawakilishi Zanzibar | Katibu |

Mhe. Spika, kifungu cha 112(3)(c) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka. Mhe. Spika, Kamati ya *LAAC* imebaini kuwa masharti ya kifungu hiki hayatekelezwi ipasavyo, kwani yapo baadhi ya Mashirika hesabu zao hazikaguliwi kila mwaka na endepo zitakaguliwa katika mwaka unaofuata basi hesabu za miaka iliyopita huwa haziripotiwi tena katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, katika kuthibitisha kauli yangu hiyo naomba kutoa mifano kwa baadhi ya Mashirika hayo kama ifuatavyo: Shirika la Umeme la Zanzibar *(ZECO)*, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar *(ZSSF)* na Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)* hesabu zao za mwaka hazijaripotiwa takriban miaka mitatu mfululizo (yaani kuanzia Ripoti ya mwaka wa fedha mwaka 2015/2016, 2016/2017, 2017/2018) na badala yake hesabu zao zinaonekana za mwaka wa fedha 2018/2019 pekee wakati Mashirika haya yalikusanya mapato na kufanya matumizi yao katika kipindi chote hicho ambacho hesabu zao hazikukaguliwa na kuripotiwa.
Mhe. Spika, sambamba na hilo, tumebaini kuwa ripoti ya ukaguzi ya Shirika la Bima la Zanzibar haikuwahi kuwasilishwa ndani ya Baraza kwa kipindi chote cha uhai wa Baraza la Tisa la Wawakilishi na hata katika Ripoti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kwa mnasaba huo, ni miaka

minne sasa Shirika hilo taarifa zake za mapato na matumizi hazijawasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu kama Katiba ya Zanzibar inavyoelekeza.

Mhe. Spika, aidha, taarifa za ukaguzi wa hesabu za Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)* zimeripotiwa Barazani tangu mwaka wa fedha 2013/2014 na kuwasilishwa Barazani katika mwaka wa fedha 2016/2017 na hadi hivi sasa taarifa za ukaguzi wa hesabu za Bodi ya Mapato Zanzibar hazijaonekana tena katika Ripoti za Ukaguzi zinazowasilishwa Barazani.

Mhe. Spika, ingawa kifungu cha 112(7) cha Katiba ya Zanzibar kinapiga marufuku kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuata maagizo au amri ya mtu yeyote. Hata hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri wakati wa kufanya majumuisho yake alieleze Baraza hili kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar ni sababu zipi zilizopelekea Mashirika haya hesabu zao kutowasilishwa Barazani kila mwaka kama Katiba ya nchi inavyelekeza.

Vile vile, atueleze kwa kina ni sababu zipi zinazoikwaza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hata ikashindwa kuwasilisha taarifa za hesabu za Shirika la Bima la Zanzibar kwa miaka minne mfululizo sasa.

Mhe. Spika, Kamati ya *LAAC* imelazimika kuuliza maswali hayo hasa ikizingatiwa kuwa Mashirika haya yanaendelea kukusanya mapato na pia yanafanya matumizi, hivyo, Kamati hii haina uhakika kama shughuli hizo zinafanywa kwa uhalisia wake au laa, na hasa ikizingatiwa kuwa bajeti za Mashirika huwa hazipitishwi na Baraza hili.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, Baraza lako kuendelea kutokupokea ripoti za ukaguzi wa hesabu za Shirika la Bima na Bodi ya Mapato Zanzibar ni kwenda kinyume na Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Usimamizi wa Fedha Namba 12 ya mwaka 2016 pamoja na kuitia dosari dhamira kuu ya kuwepo kwa Kamati zinazosimamia masuala ya kifedha.

Mhe. Spika, Kamati ya *LAAC* inatambua na kuthamini sana kazi kubwa inayofanywa na Ofisi hii katika kujenga nidhamu ya matumizi ya rasimali za umma katika serikali na kuimarisha dhana ya Utawala Bora hapa nchini hasa ikizingatiwa kuwa Taasisi za Umma zimekuwa zikiongezeka ukilinganisha na miaka ya zamani. Hata hivyo, kamati hii hairidhishwi na tabia ya kutowasilishwa hesabu za ukaguzi kwa taasisi zote za umma kama kifungu cha 112(3)(c) cha Katiba ya Zanzibar kinavyoelekeza.

Mhe. Spika, kwa msingi huo, Kamati ya *LAAC* inaiomba serikali kuweka mikakati imara zaidi ya kuhakikisha kuwa changamoto zinazoifanya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hata isiweze kuzikagua taasisi zote za umma na kuwasilisha taarifa zake za ukaguzi wa hesabu Barazani zinafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili ofisi hiyo iweze kutekeleza majukumu yake kama Katiba na Sheria zinavyoelekeza.

Mhe. Spika, sambamba na kutokukaguliwa kwa Taasisi na Mashirika niliyokwisha kuyataja, Kamati ya *LAAC* inaungana na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*), juu ya kutoridhishwa kukiukwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya 2016, kifungu cha 122(5), inayomtaka Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, anayeisimamia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuwasilisha hapa Barazani Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, kamati yetu inaona kuna dosari kubwa ya Sheria hii ya Usimamizi wa Fedha kumpa dhamana waziri anayesimamia Ofisi ya Mdhibiti kuteua mtu ama kampuni ya kuikagua ofisi hii, wakati kiuhalisia waziri huyo ni Msimamizi wa ofisi hiyo. Aidha, dosari nyengine ni kuwa mtu huyo hulipwa malipo yake ya ukaguzi na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, huku tukijua kuwa siku zote, "Anayemlipa Mpiga Zumari, ndiye Anayechagua wimbo".

Mhe. Spika, hii ina maana utaratibu mzima wa kukaguliwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, unatia mashaka makubwa katika Misingi ya Utawala Bora, na ndio maana tokea kuanzishwa kwa Baraza hili na kuasisiwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hapa Zanzibar, haijawahi kutokea taarifa za ukaguzi wake kuwasilishwa na kujadiliwa Barazani na ni sawa na kusema, hakuna taarifa rasmi inayotambuliwa na Baraza hili na ya hakika kuwa ofisi hii imewahi kukaguliwa.

Mhe. Spika, katika Mabunge mengine ulimwenguni, Kamati ya *PAC* ama *LAAC*, ndio huteua mtu wa kuikagua Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu badala ya waziri anayehusika na ofisi hiyo, ni vyema wajumbe wako wakalitizama tena suala hili na hatimae haki yao ya kuzifahamu na kuzijadili hesabu za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ikapatikana ipasavyo.

Mhe. Spika, kiujumla Kamati ya *LAAC* inayapongeza Mashirika na Taasisi zote za Serikali zilizokaguliwa na taarifa zao za hesabu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kuwasilishwa Barazani zikiwa hazina hoja za moja kwa moja. Mhe. Spika, tunatoa pongezi hizo kwa kuwa kati ya Mashirika na Taasisi 18 zilizokaguliwa ni Mashirika mawili tu yaliyobainika kuwa na hoja ya moja kwa moja, inayoonesha upungufu wa matumizi ya fedha za umma. Mashirika yenyewe ni Shirika la Utangazaji Zanzibar na Shirika la Nyumba Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati ya *LAAC* inayaomba Mashirika haya kutekeleza vyema majukumu yao ili dhamira ya kuanzishwa kwao iweze kupatikana.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, Kamati ya *LAAC* inashangazwa sana na ripoti za Ukaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Serikali za Mitaa bila ya kufanya ukaguzi mwengine ikiwa ni pamoja na Ukaguzi Maalum wa Miradi Mikubwa ya Maendeleo, Ukaguzi Yakinifu (*Value for Money Audit*), Ukaguzi Maalum wa Mikataba ya Serikali na kaguzi nyengine za kitaalamu, tofauti na ukaguzi wa hesabu kwa zaidi ya miaka mitano sasa.

Jambo la kushangaza zaidi, ripoti hizo za hesabu kwa upande wa Mashirika zinazungumzia mambo yale yale ya Taarifa za Mapato, Taarifa za Matumizi na Hesabu za Mwisho wa Mwaka, huku katika uzoefu wa uchunguzi wa Kamati zetu za Kusimamia Masuala ya Fedha zinapofanya ukaguzi wake, hugundua kasoro nyingi za usimamizi wa fedha za umma na kukiukwa kwa taratibu za matumizi ya fedha hizo, zinazohusu Taasisi na Mashirika yaliyowahi kukaguliwa na ofisi hiyo.

Mhe. Spika, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali kwa mwaka 2018/2019 imerejea tena kutoa taarifa hizo hizo kama ilivyotolewa katika mwaka 2015/2016; 2016/2017 na huu mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika, pamoja na ukweli kuwa ofisi hii haielekezwi namna ya kutekeleza majukumu yake, ni vyema tukayasema haya ili kuikumbusha kubadilika hasa katika kwenda sambamba na kasi ya Serikali ya Awamu ya Nane, serikali iliyojipambanua kupiga vita kwa vitendo, vitendo vyote vya rushwa na ufisadi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu na Nane imeshakaa madarakani takriban kwa siku 100 tu sasa, na imeimarisha mno Utawala Bora nchini na kupiga vita ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma. Serikali hii imekuwa karibu sana na wananchi na inawasikiliza sana, imekuwa karibu na waandishi wa habari na inawaheshimu sana, imekuwa karibu na kila mtu na inamheshimu kila mtu.

Mhe. Spika, wananchi wanajiuliza masuala mengi sana kufuatia kasi na uwezo mkubwa wa Serikali hii ya Awamu na Nane kufichua ubadhirifu mkubwa wa mali za umma, wakati Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikuwepo muda wote, bila ya kuyaibua madhaifu hayo katika ripoti zake, huku Katiba ya Nchi hii na Sheria zake, zimempa Mamlaka na wajibu wa kuyaeleza hayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Wananchi hawa wanajiuliza alikuwa wapi, Alikuwa wapi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, wakati Mradi wa Ukarabati wa Jumba la Treni Darajani unaanza na kuendelea hadi kumaliza, huku zaidi ya bilioni 3 zikipotea na kuvurugwa kwa taratibu za manunuzi na kuvunjwa kwa Sheria za Kusimamia Fedha za Umma, wakati Ofisi ya Mdhibiti haikuyaeleza haya katika ripoti yake yoyote ile.

Mhe. Spika, wananchi wanauliza alikuwa wapi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, wakati Mradi wa *ZUSP* ulipoanza na kutekelezwa bila ya kueleza chochote katika kasoro zake, huku fedha za wananchi kupitia Mradi huo zikitumika kwa maslahi ya wachache na Mradi kutoleta tija iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, wananchi wanajiuliza alikuwa wapi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati fedha za Umma zikitumika kinyume na utaratibu ikiwa ni pamoja na kukithiri kwa wafanyakazi hewa, kuvurugwa kwa taratibu za manunuzi na wizi wa fedha za umma katika miradi mbali mbali iliyosimamiwa na baadhi ya Vikosi vya SMZ, huku baadhi ya wahasibu na baadhi ya Watendaji Wakuu wa baadhi ya vikosi hivyo, wakihusika na wizi wa mamilioni ya fedha za umma, bila ya kasoro hizo kuelezwa katika ripoti za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na hatimae kuja kuibuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Wasaidizi wake.

Mhe. Spika, wananchi wanasema alikuwa wapi Mdhibiti na kaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zaidi ya kueleza taarifa za Mapato na Mtumizi labda na Hesabu za Mwisho wa Mwaka, kwa Shirika la Bandari na Shirika la Meli, wakati fedha zilizopatikana kwa kiwango kikubwa katika Mashirika hayo, zilitumika kwa ulafi na watendaji kujilumbikizia mali kupitia mgongo wa

Mashirika hayo, wakati kazi hii inakuja kuibuliwa katika siku 100 za Utumishi uliotukuka wa Mheshimwa Rais na wasaidizi wake.

Mhe. Spika, masuala ya alikuwa wapi ni mengi sana, na labda niwaachie baadhi ya Wajumbe wako wa Baraza hili wamuulize Mhe. Waziri pale utakapopendezewa kuwapa nafasi ya kuuliza masuala kuhusiana na ripoti hizi za ukaguzi zilizowasilishwa.

Mhe. Spika, kasoro nyengine inayohitaji kufanyiwa kazi kwa haraka na ni maarufu kwa ofisi hii, ni kuwa nyuma katika kazi zake za ukaguzi. Mpaka leo mwaka 2020/2021, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, bado inawasilisha Barazani ripoti zilizokwishapitwa na muda, za mwaka 2018/2019, hali inayozifanya kamati zetu kushindwa kuisimamia vyema serikali, kwani hata ukifuatilia ripoti hizo, kamati zinakutana na mambo mengi yanayoshindwa kupatiwa ufumbuzi kwa wakati tulionao sasa.

Mfano wa changamoto hizo ni kuondoshwa kwa Maafisa Masuuli waliohusika na uzembe na ubadhirifu wa mali za umma, kumaliza muda wa Bodi za Wakurugenzi na Mabaraza ya Vyuo, kutopata tena taarifa zinazokwenda na wakati kutoka kwa Mashirika na Taasisi hizo pamoja na kuzifanya kamati zetu kuonekana kama kituko kwa kufuatilia taarifa za mapato na matumizi yaliyokwisha kupitwa na mwaka wake wa matumizi.

Mhe. Spika, Kamati ya *LAAC* inafahamu juhudi zinazochukuliwa na ofisi hii na inaziheshimu, na kwa kuyasema haya, kamati yetu inaihitaji ofisi hii kama inavyoiomba serikali, kuhakikisha ukaguzi wake unakwenda na wakati.

Mhe. Spika, Kamati ya *LAAC* ilipohitaji kufanya tathmini fupi ya kuongezeka kwa makusanyo kwa miaka miwili kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi, imesikitishwa kuona taarifa hizo zinatofautiana katika ripoti mbili za ukaguzi wa hesabu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baina ya mwaka 2017/2018 na 2018/2019, jambo linaloipa shida kamati wakati wa kutekeleza kazi zake za ukaguzi na pia inatia doa kwa ofisi kubwa yenye wataalamu waliobobea kwa kazi za ukaguzi, hasa ikizingatiwa heshima ya ofisi hiyo. Aidha, kamati inaomba ofisi hii iwe makini katika kutoa taarifa zake juu ya Taasisi na Mashirika ya Serikali, ili kuzifanya kazi za kamati zitekelezwe kwa wepesi mkubwa, sambamba na kulinda heshima ya ofisi hii.

Mhe. Spika, Kamati ya *LAAC*, imeona vyema kuonesha kasoro hiyo kwa baadhi ya Taasisi na Mashirika hayo kama ifuatavyo:-

| **JINA LA TAASISI/ SHIRIKA** | **MAPATO HALISI YALIYOELEZWA 2017/2018** | **MAPATO HALISI YALIYOELEZWA 2018/2019** | **TOFAUTI** |
|---|---|---|---|
| Shirika la Bandari | 34,361,996,258 | 38,246,498,086.74 | 3,884,501,828.74 |
| Mamlaka ya Viwanja vya Ndege | 11,039,978,607.88 | 11,730,617,475 | 690,638,867.12 |
| Mamlaka ya Udhibiti wa | 16,362,952,000 | 16,362,951,000 | 1,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Huduma za Maji na Nishati Zanzibar | | | |
| Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar | Yameelezwa kuwa ni 27,234,629,383 pia katika ripoti hiyo hiyo imesema kuwa ni 132,352,525,969.48 | 133,861,030,528.93 | 106,626,401,145.9 (kwa mlinganisho wa 27,234,629,383)<br>NA TOFAUTI YA 1,508,504,559.45 (kwa mlinganisho wa 132,352,525,969.48 |

Mhe. Spika, pamoja na kasoro hiyo iliyojitokeza Kamati ya *LAAC* kwa kuzingatia haja ya kufanya tathmini ya kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya Taasisi na Mashirika kwa miaka miwili ya ukaguzi wa hesabu zao za fedha (2017/2018 na 2018/2019), imejiridhisha kuwa, kuna Taasisi na Mashirika ya Serikali yanayoendelea kufanya vizuri katika kukusanya mapato yao na hivyo, kuimarisha uwezo wao wa kujiendesha na kutoitegemea serikali na pia yapo yanayofanya vibaya kwa kushuka kwa makusanyo ya mapato na hivyo kushuka kwa uwezo wao wa kujiendesha na kutoitegemea serikali kama ifuatavyo:-

| **MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOFANYA VIZURI KATIKA KUONGEZA MAKUSANYO YA MAPATO** | | | |
|---|---|---|---|
| NA. | JINA | 2017/2018 | 2018/2019 |
| 1. | Shirika la Bandari | 34,361,996,258 | 37,506,713,124.69 (sawa na ongezeko la asilimia 109) |
| 2. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege | 11,039,978,607.88 | 14,542,276,472.72 (sawa na asilimia 24 ya ongezeko) |
| 3. | Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) | 3,582,622,247 | 4,746,059,938.24 (sawa na ongezeko la asilimia 32.47) |
| 4. | Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*) | 2,225,588,021 | 2,516,366,245.5 (sawa na ongezeko la asilimia 13) |
| 5. | Chuo cha Utawala wa Umma (*IPA*) | 2,623,161,450 | 2,668,523,825 (sawa na ongezeko la asilimia 1.7) |
| 6. | Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asili Zanzibar (*ZPRA*) | 956,480,797 | 6,349,932,036.12 (sawa na ongezeko la asilimia 563.88) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Shirika la Nyumba Zanzibar | 2,007,144,882 | 2,878,682,812 (sawa na ongezeko la asilimia 43.42) |

Mhe. Spika, kwa upande wa Mashirika na Taasisi zinazofanya vibaya na kushuka kwa makusanyo yao ya mapato.

| **MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOFANYA VIBAYA KATIKA KUONGEZA MAKUSANYO YA MAPATO** | | | |
|---|---|---|---|
| **NA.** | **JINA** | **2017/2018** | **2018/2019** |
| 8. | Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*) | Tsh. 18,375,430,857 | 14,274,517,682 (sawa na asilimia 22.3 ya upungufu) |
| 9. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar | 16,362,952,000 | 16,330,859,000 (sawa na asilimia 0.2 ya upungufu) |
| 10. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar | 27,234,629,383 AU 132,352,529,967.48 | 9,991,220,910.84 (sawa na asilimia 92.5 ya upungufu) |
| 11. | Shirika la Magazeti | 1,429,540,404 | 1,341,801,136 (sawa na asilimia 6.14 ya upungufu) |
| 12. | Chuo cha Uandishi wa Habari | 770,048,355 | 769,988,075(sawa na asilimia 0.008 ya upungufu) |
| 13. | Mamlaka ya Usafiri Baharini | 3,718,893,422 | 2,491,553,437 (sawa na asilimia 33 ya upungufu) |
| 14. | Shirika la Meli na Uwakala | 10,156,959,371.01 | 10,149,725,091.66(sawa na upungufu wa asilimia 0.071) |

**Mhe. Spika:** Mhe. Mwenyekiti, una dakika tatu za kumalizia.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma (Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Mashirika na Serikali za Mitaa (*LAAC*):** Ahsante mheshimiwa namalizia. Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuna shilingi 27,234,629383.

Mhe. Spika, nadhani katika mashirika na taasisi zinazofanya vibaya tumebakisha kama mashirika matatu kuyasema naomba yaingie kwenye *Hansard* ili tuendelee na mambo mengine.

Mhe. Spika, Kamati ya *LAAC* inaendelea kuishauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuyafanyia tathmini Mashirika na Taasisi zote za Umma kwa kulinganisha miaka miwili ya fedha ili kuweza kupima uwezo wa Mashirika na Taasisi hizo katika miaka miwili ya fedha, lakini kama tulivyokwishasema awali, tathmini hiyo ifanywe kwa usahihi na uangalifu mkubwa.

Mhe. Spika, kwa upande wa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa, kati ya Taasisi 11 za Mabaraza ya Manispaa, Halmashauri na Mabaraza ya Miji ni taasisi moja tu ambayo haikupata hoja ya moja kwa moja, taasisi yenyewe ni Baraza la Mji Chake Chake.

Mhe. Spika, Kamati ya *LAAC* kwa huzuni kubwa inadiriki kutamka kuwa haikuridhika kabisa na matokeo ya ukaguzi wa hesabu wa taasisi hizi, ingawa ni taasisi moja tu kati ya taasisi 11 ambayo imepata hati isiyoridhisha. Taasisi yenyewe ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaskasini "A".

Mhe. Spika, kutokana na matokeo hayo mabaya ya ukaguzi tunaishauri Serikali Kuu kuendelea kuwa karibu na Serikali za Mitaa kwa kuwapatia watendaji wenye uwezo ili kuepusha kasoro hizo zilizojitokeza katika siku zijazo.

Mhe. Spika, kiujumla Kamati ya *LAAC* imezipokea na kuzifanyia kazi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upande wa Mashirika, Taasisi za Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na hatimae kuwasilisha ripoti yake kama Kanuni ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 inavyoelekeza.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba kuwashukuru Wajumbe wa Baraza hili kwa utulivu wao na kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha Maoni ya Kamati ya *LAAC* kuhusiana na Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upande wa Mashirika, Taasisi za Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, nawaomba wajumbe wako waitumie haki yao ya msingi iliyotolewa na Kanuni ya 43(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya kumuuliza maswali Mhe. Waziri husika juu ya ripoti hizi kwa lengo la kupata ufafanuzi zaidi.

Mwisho kabisa sio kwa umuhimu wake Mheshimiwa naomba niwapongeze wananchi wa Jimbo la Dimani kwa kunichagua mimi Mwakilishi ili niweze kuwakilisha vyema ndani ya Baraza hili. Nawapongeza sana na nawaambia nitafanya nao kazi bega kwa bega ili tuweze kuleta maendeleo ndani ya Jimbo la Dimani.
Mhe. Spika, naomba kuwasilisha ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC*. Ahsante waheshimiwa maoni haya ya *LAAC* ni balaa. (*Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa kwa kuwa Mhe. Waziri alipowasilisha kwa kweli aliwasilisha kwa zote tatu. Kwa hivyo, naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali *(PAC)* na yeye aje awasilishe maoni ya kamati yake. *(Makofi)*

**Mhe. Juma Ali Khatib (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali *(PAC):*** Ahsante nashukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa kutoa Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*) juu ya uwasilishaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wizara za SMZ kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Spika, sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake, ambae ametujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kukutana hapa leo, kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa leo nimesimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa mara ya kwanza nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*) na kamati yetu ndio inawasilisha hotuba yake kwa mara ya kwanza katika Baraza hili la Kumi, naomba kwa moyo mkunjufu kutoa pongezi nyingi kwa Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kwa zaidi ya asilimia 70 ya kura zote zilizopigwa na wananchi wa Zanzibar. Ushindi huo unaonesha wazi kwamba wananchi wa Zanzibar wana imani nae na wanamkubali awe kiongozi wao. Sasa wananchi wanafaidika na uamuzi walioufanya kwani kwa kiasi kikubwa mapato yameanza kuongezeka na uchumi wa nchi yetu unaendelea kuimarika kwa kasi kubwa. Aidha, namshukuru Mhe. Rais kwa kunichagua mimi kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza kwa dhati Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo na kwa namna anavyomsaidia Mhe. Rais kutekeleza shughuli za umma na kusimamia vyema utekelezaji wa shughuli za serikali. Kadhalika, nampongeza Makamu wa Kwanza wa Rais kwa heshima kubwa aliyopewa Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Rais kumsaidia katika utekelezaji wa majukumu mbali mbali ya serikali yetu.

Mhe. Spika, kadhalika naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kuzungumzia machache na ya umuhimu, yanayohusu uwasilishwaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2018/2019, kama ambavyo Kanuni ya 43(1) ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 inavyoelekeza.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha hapa Barazani ripoti hizi za ukaguzi za mwaka 2018/2019 ambazo ndizo nyenzo kuu za kazi za kamati zinazosimamia masuala ya fedha, ambapo katika utaratibu mpya wa hivi sasa zinajumuisha Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali *(PAC)* na Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika *(LAAC).*

Mhe. Spika, naomba kwa namna ya pekee, kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya *PAC* kwa kunichagua kwa kura zote zilizopigwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Ni dhahiri kuwa imani kubwa waliyoionesha kwangu imenipa faraja na nguvu za kutekeleza majukumu mazito ya kamati hii na kusimama kifua mbele katika Baraza lako tukufu kuwasilisha taarifa hii.

Vile vile, napenda kutoa pongezi na shukurani za dhati tena kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kwa umoja, ushirikiano, mshikamano na ari kubwa waliyoionesha wakati wote wa utekelezaji wa kazi za kamati ikiwa ni pamoja na kazi hii ya kuipitia, kuichambua na kuijadili taarifa hii. Ni ukweli usiopingika kuwa mashirikiano na moyo wao wa kujituma ndio chachu iliyoifanya kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wao, naomba kuwatambua kwa majina wajumbe na makatibu hao wa kamati yetu kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma Ali Khatib | - | Mwenyekiti. |
| 2. | Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma | - | Makamu Mwenyekiti. |
| 3. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Maryam Thani Juma | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Yussuf Hassan Iddi | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Haji Khatib Haji | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Said Khamis Ramadhan | - | Katibu |

Mhe. Spika, aidha nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa dhati viongozi na watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya za kufuatilia mapato na matumizi ya fedha za umma zinazotumika kwa shughuli mbali mbali za uendeshaji wa serikali. Ofisi hii imefanya kazi kubwa na nzito ya kufanya ukaguzi katika Mawizara na Taasisi mbali mbali za Serikali na kuandaa ripoti hizi kama ambavyo kifungu cha 112 cha katiba yetu kinavyoelezea.

Mhe. Spika, Kamati ya *PAC* inatambua na kuthamini sana kazi kubwa inayofanywa na ofisi hii katika kujenga nidhamu ya matumizi ya rasimali za umma katika serikali na kuimarisha misingi ya kidemokrasia ya utawala bora hapa nchini hasa ikizingatiwa kuwa taasisi za umma zimekuwa zikiongezeka ukilinganisha na miaka ya zamani.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya kuwepo kwa taasisi hizi za ukaguzi ni kuleta mabadiliko katika maisha ya wananchi kwa kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinazotumika kulingana na malengo yaliyowekwa na kuleta tija ilivyokusudiwa kwa wananchi. Aidha, kiwango cha kupima ni kwa kiasi gani Taasisi za Ukaguzi zinaleta mabadiliko katika maisha ya watu hutegemea sana mapato na mambo mengine, uwezo wa taasisi za ukaguzi, kuongeza uwajibikaji, uwazi na uadilifu kwa serikali na taasisi za umma.

Mhe. Spika, Mhe. Dkt Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alipolizindua Baraza hili la Kumi la Wawakilishi tarehe 11 Novemba, 2020 alisema kwamba, naomba kununukuu:-

> “Miongoni mwa mambo yanayodhoofisha Misingi ya Utawala Bora ni vitendo vya rushwa, uzembe, kukosa uwajibikaji, kutofuata Sheria na ukiukwaji wa maadili, vitendo vya rushwa na ufisadi vinavyowanyima haki wananchi na kuitia hasara serikali”.

Mhe. Spika, kuwepo kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hapa nchini kuna umuhimu mkubwa sana katika kusaidia kukomesha matumizi mabaya ya fedha za umma, uzembe, ufisadi na udanganyifu pamoja na ukiukwaji wa sheria na taratibu za nchi.

Mhe. Spika, sambamba na hilo, matumizi mazuri ya rasilimali fedha ni jambo la lazima iwapo serikali inataka kutoa huduma mbali mbali kwa wananchi wake. Hapo ndipo umuhimu wa

kuwepo kwa Kamati za Kusimamia Masuala ya Fedha katika Mabunge ya nchi mbali mbali duniani unapopatikana, kwani kamati hizi kupitia Ripoti za Ukaguzi ndizo zenye jukumu la kuhakikisha kuwa serikali zinakuwa na udhibiti mzuri wa matumizi ya fedha unaoambatana na usimamizi na utekelezaji bora wa sheria na taratibu za fedha na ununuzi pamoja na sheria nyengine zilizopo.

Mhe. Spika, naomba kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa ukaguzi hupima usahihi na usawa wa taratibu za utunzaji wa Hesabu za Taasisi za Serikali pamoja na taarifa za fedha zilizotolewa na taasisi hizo. Aidha, ukaguzi hupima kama fedha zilitumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo. Vile vile, ukaguzi huchambua uhalali wa gharama, ufanisi wa mbinu zilizotumika, viwango na ubora pamoja na ufanisi wa mipango ya serikali. Kiujumla hufikia malengo iliyojiwekea. Zaidi ya hayo, kwa kutoa Ripoti hizi za Ukaguzi kwa vyombo vinavyowakilisha wananchi kama hiki, Taasisi za Ukaguzi zinatoa fursa muhimu ya uwazi katika usimamizi na uendeshaji wa masuala ya fedha za serikali kwa umma.

Mhe. Spika, kutokana na dhima hiyo kubwa iliyopo katika kazi za ukaguzi na uchunguzi wa hesabu, Wajumbe wa Baraza lako Tukufu watakubaliana nami kuwa ukaguzi ni kazi ngumu inayohitaji moyo wa kujituma, uzalendo, uvumilivu, uadilifu, ujuzi, weledi na umakini mkubwa kwenye mambo yote yanayohusu ukaguzi. Aidha, kutokana na maendeleo mbali mbali yakiwemo ya sayansi na teknolojia, uchunguzi wa hesabu katika sekta ya umma kwa miaka ya hivi karibuni umekuwa ni wigo mpana zaidi ukilinganisha na miaka ya zamani, kutoka katika eneo la ukaguzi wa utii wa sheria na taratibu za fedha *(Compliance Audit)* na kuongezeka hadi katika maeneo mengi zaidi yakiwemo ya ukaguzi katika ufanisi *(Performance Audit),* ukaguzi wa thamani halisi ya fedha *(Value for Money Audit)* pamoja na ukaguzi katika mifumo na michakato ya udhibiti wa kifedha *(Audit of Systems and Processes of Financial Control)*.

Mhe. Spika, hivyo basi, kutokana na wigo huo mpana unaohusiana na masuala ya uchunguzi wa hesabu za serikali ni wazi kuwa kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara yakiwemo mafunzo ya mbinu na aina mbali mbali za ukaguzi kwa kamati hizi zinazosimamia masuala ya kifedha ni jambo la lazima na lisiloepukika, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kamati hizi. Kwa msingi huo Kamati ya *PAC* inaomba kusisitiza mambo yafuatayo:-

i. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iendelee kuzipatia kamati hizi mafunzo maalum kwa wakati yanayohusu Ripoti za Ukaguzi zinazowasilishwa katika Baraza lako Tukufu kabla ya ripoti hizo kufanyiwa kazi na kamati kama ambavyo ofisi hii ilivyokuwa ikifanya hapo awali. Kamati ya *PAC* inalisisitiza hili kwa mkazo mkubwa kwani ni jambo lisilo la kawaida kuona hivi sasa baadhi ya Ripoti za Ukaguzi za mwaka 2017/2018 zimeanza kufanyiwa kazi na kamati zetu bila ya Ofisi hii ya Mdhibiti kuzipatia mafunzo kamati hizi, ingawa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa jitihada zake iliwezesha kufanya mafunzo kwa kamati hizi na angalau zikaweza kufunua macho juu ya masuala mbali mbali ya kitaalamu. Mafunzo ya Ripoti za Ukaguzi ni muhimu sana kwa kuwa Ofisi ya Mdhibiti ndio inayofahamu kwa kina ufafanuzi wa hoja zilizomo katika ripoti hizi ambazo zinakwenda kushughulikiwa na kamati zetu.

ii. Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia bajeti yake yenye Programu Kuu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma, pale inapohitajika isisite kuwezesha

kufanyika mafunzo mbali mbali kwa kamati hizi yanayohusu usimamizi wa fedha za umma kama ilivyokuwa ikifanyika katika awamu iliyopita, hasa ikizingatiwa kuwa kamati hizi ni mpya na masuala ya usimamizi wa fedha za umma yanahusiana na maeneo mengi ya kitaalamu.

iii. Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ijipange vizuri zaidi katika kukuza maarifa na uwezo wa kamati hizi na kamati nyengine za Baraza ili jukumu la kuisimamia serikali liweze kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, leo hii Ripoti za Ukaguzi za Mwaka 2018/2019 zimewasilishwa hapa Barazani. Ikumbukwe kuwa baadhi ya Ripoti za Ukaguzi za Mwaka 2017/2018 ndio kwanza zimeanza kufuatiliwa na kamati hizi na ripoti nyengine za mwaka huo bado hazijaanza kushughulikIwa na kamati zetu. Aidha, naomba ifahamike kuwa Ripoti za Ukaguzi kama zinavyoonekana huwa zinasheheni mambo mengi makubwa ambayo huhitaji kufanyiwa kazi kwa kina na kwa umakini mkubwa.

Mhe. Spika, hivyo basi, Kamati ya *PAC* inaiomba ofisi yako kuzitengea muda wa kutosha kamati hizi za kusimamaia masuala ya fedha ili ziweze kuendana na kasi na wingi wa ripoti zinazohitaji kufanyiwa kazi na kuweza kufanya kazi zao kwa weledi na ufanisi mkubwa bila ya kuondosha njiani (kuripua).

Mhe. Spika, pamoja na kuwasilishwa kwa ripoti hizi hapa Barazani leo, takwimu na historia ya hivi karibuni inaonesha kuwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wamekuwa na kilio cha muda mrefu cha kutaka kuwasilishwa hapa Barazani Ripoti ya Ukaguzi ya Ofisi yenyewe ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kifungu cha 122 (4) na (5) cha Sheria ya Usimamaizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya Mwaka 2016 kinaelekeza kuwa angalau mara moja katika kila mwaka wa fedha, Hesabu za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zitakaguliwa na mtu atakayeteuliwa na waziri anayehusika na ofisi hii ya Mdhibiti. Aidha, waziri anayehusika na Ofisi hii ya Mdhibiti anatakiwa kuiwasilisha Barazani Ripoti ya Ukaguzi ya Ofisi ya Mdhibiti ndani ya miezi mitatu au angalau katika mkutano unaofuata wa Baraza baada ya kuipokea ripoti hiyo.

Mhe. Spika, naomba ieleweke kuwa kukaguliwa kwa Hesabu za Ofisi hii ni suala moja na kuwasilishwa hapa Barazani kwa ripoti hiyo ya Ukaguzi ya Ofisi hii ni suala jengine. Ukweli uliopo ni kuwa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu ya Ofisi ya Mdhibiti haijawasilishwa hapa Barazani kwa kipindi cha miaka mingi sasa.

Mhe. Spika, kutowasilishwa hapa Barazani kwa Ripoti ya Mkaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti sio tu kuvunja Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya Mwaka 2016, bali pia kumelifanya Baraza lako Tukufu kushindwa kupata kipimo cha uwajibikaji wa fedha wa ofisi hii muhimu katika nchi yetu *(Financial Accountability),* hivyo kuweza kuitia doa ofisi hii ambayo inapaswa kuwa kigezo chema na mfano bora kwa uadilifu, uwazi na uwajibikaji.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati ya *PAC* inamuomba Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kurekebisha dosari hiyo kwa kuwasilisha

hapa Barazani Ripoti ya Ukaguzi ya Ofisi ya Mdhibiti kama matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha yanavyoelezea.

Mhe. Spika, **s**ambamba na hilo, Kamati ya *PAC* imebaini kuwa kwa kipindi kirefu sasa Ripoti za Ukaguzi Yakinifu ya Miradi ya Mikubwa ya Serikali ikiwemo miradi ya ujenzi hazijawahi kuwasilishwa hapa Barazani. Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba ripoti ya mwisho ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyowasilishwa ilikuwa ni ripoti ya mwaka 2012/2013. Hali hii inaipa wasi wasi sana kamati hasa kwa kuwa fedha nyingi za umma zinaendelea kutumika katika miradi hiyo bila ya wasimamizi wa serikali kupata fursa ya kuzikagua kikamilifu.

Kwa mnasaba huo, Kamati inaiomba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya juhudi maalum kuhakikisha kuwa ukaguzi yakinifu wa miradi unakamilishwa na ripoti zake kuwasilishwa Barazani kama matakwa ya Katiba na Sheria inavyoelezea.

Mhe. Spika, tunapoiangalia taswira ya jumla na ya awali ya Ripoti ya Ukaguzi wa Mawizara ya SMZ ya mwaka 2018/2019 ambayo inayoihusu Kamati ya *PAC*, itabaini kuwa Wizara na Taasisi zote 65 zimepata hati zinazoridhisha katika matokeo yao ya ukaguzi, ingawa ilibainika dosari maeneo ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani, Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi, Uondoshaji wa Mali za Umma na Sheria ya Fedha za Umma pamoja na eneo la Usimamizi wa matumizi.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020, Kamati ya Kusimamia Masuala ya Fedha pamoja na mambo mengine ndio zenye jukumu la kuchunguza na kutoa taarifa juu ya Hesabu ya Mwaka wa Matumizi ya Fedha za Serikali na Hesabu nyengine zote zitakazojumuishwa mbele ya Baraza lako kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, kwa msingi huo, Kamati ya *PAC* ambayo ni moja ya Kamati ya Kusimamia Masuala ya Fedha, itaifanyia kazi ipasavyo Ripoti hii ya Ukaguzi wa Mawizara na hatimae kuwasilisha ripoti yake kwa kina hapa Barazani katika muda muafaka, kama Katiba na Sheria za nchi hii, pamoja na Kanuni za Baraza hili zinavyoelekeza.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba kuishukuru Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano mkubwa inayoipatia kamati yetu wakati wa kutekeleza majukumu yake ikiwemo utekelezaji wa kazi hii ya kuchambua na kutoa maoni ya kamati juu ya uwasilishwaji wa Ripoti hii ya Ukaguzi. Nawashukuru pia Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Spika, kwa pekee ambao sio kwa umuhimu sana lakini napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru viongozi wa chama changu cha *ADA-TADEA* kwa kuridhia uteuzi alioufanya Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuniteua mimi kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na chama changu kikaniruhusu na leo nimesimama hapa. Nawapongeza sana chama changu cha *ADA-TADEA.* Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe**. **Spika:** Ahsante Mheshimiwa, Waheshimiwa Wajumbe, nina orodha hapa ya Waheshimiwa Wajumbe ambao wanataka kuuliza maswali lakini sote ni mashahidi kwamba taarifa iliyosomwa ya *LAAC* hapa ina maswali mengi sana ambayo yanahitaji majibu na

nikichanganya na hayo ambayo nitayaruhusu. Sasa sidhani kama tutakuwa na muda wa kutosha wa waziri kuyajibu sasa hivi yote hapa. Nitaruhusu Mheshimiwa aende wakayajibu halafu tuletewe kwa maandishi yale maswali yanayohusika. Sasa nina watu sita ambao nitawapa kuuliza maswali na watumie muda mfupi tu kwa sababu ni kuuliza maswali halafu Mhe. Waziri atayachukua.

Wa kwanza ni Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, atafuatiwa na Mhe. Shaib Hassan Kaduara na Mhe. Rukia Omar Ramadhan ajiandae. Mhe. Shadya karibu.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Spika, niendelee tena kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi kwa mara nyengine tena ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri maswali kutokana na Hotuba ya Maoni ya Kamati ya *LAAC* yaliyosomwa muda mchache na Mwenyekiti wa kamati hiyo.

Mhe. Spika, maswali yangu mimi nitajikita sehemu mbili tu, Bima na *ZRB*. Mhe. Spika, kwa kuwa kifungu cha 112 (3) (c) cha Katiba ya Zanzibar cha mwaka 1984 kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi angalau mara moja kwa mwaka.

a) Je, ni kitu gani kilichopelekea Shirika la Bima kwa kipindi kirefu kutowasilisha Ripoti ya Mashirika makusanyo wanayokusanya.

b) Kwa vile shirika lilikuwa na mkurugenzi mwenye uelewa wa ukusanyaji wa mapato. Naomba kwa ufupi makusanyo yote kwa muda huo yalikuwa yakitumika vipi na kwa shughuli gani.

c) Swali la tatu kwa Shirika la Bima ambalo litakuwa la mwisho Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri aeleze Baraza lako Tukufu makusanyo na matumizi ya shughuli zilizofanywa kwa kipindi ambacho shirika halikuwasilisha ripoti zake ili wananchi waone ufanisi wa Shirika la Bima.

Mhe. Spika, naomba niende *ZRB*. Serikali zote duniani ili ziende sambamba na kasi ya uimarishaji wa hali za wananchi wake katika kupata huduma za kijamii. Mfano, elimu bora, afya, maji safi na salama. Lazima serikali ikusanye mapato na *ZRB* kwa vile ndio eneo muhimu la ukusanyaji wa mapato hapa nchini. Swali langu liko hivi wizara ilipitikiwa na nini kukiacha chombo hiki kutoleta ripoti yake tangu mwaka wa fedha 2013/2014 na kuwasilisha Barazani mwaka wa fedha 2016/2017.

Lakini la mwisho Mhe.Spika. Je, wananchi wa Zanzibar wataielewa vipi serikali yao katika upatikanaji wa huduma za kijamii, bila ya upatikanaji wa Ripoti ya Mapato kutoka Bodi ya Mapato. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante, sasa naomba nimwite Mhe. Shaib Hassan Kaduara, atafuatiwa na Mhe. Rukia Omar Ramadhan na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii adimu na adhimu. Mhe. Spika, naomba kwanza niwashukuru wananchi wa Jimbo la Chake Chake kwa kunichagua mimi ili niwe mwakilishi wao, nawaambia sitowaangusha.

Mhe. Spika, mimi kwanza naunga mkono Kamati ya *LAAC* na masuala yote ambayo yametolewa na Kamati ya *LAAC*. Mhe. Spika, mimi mwenyewe nimeridhika nayo, isipokuwa nina dogo tu. Mhe. Spika, mkabidhiwa nyumba kakataa nyumba huyo ana kauli yake anaitwa lakini sitaki nitoe katika Baraza lako hili.

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imempa mtu nyumba lakini akakataa nyumba na hatimae akatufanya Wazanzibari leo hii tunasumbuka kutokana na kupigwa kupitia mashirika haya na ndio maana Kamati ya *LAAC* ikaona matatizo haya. Kuna mashirika yanatumia, yanakusanya, yanatumia na *still* mahesabu yao hayawasilishwi. Mhe. Spika, hili ni kutukosea Wazanzibari. Lakini Mhe. Spika, ...

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa naomba usichangie, naomba uulize maswali.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Mhe. Spika, mimi nauliza hili, utoaji wa hati ambayo inatoka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Spika, hati hii anatumia kigezo gani, shirika limefanya vibaya lakini hatimae unakuta imepata hati iliyokuwa inaridhisha. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante, naomba nimwite sasa Mhe. Rukia Omar Ramadhan atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma  na Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir ajiandae.

**Mhe. Rukia Omar Ramadhan:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi niweze kumuuliza Mhe. Waziri maswali mawili kupitia Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kuweza kukutana jioni hii tena. Niwashukuru pia wananchi wa Jimbo la Amani kwa kuniamini ili niwe mwakilishi wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maswali yangu mawili, moja ni *ZRB* na jengine ni mradi ambao upo katika Uwanja wa Ndege wa Karume Unguja. *ZRB* ni Taasisi au Wakala wa Serikali katika kukusanya kodi na ina wataalam wazuri na mifumo mizuri.

Je, ni kwa nini *CAG* hajawahi kufanya ukaguzi na tathmini ya uwezo wa taasisi juu ya ukusanywaji wa mapato na kujua hali halisi ya uwezo wa taasisi katika ukusanyaji wa mapato.

Swali langu la pili linahusiana na Mradi wa Ufungaji wa Mashine za Ukaguzi Uwanja wa Ndege, ufungaji wa ukanda wa kusukuma mizigo *conveyance belt*. Je, ni kwa nini ripoti hizi hazikuonesha katika ukaguzi wake wakati tunajua utekelezaji wa bajeti ulifanyika katika mwaka 2018/2019. Mheshimiwa naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante, naomba sasa nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma atafuatiwa na Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir na Mhe. Omar Said Shaaban ajiandae.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza maswali Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, tangu Mhe. Waziri alipokuwa akisoma hii ripoti na yeye mwenyewe nilikuwa namuona kama anasikitika kwa sababu ripoti yenyewe inasikitisha na Mwenyekiti wa *LAAC* alipokuja yeye ndio akamaliza kabisa. Sasa na mimi maswali yangu naona yatakuwa sio mapya sana hapa Barazani kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, katika vikao vilivyopita vya Baraza la Wawakilishi kuna mjumbe mmoja wa Baraza la Wawakilishi lililopita aliwahi kuleta hoja binafsi ya kutaka kwamba mashirika yote ya serikali lazima yawasilishe taarifa zao za kila mwaka na mwalimu wangu Mhe. Haroun Ali Suleiman kipindi hicho bado alikuwa Mhe.Waziri wa Katiba na suala la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutokukaguliwa pia aliweza kuligusia na mpaka hii leo Wenyeviti wa Kamati ya *PAC* pamoja na *LAAC* wanaendelea kulalamikia hilo hilo.

Sasa Mhe.Waziri, labda uniambie kwamba kwa kuwa Baraza lililopita haya maswali hukuyapatia jawabu. Je, katika Baraza hili unatuahidi haya majawabu yataweza kupatikana au vipi.

Mhe. Spika, kwa sababu hizi ripoti zote zinazosomwa tunasoma sasa ripoti za viporo ingawa kuna lugha siku hizi huko mjini imeenea kufukua nini sijui sitaki kutaja huko. Lakini hii ripoti ina maana tunazungumzia taarifa ambazo hata tukizizungumza sasa hivi sitegemei kama zitaongezea mapato kwa taifa. Kwa sababu kwanza wao wenyewe Ofisa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekiuka katiba, Mashirika ya Umma yamekiuka katiba. Kwa sababu...

**Mhe. Spika:** Samahani Mheshimiwa, naomba usichangie, naomba uulize maswali.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, mimi swali langu lilikuwa ni moja zaidi kubwa. Je, hizi ripoti za mwaka 2014/2015/2016 tutaweza kuzipata vipi na hesabu ambazo za mwaka uliopita 2019/2020 tutazipata vipi, ili tunapokuja sasa kwenye bajeti tusije tukarejea kuendelea kujadili mambo ambayo sasa hivi sitegemei kama yataweza kutusaidia zaidi.

Lakini jengine swali la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyoshauriwa na Wenyeviti wote wa Kamati kwamba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali sasa hivi hakaguliwi. Kwa hiyo, tumependekeza au tunaomba kwamba sasa hivi kama wanavyofanya hayo mabunge mengine, aidha, Kamati ya *PAC* au tutafute chombo kingine chochote ambacho kitaweza kumkagua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa sababu hatuwezi kwamba yeye tunapokea ripoti yake kakagua wenzake wakati yeye vile vile hajakaguliwa. Sasa je, hili kwa mujibu wa sheria ipo tutafanya vipi ili kuhakikisha kwamba haya yote tunayaondoa. Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Spika:** Naomba kumwita sasa Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir atafuatiwa na Mhe. Omar Said Shaaban na Mhe. Suleiman Makame Ali ajiandae.

**Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir:** Ahsante Mhe.Spika, kwa kunipa nafasi hii nikushukuru sana lakini pia niwashukuru Baraza la Umoja wa Vijana Tanzania kwa kuweza kuniwakilisha hapa, lakini kwa upekee na shukrani za dhati Baraza la Umoja wa Vijana Mkoa wa Mjini.

Mhe. Spika, na mimi naomba kuuliza kuna miradi mingi ambayo illitekelezwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mfano wa miradi hiyo kama Mradi wa Zanzibar Salama na Mradi wa Kubadilisha Walimu wa *Art* kwenda Sayansi. Je, ni kwa nini miradi hiyo haijakaguliwa na kuletwa ripoti zake hapa Barazani juu ya utekelezaji wake pamoja na matokeo ya matumizi yake.

Lakini pia Mhe. Spika, naomba kujua ni kauli ipi ya serikali juu ya Idara hii ya Ukaguzi kwa kuzorotesha kila leo matokeo ya ukaguzi wa ndani. Ahsante Mhe.Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir, naomba sasa nimwite Mhe. Omar Said Shaaban atafuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe.Yussuf Hassan Iddi ajiandae.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi. Mhe. Spika, wakati wenyeviti wanawasilisha ripoti zao walieleza kwamba katiba ibara ya 112 ibara ndogo ya 7 inatuzuia kumhoji *CAG*. Lakini Mhe. Spika, katiba yetu ibara ya 5 (A) ibara ndogo ya 2 inaipa mamlaka Baraza lako Tukufu kuhoji mambo yote yanayohusiana na shughuli za umma kuuliza maswali ikiwa pamoja na ibara ya 88 ambayo inaeleza Kazi za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, lakini kinga anayowekewa *CAG*, *CAG* hawekewi kinga ya kuvunja katiba na mamlaka aliyopewa atekeleze ni ya kuvunja katiba ambayo tunayahoji hapa kwamba yamevunja katiba.

Swali ambalo nataka kuuliza Mhe. Spika, hata kama Baraza hatutamhoji *CAG* kwa kinga anayopewa 102 sisi tunaye waziri tunaweza kumuuliza, wetu sisi ni waziri. Swali ambalo mimi ningependa kuliuliza Mhe. Spika, waziri alikuwa wapi hajatekeleza wajibu wake wa kumsimamia *CAG* kama ambavyo anaruhusiwa na sheria. Ahsante.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Omar Said Shaaban, naomba sasa nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali ambaye atafuatiwa na Mhe.Yussuf Hassan Iddi.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kuna msemo unasema kama ni "zumari ya ukuti hii ishachauka". *(Vicheko)*

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri hususan kwenye wakaguzi wa ndani ambao wanajua sheria zote za ukaguzi katika ofisi zao na ilikuwa bado wanaendelea kuficha taarifa za ukaguzi kwa sababu ya hilo changa la macho ambalo walikuwa wameshalifanya.

Je, Mhe. Waziri na wakaguzi hawa nina imani bado wamo katika ofisi hadi leo hatua gani watachukuliwa za sheria kali ambazo kuhakikisha masuala hayo waliyoyafanya yasije yakajitokeza siku nyengine.

**Mhe. Spika:** Ahsante, kwa kumalizia sasa naomba nimwite Mhe. Yussuf Hassan Iddi.

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi:** Ahsante Mhe. Spika  kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Spika, Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2018/2019 ilibaini mapungufu katika mfumo wa ndani *internal control system*. Je, serikali imepanga vipi kuhakikisha kwamba inauimarisha mfumo huu wa *internal control system* ili mapungufu haya yaliyotokezea katika mwaka 2018/2019 yasijitokeze tena katika miaka inayokuja. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri ili kama kuna chochote. Mhe. Waziri tafadhali.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, niwashukuru wajumbe wote waliouliza maswali yao. Naomba kutokana na umuhimu wa kuyapatia uhakika maswali haya, basi *in shaa Allah* tukijaaliwa nipewe muda hadi kesho ili nikakae na watendaji tushauriane namna gani tulete jawabu za uhakika Barazani.

**Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe nihoji zote kwa pamoja kwamba tumezipokea, wale wanaokubali wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Marekebisho ya Jadweli ya Pili ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar Nam. 4 ya 2015**

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, samahani, hapa kuna kidude kinatutaabisha kidogo, na katika mazingira kama haya ndio kinazidi kututaabisha.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa hicho ni kwa ajili ya wale waheshimiwa wafupi kidogo, wewe mrefu unaweza ukasimama nje ya hicho, halafu ukaongea.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Sasa nikikaa hapa nitatanua miguu sana. *(Kicheko)*

**Mhe. Spika:** Naomba uendelee Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu Marekebisho ya Jadweli ya Pili ya Sheria Nam. 4 ya 2015.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanyia marekebisho Jadweli ya Pili inayohusiana na Fomu ya Tamko la Rasilimali na Madeni kwa mujibu wa kifungu cha 41(1) cha Sheria ya Maadili. Marekebisho haya yamefanyika ili kuwezesha Tume ya Maadili kukusanya

taarifa za ziada zanazohusiana na rasilimali na madeni ya viongozi wa umma ikilinganishwa na fomu inayotumika hivi sasa.

Mhe. Spika, marekebisho yaliyofanyika pia yanajumuisha muonekano wa jadweli yenyewe (*print out)* ambapo kwa kulinganisha na fomu ya tamko la sasa idadi ya kurasa zimepungua kutoka 28 hadi 17. Aidha, marekebisho hayo yamerahisisha zaidi ujazaji wa fomu ya tamko la mali na madeni.

**Marekebisho Yaliyofanyika**

Mhe. Spika, baada ya utangulizi wa hapo juu. Naomba sasa uniruhusu kuwasilisha marekebisho husika kama ifuatavyo.

Katika sehemu ya maelezo muhimu ambayo kiongozi anatakiwa kuyazingitia kabla ya kujaza fomu**.**

Kwanza, marekebisho yamefanyika kwa kuongeza kifungu nambari 9 chenye maneno "sehemu ya rasilimali za mume, mke au wake na watoto ijazwe na kiongozi wa umma kwa ajili ya mume, mke au watoto kadri ilivyo.

Pili, kifungu nambari 10 kimeongezwa maneno "ambatanisha maelezo ya muda wa miezi mitatu ya utoaji na uingizwaji wa fedha *(bank statement)* ya benki ulizozitaja".

Kifungu nambari 11 kimeongezwa maneno "fomu hii inapatikana katika Ofisi ya Tume ya Maadili zilizopo Unguja na Pemba". Aidha, unaweza kutumia kupitia tovuti hiyo hapo inaonesha wwwethicscommission.go.tz kwa kuifungua, kuijaza na kuichapisha kwa ajili ya kiapo na kuiwasilisha Ofisi ya Tume ya Maadili.
Pili, sehemu ya kwanza marekebisho yamefanyika kwa kuongeza kipengele cha nafasi nyengine na uteuzi, uongozi katika taasisi za umma na binafsi kwa sasa.

Tatu, sehemu ya pili marekebisho yamefanyika kwa kutenganisha taarifa za wadhifa, cheo, ajira, wakati wa kutoa tamko na taarifa za kiongozi kuhusu wadhifa, cheo na ajira zilizopita.

Nne, sehemu ya tatu marekebisho yamefanyika kwa kuongeza kipengele cha *account* ya benki zilizofungwa ndani kwa mwaka wa tamko, *account* ambazo hazitumiki, rasilimali, mapato ya biashara ya kiogozi, mke, mume, mke au wake ambazo zimesimamiwa na wakala wa kiongozi.

**Rasilimali na Mapato, Biashara Ambazo Kiongozi Mume, Mke au Wake Anazozisimamia**

Majumuisho mengine yamejumuisha taarifa za madeni anayodaiwa kiongozi kwa kuongeza vipengele vya jina la mhusika, kiongozi mume, mke, wake au watoto. Jina na anuani na wanaodai kiwango cha deni unachodaiwa, tarehe ya mwanzo ya mwisho wa deni, malipo kwa mwezi na bakaa hadi tarehe za kujaza fomu hiyo.

Mhe. Spika, kadhalika marekebisho yamefanyika katika taarifa ya madeni anayodai kiongozi kwa kuongeza vipengele vya jina la mhusika, kiongozi, mume, mke, wake au watoto, jina na

anuani na kiwango cha madeni unachodai, tarehe ya mwanzo na ya mwisho wa deni, malipo ya mwezi na bakaa hadi tarehe ya kujaza fomu hii.

Katika sehemu hii, marekebisho mengine yanajumuisha taarifa za rasilimali nyengine ambazo hazikuorodheshwa katika fomu hii. Zikiwemo jina la mhusika, kiongozi, mume, mke, wake au watoto, aina za rasilimali, gharama za ununuzi, mwaka wa kupatikana, mahali alipo, chanzo cha fedha na matumizi binafsi au biashara.

Marekebisho ya taarifa ya rasilimali ya mapato ya biashara za kiongozi mume, mke au wake ambazo zinasimamiwa na wakala wa kiongozi zenye vipengele jina la msimamizi wa mali, biashara na uhusiano, jina la mmiliki halisi kiongozi mume, mke, wake au watoto, aina ya mahali pa mali, biashara, muda wa uangalizi, thamani ya mali/mapato kwa mwaka, chanzo cha fedha, malipo na usimamizi kwa mwaka.

Marekebisho ya taarifa ya rasilimali ya mapato ya biashara za kiongozi, mume, mke au wake ambazo kiongozi anasimamia zenye vipengele, jina la msimamizi wa mali, biashara na uhusiano, jina la mmiliki halisi, kiongozi, mume na mke au watoto, aina ya mahali na mali, biashara, muda na uangalizi wa tathmini ya mali, mapato ya mwaka, chanzo na fedha na malipo ya usimamizi wa mwaka.

Sehemu ya nne ya marekebisho ya taarifa za mali zilizoongezwa na zilizotambuliwa ndani ya kipindi cha mwaka wa tamko kuanzia Januari hadi Disemba ikiwemo nyumba, gari, uwekaji hisa na kadhalika vimefanyiwa kwa vipengele vifuatavyo.

Jina la mmiliki, kiongozi mume, mke, wake au watoto, aina ya rasilimali, gharama na thamani ya uhaulishaji, mwaka wa uhaulishaji, mahali alipo, chanzo cha fedha, jina na anuani ya mhaulishaji.

Sehemu ya tano marekebisho yamefanyika kwa jadweli ndogo inayomhoji kiongozi kama amewahi kutuhumiwa kwa kukiuka Sheria za Maadili ya Viongozi wa Umma. Jadweli hiyo ndogo inamtaka kiongozi ajibu ndio au hapana kwa kuweka alama ya vyema. Pia aoneshe tuhuma za aina ya ukiukwaji na hatua zilizochukuliwa.

**Hitimisho**

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha marekebisho hayo, kwa ruhusa yako naomba uwaruhusu wajumbe wako waipitie, waijadili, hatimae waridhie marekebisho hayo ili kuwaruhusu viongozi wa umma kuanza kutumia rasmi fomu mpya ya rasilimali na madeni, Jadweli ya Pili Sheria Nam. 4 ya 2015, hivyo, kuwezesha Tume ya Maadili kuweza kukusanya taarifa zote zinazohitajika katika utekelezaji wa kazi zao. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri, Waheshimiwa sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ili aje atoe maoni ya kamati. Karibu mheshimiwa.

**Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Juu ya Taarifa ya Serikali Kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar, Nam. 4 ya 2015**

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Spika, sina budi kuchukua fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma na Mwenye kurehemu, Muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Mhe. Spika, pia, nachukua fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa, hali ambayo imeendelea kutupa nafasi Serikali na wananchi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Naomba kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla, tuendelee kudumisha kikamilifu amani na utulivu huo kwani bila ya amani hakuna maendeleo yatakayopatikana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kadhalika naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Zanzibar kwa kumchagua Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pili napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Welezo kwa kunichagua mimi kwa mara nyengine tena kuwa mwakilishi wao na kuwawakilisha katika Baraza hili tukufu.

Kadhalika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza na kuishukuru Kamati inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kunichagua mimi kuwa Mwenyekiti wao.
Mhe. Spika, aidha, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kutoa Maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Taarifa ya Serikali kuhusu Marekebisho ya Fomu ya Tamko la Mali na Madeni chini ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar, Nam. 4 ya 2015 ambapo marekebisho hayo yatawezesha kupatikana kwa taarifa zaidi za kiongozi ambazo hazikuwa zinapatikana katika fomu ya awali.

Mhe. Spika,Taarifa hiyo ya Serikali, inapendekeza kufanywa kwa marekebisho katika Jadweli la Pili kwa kulifuta na kuliweka badala yake Jadweli la Pili jipya ambalo linatokana na kifungu cha 41(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015 (kama ilivyorekebishwa na Sheria Nam. 1 ya 2018) ambacho kinampa nguvu na mamlaka Waziri kuweza kufanya marekebisho baada ya kuridhiwa na Baraza Tukufu la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje Wajumbe wanaounda Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Haji Jecha Salim | Katibu |
| 9. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 10. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Msaidizi wa Mjumbe |

Mhe. Spika, aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa viongozi na watendaji wote wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kazi zao nzuri na ngumu wanazozifanya katika kuhakikisha kuwa wanasimamia vyema haki na uadilifu wa Viongozi wa Umma Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati imeyapitia kwa kina mapendekezo hayo na haina pingamizi nayo kwa vile yamefuata taratibu zote zinazohusika.

Mhe. Spika, kamati yangu inawasisitiza viongozi wote wanaohusika kujaza na kuwasilisha fomu zao kwa wakati ili lengo la Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Serikali kwa ujumla liweze kufikiwa.

Mhe. Spika, kamati inaliomba Baraza lako Tukufu kuipokea na kuiunga mkono taarifa hii na inawaomba viongozi wote walioingizwa kwa kupitia marekebisho haya kuzingatia sheria.

Mhe. Spika, kwa niaba ya kamati hii naunga mkono hoja. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mwenyekiti wa hii kamati. Waheshimiwa Wajumbe sina maombi yoyote ya michango, naam. Nimehisi kama kuna mtu anataka kuchangia chochote hapa. Haya kwa vile hamna basi naomba nimwite Mhe. Waziri ili aje ahitimishe.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa siku ya leo kunipa nafasi hii kwa mara ya tano. Nashukuru vile vile, nimshukuru Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa maoni yao na ripoti yao.

Kwa ujumla, wametoa pongezi na sisi kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Tume hii ya Maadili ya Viongozi wa Umma tunapokea maoni hayo na tunashukuru kwa pongezi hizo.  Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante Waheshimiwa wajumbe, naomba niwahoji wale wote wanaoridhia marekebisho ya Jadweli ya Pili ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar Nam. 4 ya 2015 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa wajumbe, kabla hatujaelekea mwisho, naomba nitoe matangazo mawili. Tangazo la kwanza ni la taarifa ya msiba, tumepokea taarifa ya kufiwa na aliyekuwa Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi kwenye Baraza la Nane la Wawakilishi Mhe. Ali Aballa Ali ambaye alikuwa Mwakilishi wa Mfenesini na tumeambiwa kwamba maziko yatafanyika kesho saa nne asubuhi kwake Mfenesini.

Tangazo la pili linatoka kwa Mnadhim wa Chama cha Mapinduzi Barazani ambaye ameomba mara tu baada ya kumaliza kikao hichi anawaomba Wajumbe wote CCM wabaki humu ndani kuna jambo muhimu ambalo linataka kuzungumzwa. Baada ya matangazo hayo, naona bado tunao wakati, kama kuna chochote Katibu.

Ahsante, Waheshimiwa shughuli zote ambazo zimepangwa kwenye *order paper* zimekamilika. Kwa hivyo, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kushukuru sana na kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano ambayo tumeyapata leo hii, basi nichukue nafasi hii kuakhirisha shughuli za Baraza mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1:20 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 11/02/2021 saa 3:00 asubuhi)*